**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TAARIFA YA MIAKA 50 YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR
# 1964 - 2014

**APRILI, 2014**





*Bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

# MIPAKA YA UTAWALA TANZANIA




*Ramani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*




*Ramani ya Visiwa vya Unguja na Pemba*



MHESHIMIWA DKT. JAKAYA MRISHO KIKWETE

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



MHESHIMIWA DKT. ALI MOHAMED SHEIN
**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

## YALIYOMO

Orodha ya Majedwali na Michoro.........................................................x
Akronimu.......................................................................................xi
Tamko la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.............................xv
Tamko la Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi..........xix
Shukurani......................................................................................xxii
Sura ya Kwanza: Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar...........1
1.1 Utangulizi...................................................................................1
1.2 Historia Fupi ya Tanganyika na Zanzibar Kabla ya Muungano.........................................................................1
1.2.1 Historia ya Tanganyika.........................................................1
1.2.2 Historia ya Zanzibar..............................................................3
1.3 Ushirikiano kati ya Tanganyika na Zanzibar......................................5
1.3.1 Ushirikiano kabla ya Ukoloni.....................................................5
1.3.2 Ushirikiano wakati wa Ukoloni...................................................6
1.4 Uhusiano kati ya Muungano na Harakati za Umajumui wa Kiafrika......8
1.5 Matukio Muhimu Kuelekea Muungano wa Tanganyika na Zanzibar....10
1.6 Hatua Muhimu katika Kuundwa kwa Muungano..............................12
1.7 Chimbuko la Jina la Tanzania.......................................................15
1.8 Mipaka na Jiografia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...............16
1.9 Muundo na Mambo ya Muungano.................................................16
1.10 Mabadiliko katika Orodha ya Mambo ya Muungano..........................17
1.11 Mabadiliko ya Uongozi Mwaka 1964–2014.......................................18
Sura ya Pili: Utekelezaji na Mafanikio ya Muungano................................24
2.1 Utangulizi...................................................................................24
2.2 Sera, Mipango, Mikakati na Programmu Mbalimbali za Utekelezaji wa Mambo ya Muungano.........................................24
2.2.1 Maendeleo ya Uchumi mwaka 1961-1966....................................24
2.2.2 Maendeleo ya Uchumi mwaka 1967-1985....................................26
2.2.3 Sera, Mipango na Maendeleo mwaka 1985-2013.........................28
2.2.4 Urekebishaji wa Mashirika ya Umma..........................................29
2.2.5 Dira ya Maendeleo...................................................................31
2.2.6 Programu na Mikakati Mingine ya Maendeleo.............................31

2.2.7 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana....32
2.2.8 Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wanawake....32
2.2.9 Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Mauzo Nje....33
2.2.10 Mfuko wa Kudhamini Mabenki na Taasisi za Fedha....33
2.2.11 Mifuko ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi....33
2.3 Utekelezaji wa Mambo ya Muungano....33
2.3.1 Katiba, Bunge na Utawala Bora....33
2.3.2 Ulinzi na Usalama....41
2.3.3 Diplomasia na Ushirikiano wa Kimataifa....50
2.3.4 Masuala ya Kiuchumi ya Muungano....55
2.3.5 Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu....69
2.3.6 Usafiri wa Anga....70
2.3.7 Takwimu....72
2.3.8 Elimu ya Juu....74
2.3.9 Uchangiaji Gharama za Elimu ya Juu....77
2.3.10 Usimamizi wa Mitihani....78
2.3.11 Utafiti....79
2.3.12 Utabiri wa Hali ya Hewa....81
2.3.13 Huduma za Posta na Simu....83
2.4 Mambo ya Muungano kwa Mujibu wa Sheria....85
2.4.1 Tume ya Taifa ya Uchaguzi....85
2.4.2 Udhibiti wa Fedha Haramu....87
2.4.3 Mawasiliano Tanzania....88
2.4.4 Huduma za Bandari....89
2.5 Ushirikiano katika Mambo Yasiyo ya Muungano....90
2.5.1 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania....92
2.5.2 Ndege za Serikali....94
2.6 Mafanikio ya Muungano....94
2.6.1 Mafanikio ya Kisiasa....95
2.6.2 Mafanikio ya Kiuchumi....98
2.6.3 Mafanikio ya Ulinzi na Usalama....100
2.6.4 Mafanikio ya Kijamii....101

2.6.5 Mafanikio katika Sayansi na Teknolojia....................................103
Sura ya Tatu: Changamoto za Muungano..........................................105
3.1 Utangulizi............................................................................105
3.2 Changamoto za Ujumla.........................................................105
3.2.1 Kisiasa......................................................................105
3.2.2 Kiuchumi....................................................................106
3.2.3 Ulinzi na Usalama.......................................................108
3.2.4 Kijamii.......................................................................110
3.2.5 Sayansi, Teknolojia na Utafiti.......................................111
3.3 Changamoto Mahususi za Muungano..........................................112
3.3.1 Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora....................................................................112
3.3.2 Uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu......................112
3.3.3 Utekelezaji wa Sheria ya Usafiri wa Majini................................113
3.3.4 Mgawanyo wa Mapato ya Misaada na Uwezo wa Zanzibar Kukopa.........................................................................113
3.3.5 Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa SMT..................................113
3.3.6 Kodi Nyinginezo.....................................................................114
3.3.7 Ongezeko la Gharama za Umeme..........................................114
3.3.8 Wafanyabiashara wa Zanzibar Kutozwa Kodi mara Mbili............114
3.4 Changamoto Mahususi zinazotafutiwa ufumbuzi............................115
3.4.1 Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki............115
3.4.2 Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia........................115
3.4.3 Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Kimataifa........................115
3.4.4 Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano....116
3.4.5 Usajili wa Vyombo vya Moto.................................................116
3.4.6 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha.......116
Sura ya Nne: Fursa na Matarajio ya Muungano kwa Miaka Ijayo...........117
4.1 Utangulizi............................................................................117
4.2 Fursa..................................................................................118
4.3 Matarajio.............................................................................120
Hitimisho.................................................................................123

# Orodha ya Majedwali na Michoro

## A: MAJEDWALI


Jedwali 1: Uhimilivu wa Deni la Nje kwa Mwaka 2012.............................64

Jedwali 2: Mchango wa Uvuvi wa Bahari Kuu katika Pato la Taifa kwa Mwaka 2009/10-2012/13....................................................70

Jedwali 3: Mwenendo wa Ajali na Matukio katika Usafiri wa Anga kwa Mwaka 2004-2012..............................................................72

Jedwali 4: Udahili wa Wanafunzi kwa Programu Mbalimbali Kuanzia Mwaka 2009/10 - 2013/14..............................................................76

Jedwali 5: Matokeo ya Uchaguzi wa Rais Kuanzia Mwaka 1995 hadi 2010....................................................................86

Jedwali 6: Muhtasari wa Miradi ya Jamii Iliyotekelezwa na TASAF katika Awamu ya Pili...................................................................93


## B: MICHORO


Mchoro Na. 1: Mgawanyo wa Wabunge wa Kuchaguliwa 2010.................39

Mchoro Na. 2: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato Kuanzia Mwaka 1996/97-2012/13..........................................................56

Mchoro Na. 3: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Tanzania Bara Kuanzia Mwaka 1970-2013.........................................................62

Mchoro Na. 4: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar Kuanzia Mwaka 2001-2013.................................................................63

Mchoro Na. 5: Mwenendo wa Thamani ya Mauzo Nje Kuanzia Mwaka 1963-2012.................................................................67

Mchoro Na. 6: Mwenendo wa Ongezeko la Idadi ya Watu Tanzania Kuanzia Mwaka 1965-2012.........................................................74

# Akronimu

| | | |
|---|---|---|
| **AA** | - | African Association |
| **AFP** | - | African Farmers Party |
| **ANC** | - | African National Congress |
| **ASDP** | - | Agriculture Sector Development Programme |
| **ASP** | - | Afro-Shirazi Party |
| **ATC** | - | Air Tanzania Corporation |
| **ATM** | - | Automated Tellering Machine |
| **BBU** | - | Bukoba Bahaya Union |
| **BET** | - | Board of External Trade |
| **BHESCO** | - | Building, Hardware and Electrical Supplies Company |
| **BIT** | - | Board of Internal Trade |
| **BIZANJE** | - | Shirika la Biashara za Nje |
| **BRELA** | - | Business Registration and Licensing Agency |
| **CAADP** | - | Comprehensive Africa's Agriculture Development Programme |
| **CCM** | - | Chama Cha Mapinduzi |
| **CFC** | - | Common Fund for Commodities |
| **CFT** | - | Crash Fire Tender |
| **CHADEMA** | - | Chama Cha Demokrasia na Maendeleo |
| **CHAUSTA** | - | Chama Cha Haki na Ustawi Tanzania |
| **COMESA** | - | Common Market for Eastern and Southern Africa |
| **CUF** | - | Civic United Front |
| **DCA** | - | Directorate of Civil Aviation |
| **DITF** | - | Dar es Salaam International Trade Fair |
| **DP** | - | Democratic Party |
| **DRC** | - | Democratic Republic of Congo |
| **EACSO** | - | East African Common Services Organisation |
| **EAMD** | - | East African Meteorological Department |
| **EAPTC** | - | East African Posts and Telecommunication Corporation |
| **EASSy** | - | Eastern Africa Submarine Cable System |
| **ECOWAS** | - | Economic Community of West African States |
| **EPOCA** | - | Electronic and Postal Communications Act |
| **EWURA** | - | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| **FIU** | - | Financial Intelligence Unit |
| **FORD** | - | Forum for the Restoration of Democracy |

| | | |
|---|---|---|
| **FRELIMO** | - | Frente de Liberracao de Mozambique (Liberation Front of Mozambique) |
| **FTA** | - | Free Trade Area |
| **GAPEX** | - | General Agricultural Products Export Company |
| **GPO** | - | General Postal Office |
| **HOSCO** | - | Household Supplies Company |
| **IDM** | - | Institute of Development Management |
| **IMO** | - | International Maritime Organization |
| **IMS** | - | Institute of Marine Sciences |
| **IOC** | - | Indian Ocean Commission |
| **IOTC** | - | Indian Ocean Tuna Commission |
| **JKT** | - | Jeshi la Kujenga Taifa |
| **JKU** | - | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| **JLU** | - | Jeshi la Ugombozi |
| **JWTZ** | - | Jeshi la Wananchi wa Tanzania |
| **KCB** | - | Kenya Commercial Bank |
| **KMKM** | - | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo |
| **KNCU** | - | Kilimanjaro Natives Cooperative Union |
| **KNPA** | - | Kilimanjaro Native Planters Association |
| **MACEMP** | - | Marine and Coastal Environmental Management Programme |
| **MFT** | - | Municipal Fire Tender |
| **MKUKUTA** | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| **MKUZA** | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar |
| **MPLA** | - | Movimento Popular de Liberracao de Angola |
| **MTAKULA** | - | Mpango wa Kujitosheleza kwa Chakula |
| **NAFCO** | - | National Food Corporation |
| **NCCR** | - | National Convention for Construction and Reform |
| **NEPAD** | - | New Partnership for Africa's Development |
| **NGOMAT** | - | Ngoni-Matengo Cooperative Union Ltd |
| **NICTBB** | - | National Information and Communication Technology Broadband Backbone |
| **NIDA** | - | National Identification Development Authority |
| **NLD** | - | National League for Democracy |
| **NMC** | - | National Milling Corporation |
| **NPSS** | - | Nationalist Party of the Sultan's Subjects |

| | | |
|---|---|---|
| **NRA** | - | National Reconstruction Alliance |
| **OAU** | - | Organization of African Unity |
| **PAC** | - | Pan Africanist Congress |
| **PAFMECA** | - | Pan-African Freedom Movement of Eastern and Central Africa |
| **PAYE** | - | Pay As You Earn |
| **PBZ** | - | People's Bank of Zanzibar |
| **PONA** | - | Popular National Alliance |
| **PSA** | - | Production Sharing Agreement |
| **PTA** | - | Preferential Trade Area |
| **RETCO** | - | Regional Transport Companies |
| **RIV** | - | Rapid Intervention Vehicle |
| **RORO** | - | Roll on Roll off |
| **SA** | - | Shiraz Association |
| **SACCOS** | - | Savings and Credit Cooperative Societies |
| **SADC** | - | Southern Africa Development Community |
| **SAU** | - | Sauti ya Umma |
| **SELF** | - | Small Entrepreneur Loan Facility |
| **SMT** | - | Serikali ya Muungano wa Tanzania |
| **SMZ** | - | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| **SUMATRA** | - | Surface and Marine Transport Regulatory Authority |
| **SWAPO** | - | South West Africa People's Organization |
| **SWIOFC** | - | South West Indian Ocean Fisheries Commission |
| **TAA** | - | Tanganyika African Association |
| **TADEA** | - | Tanzania Democratic Alliance |
| **TAFIRI** | - | Tanzania Fisheries Research Institute |
| **TAFSIP** | - | Tanzania Food Security and Investment Plan |
| **TANESCO** | - | Tanzania Electricity Supply Company |
| **TANTRADE** | - | Tanzania Trade Development Authority |
| **TANU** | - | Tanganyika African National Union |
| **TASAF** | - | Tanzania Social Action Fund |
| **TAZARA** | - | Tanzania Zambia Railway Authority |
| **TBC** | - | Tanzania Broadcasting Commission |
| **TBL** | - | Tanzania Breweries Limited |
| **TCAA** | - | Tanzania Civil Aviation Authority |
| **TCC** | - | Tanzania Communication Commission |
| **TCF** | - | Trillion Cubic Feet |
| **TEHAMA** | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |

| | | |
|---|---|---|
| **TFL** | - | Tanganyika Federation of Labour |
| **TIB** | - | Tanzania Investment Bank |
| **TLP** | - | Tanzania Labour Party |
| **TPA** | - | Tanzania Ports Authority |
| **TPC** | - | Tanzania Posts Corporation |
| **TPC** | - | Tanganyika Plantation Company |
| **TPDC** | - | Tanzania Petroleum Development Corporation |
| **TPP** | - | Tanzania Peoples Party |
| **TPTC** | - | Tanzania Posts and Telecommunication Corporation |
| **TRA** | - | Tanzania Revenue Authority |
| **TRDB** | - | Tanzania Rural Development Bank |
| **TTCL** | - | Tanzania Telecomunications Limited |
| **UDP** | - | United Democratic Party |
| **UMD** | - | Union for Multiparty Democracy |
| **UPDP** | - | United Peoples Democratic Party |
| **UPU** | - | Universal Postal Union |
| **UTP** | - | United Tanganyika Party |
| **VFCU** | - | Victoria Federation of Cooperative Unions |
| **YOU** | - | Youth Own Union |
| **ZAFREZA** | - | Zanzibar Free Zone Authority |
| **ZANU** | - | Zimbabwe African National Union |
| **ZECO** | - | Zanzibar Electrical Corporation |
| **ZFPA** | - | Zanzibar Free Port Authority |
| **ZIPA** | - | Zanzibar Investment Promotion Authority |
| **ZMA** | - | Zanzibar Maritime Authority |
| **ZNP** | - | Zanzibar Nationalist Party |
| **ZPC** | - | Zanzibar Ports Corporation |
| **ZPPP** | - | Zanzibar and Pemba People's Party |
| **ZRB** | - | Zanzibar Revenue Board |
| **ZSTC** | - | Zanzibar State Trading Corporation |

# Tamko la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Tarehe 26 Aprili ya kila mwaka ni muhimu katika historia ya Tanzania kwani ni siku ambayo Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ziliungana na kuwa nchi moja, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tarehe 26 Aprili, 2014, tunaadhimisha kwa namna ya pekee Jubilei ya Muungano wetu kutimiza miaka 50 tangu ulipoasisiwa. Hivyo, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijalia nchi yetu na watu wake kuifikia siku hii.

Muungano wa Tanzania umejengeka katika misingi ya historia ya uhusiano wa damu, harakati za pamoja na ushirikiano wa Vyama vya Ukombozi vya Zanzibar na Tanganyika katika kupigania uhuru. Ninawashukuru Waasisi wetu wa Muungano, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, ambao waliendeleza uhusiano huo uliowezesha kurasimisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Tunapoadhimisha Miaka 50 ya Muungano, tuna kila sababu ya kukumbuka, kutathmini na kuweka mwelekeo wa masuala muhimu yaliyokusudiwa na Waasisi wetu ambao walitia saini Hati ya Makubaliano ya Muungano kwa niaba ya wananchi wa nchi hizo mbili. Pamoja na Waasisi wetu kutangulia mbele ya haki, msingi waliotuachia umeendelea kuimarisha umoja, amani, na utulivu wa Taifa letu. Tumuombe Mwenyezi Mungu awapumzishe mahali pema. Amina!

Muungano huu umedumu kutokana na dhamira za dhati za umoja waliokuwa nao Waasisi wake, sera sahihi za Serikali zote mbili za TANU na ASP na sasa CCM, jitihada zinazoendelezwa na viongozi waliofuatia baada ya Waasisi pamoja na kuungwa mkono na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zaidi ya yote, utamaduni wa kukaa na kuzungumzia changamoto kila zinapojitokeza na kuzitatua kwa pamoja kwa kuzingatia misingi ya umoja na mshikamano vimeimarisha na kuufanikisha Muungano wetu.

Katika kipindi cha miaka 50 ya Muungano, tumeshuhudia mafanikio makubwa ya kujivunia kwani ni Muungano wa kipekee uliodumu kati ya majaribio kadhaa ya nchi za Afrika ya kutaka kuungana.  Watanzania wamejenga umoja, misingi endelevu ya udugu baina yao, mambo ambayo yanaonesha

kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unaendelea kuimarika. Kwa kutumia umoja huo, wananchi na viongozi wao wametumia busara na hekima kuhakikisha kwamba uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar vinaenziwa. Vilevile, pande mbili za Muungano zimejenga wigo wa kuendesha Serikali zake kwa uwazi chini ya misingi ya demokrasia na utawala bora. Misingi hiyo imeimarika kutokana na uelewa mzuri wa dhana ya uwajibikaji kwa viongozi wa ngazi zote.

Uchumi umekua kwa kasi ya kuridhisha, kipato cha mwananchi mmoja mmoja kimeongezeka na mfumuko wa bei umedhibitiwa. Aidha, tumeshuhudia kuimarika kwa miundombinu mbalimbali, hususan barabara na huduma za jamii.  Pia, tumeendelea kutumia maliasili zetu vyema zaidi kwa manufaa ya wananchi wetu kuliko hali ilivyokuwa kabla ya kuungana mwaka 1964. Mafanikio haya yametokana na usikivu, utulivu, moyo wa kujituma na kujitolea na ushirikiano wa dhati wa viongozi na wananchi. Hata hivyo, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, tumekumbana na changamoto ambazo kwa ujasiri mkubwa tumekabiliana nazo kwa kushirikiana na wananchi. Ni matarajio yangu kuwa, tutaendelea kuuenzi, kuuimarisha Muungano wetu na kukuza ushirikiano uliopo ili kujiletea maendeleo yatakayoifanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati katika miaka ya 2020.

Nachukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Viongozi wote walio hai na waliotangulia mbele ya haki ambao wameongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu kuasisiwa kwake mwaka 1964.  Kwanza nawashukuru kwa dhati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Awamu ya Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1964–1985); Mheshimiwa Alhaji Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1985-1995) na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1995-2005).

Vilevile, ninawashukuru Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Sheikh Abeid Amani Karume (1964-1972); Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi (1972-1984); na Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi (1984-1985).

Pia, ninawashukuru Makamu wa Pili wa Rais na Mawaziri Wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa (1964-1977); Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine (1977-1980 na 1983-1984); Mheshimiwa Cleopa David Msuya (1980-1983) na Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim (1984-1985).

Aidha, ninawashukuru Makamu wa Kwanza wa Rais na Mawaziri Wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Pili: Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba (1985-1990); Mheshimiwa John Samwel Malecela (1990-1994) na Mheshimiwa Cleopa David Msuya (1994-1995). Vilevile, ninawashukuru Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mheshimiwa Idris Abdulwakil Nombe (1985-1990) na Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma (1990-1995).

Pia, ninawashukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Tatu na Nne: Mheshimiwa Dkt. Omari Ali Juma (1995-2001); Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein (2005-2010) na Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal (2010 hadi sasa). Vilevile, Mawaziri Wakuu wa Awamu ya Tatu na Nne: Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye (1995-2005); Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa (2005-2007); na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (2007 hadi sasa).

Ninawashukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma (1995-2000); Mheshimiwa Amani Abeid Amani Karume (2000-2010); na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein (2010 hadi sasa).

Pia ninawashukuru wananchi kwa moyo wao wa kujitolea katika kulijenga Taifa letu. Vilevile, nawashukuru Washirika wa Maendeleo kwa mchango wao mkubwa katika kuunga mkono jitihada za kuleta maendeleo ya Taifa letu. Kwa namna ya pekee, nazipongeza Kamati Tendaji ya Maandalizi ya Maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano na Kamati Maalum iliyoandaa taarifa hii. Ni imani yangu kuwa taarifa hii itakuwa rejea muhimu kwa vizazi vya nchi yetu na nchi nyingine duniani kwa miaka mingi ijayo.

Mwisho, ninawatakia Watanzania wote kila la kheri na baraka tele katika kuadhimisha Miaka 50 ya Muungano. Ninawatakia mwanzo mwema wenye furaha na fanaka tele katika miaka ijayo ya Muungano wetu.

**UTANZANIA WETU NI MUUNGANO WETU;**
**TUULINDE, TUUIMARISHE NA KUUDUMISHA.**

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA.**

DKT. JAKAYA MRISHO KIKWETE
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

## Tamko la Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Tunapoadhimisha miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kuna kila sababu ya kuwakumbuka na kuwaenzi waasisi wa Taifa letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume. Ni ukweli usiofichika kwamba, Muungano wetu ambao msingi wake ni historia ya karne nyingi ya ushirikiano wa watu wa pande mbili na hatimaye kurasimishwa na waasisi wetu hao mwaka 1964 umezidi kuimarika na kuenziwa.

Kipindi cha miaka 50 ya Muungano wetu kimeshuhudia Awamu Nne za uongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Awamu Saba za Zanzibar. Viongozi wote wa awamu zilizopita waliupa Muungano wetu uzito mkubwa kwa kuimarisha ushirikiano kisiasa, kiuchumi na kijamii. Aidha, viongozi waliopo sasa wanaendeleza juhudi za kuimarisha Muungano wetu kwa ujasiri na umahiri mkubwa. Umakini na weledi wa viongozi wetu hao umeifanya nchi yetu kuwa ya amani na utulivu na hivyo kupata sifa kubwa kimataifa. Mifumo imara iliyowekwa ya kujadili na kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zilizoukabili Muungano wetu imewezesha pande zote za Jamhuri ya Muungano kupiga hatua kubwa sana za maendeleo katika masuala ya Muungano na hata yale ambayo si ya Muungano.

Mafanikio makubwa yamepatikana ndani ya kipindi cha miaka 50 ya Muungano wetu. Tunajivunia kuwa na jamii yenye umoja na mshikamano na isiyo na ubaguzi wa aina yoyote. Watu wa pande zote za Muungano wanaishi na wanafanya kazi zao za kujiletea maendeleo katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ya tatizo lolote. Uchumi wetu unaendelea kuimarika na matokeo yake ni kuimarika na kuongezeka kwa miundombinu mbalimbali na huduma za jamii. Demokrasia imepanuka zaidi na vipato vya wananchi wetu vinazidi kuongezeka na wananchi wengi zaidi wamepata maisha yaliyo bora zaidi. Aidha, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ambayo ni msingi muhimu wa kuimarisha uchumi na maendeleo katika dunia ya leo nayo imeimarishwa kwa kiwango kikubwa.

Mafaniko hayo yanapatikana kutokana na ushirikiano mzuri kati ya viongozi na wananchi wa pande zote za Muungano. Mafanikio haya siyo ya kubezwa hata kidogo na yanahitaji kulindwa, kudumishwa na kuendelezwa kwa nguvu zote. Kwa hivyo, ni wajibu wa kila Mtanzania kuhakikisha kuwa anaulinda, anauenzi na anaudumisha Muungano wetu. Natoa wito kwa Watanzania kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa ili tukuze zaidi uchumi wetu, tuongeze kipato na hatimaye tufikie lengo la kuwa nchi ya kipato cha kati katika miaka michache ijayo. Ni matumaini yangu kwamba, misingi imara ya amani na utulivu iliyopo, rasilimali watu, maliasili na vivutio vya utalii ni fursa zinazoweza kuleta maisha bora zaidi kwa kila Mtanzania ikiwa kila mmoja wetu atatimiza wajibu wake ipasavyo.

Natoa shukurani zangu za dhati kwa viongozi wote walioongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar kwa vipindi mbalimbali. Kazi nzuri zilizofanywa na viongozi hao ndizo zimetuwezesha kufikia hapa tulipo. Kwa namna ya pekee namshukuru Rais wa Awamu ya Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uongozi wake mahiri ambao umezifanya pande mbili za Muungano kuwa karibu zaidi, kushirikiana kwa udugu wa hali ya juu na hivyo kuufanya Muungano wetu kuwa imara zaidi na zaidi kila siku. Aidha, namshukuru kwa kuanzisha na kuongoza Mchakato wa kupatikana Katiba Mpya. Ni imani yangu kwamba hatimaye tutapata Katiba Mpya itayoufanya Muungano wetu kuwa imara zaidi; na nchi yetu kuendelea kuwa ya amani na utulivu, yenye mshikamano na umoja; na itakayowafanya wananchi wetu kuwa wamoja zaidi.

Mwisho nawashukuru Viongozi na Watendaji wa ngazi mbalimbali kutoka pande zote za Muungano na wananchi wote kwa jumla kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuliletea maendeleo Taifa letu. Nawatakia kila la kheri na mafanikio katika kuadhimisha miaka 50 ya Muungano wetu.

**UTANZANIA WETU NI MUUNGANO WETU;**
**TUULINDE, TUUIMARISHE NA KUUDUMISHA.**

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA**

DKT. ALI MOHAMED SHEIN
**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

# Shukurani

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatimiza miaka 50 tangu kuasisiwa kwake tarehe 26 Aprili, 1964. Taarifa hii inatoa historia ya Muungano, utekelezaji wa Mambo ya Muungano, mafanikio, changamoto, fursa na matarajio ya Muungano kwa miaka ijayo.

Kazi ya kuandaa Taarifa hii iliyohusisha viongozi na watendaji wa ngazi mbalimbali za Serikali kutoka pande zote za Muungano haikuwa rahisi hata kidogo. Tunatambua michango ya hali na mali iliyotolewa katika kufanikisha jukumu hilo la kihistoria. Kutokana na hali hiyo, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Watendaji Wakuu wa Serikali zote mbili, Watumishi wote wa Serikali na wadau wengine kwa kushiriki na kufanikisha maandalizi ya taarifa hii.

Ofisi yangu inatoa shukrani za pekee kwa Ofisi ya Rais, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar; Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Naishukuru pia Kamati Tendaji ya Maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano, Kikosi Kazi na Kamati Maalum iliyoandaa Taarifa hii. Aidha, natoa shukurani zangu za dhati kwa Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuratibu zoezi la uandishi wa taarifa hii.

Ninatoa wito kwa wananchi na viongozi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza wajibu wa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, ninapenda kuwakumbusha Watanzania kuwa, tunalo jukumu la kuuenzi na kuuendeleza Muungano kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

**"UTANZANIA WETU NI MUUNGANO WETU;**
**TUULINDE, TUUIMARISHE NA KUUDUMISHA".**

Dkt. Mohamed Gharib Bilal
**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

## 1.1 Utangulizi

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umetokana na historia ndefu ya ushirikiano wa kidugu na ya kiharakati katika nyanja za uchumi, utamaduni na siasa baina ya watu wa Tanganyika na Zanzibar. Historia hiyo ya ushirikiano baina ya wananchi, na mahitaji mahususi ya kisiasa na kiuchumi baada ya kuondokana na utawala wa kikoloni, ndiyo iliyotoa msukumo kwa viongozi wakuu wa nchi hizo, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, kuasisi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Aprili, 1964. Hatua hiyo iliungwa mkono na wananchi wa pande zote mbili. Aidha, ari ya kuwaunganisha watu wa Tanganyika na Zanzibar iliongezeka kutokana na chachu ya harakati za Umajumui wa Kiafrika (Pan-Africanism) zilizokuwa zikiendeshwa na viongozi wengi wa kiafrika duniani, na kupamba moto zaidi baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Lengo la harakati za Umajumui wa Kiafrika lilikuwa kuwaunganisha Waafrika kote duniani kwa nia ya kutokomeza dhuluma dhidi ya Waafrika zilizoanza tangu enzi ya biashara ya utumwa. Vilevile, matukio kadhaa yaliyotokea Tanganyika na Zanzibar mara baada ya uhuru kutoka kwa watawala wa Kiingereza yalitoa msukumo kwa Waasisi wa Muungano kutekeleza azma hiyo bila kuchelewa. Kabla ya kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watu wa Tanganyika na Zanzibar walikuwa na historia ambazo kwa kiasi kikubwa zilifanana. Kufanana huko kwa historia za watu wa nchi hizi mbili ni sababu mojawapo iliyowafanya Watanganyika na Wazanzibari kuunga mkono kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 1.2 Historia Fupi ya Tanganyika na Zanzibar Kabla ya Muungano

### 1.2.1 Historia ya Tanganyika

Kihistoria, eneo la Tanganyika linaaminika kuwa chimbuko la binadamu duniani kutokana na kugunduliwa kwa nyayo za binadamu wa kale katika Bonde la Oltupai (Olduvai) lililopo katika eneo la Mbuga ya Wanyama ya Serengeti. Kabla ya ujio wa wakoloni, jamii nyingi za Tanganyika zilitegemea

zaidi kilimo cha mazao katika kujikimu. Shughuli nyingine muhimu za kiuchumi zilikuwa uvuvi, ufugaji na uwindaji. Kufikia mwaka 1884, wakati Wajerumani walipoanza harakati za kuifanya sehemu hii ya Afrika kuwa koloni lao, kulikuwa na makabila zaidi ya 120 katika eneo la Tanganyika. Tanganyika ilitawaliwa na Wajerumani kuanzia mwaka 1884 hadi mwishoni mwa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia iliyodumu kuanzia mwaka 1914 hadi 1918.

Wakati wa uanzishwaji wa utawala wa kikoloni, Watanganyika wakiongozwa na viongozi wao walipambana dhidi ya wavamizi ili kulinda uhuru wao. Baadhi ya viongozi hao ni Bwana Abushiri Bin Salim wa Pangani, Bwana Heri wa Saadani, Bwana Isike wa Unyamwezi, Mkwawa wa Uhehe na Machemba wa Uyao. Hata baada ya kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni, Wananchi wa Tanganyika waliendesha mapambano ya aina mbalimbali kupinga uonevu dhidi yao. Wakati wa utawala wa Wajerumani kwa mfano, wananchi wa Tanganyika walipigana vita maarufu vilivyojulikana kama Vita vya Majimaji. Vita hivyo vilipiganwa katika maeneo karibu yote yaliyoko kusini mwa Tanganyika kuanzia mwaka 1905 hadi 1907, na vilichochewa na nguvu ya umoja uliojengeka juu ya imani ya maji maalumu yaliyotolewa na kiongozi wa kijadi aliyeitwa Kinjeketile Ngwale. Katika kipindi cha utawala wa Waingereza, wananchi walitetea haki zao kupitia vyama na makundi ya kimaslahi yakiwemo ya wakulima wa mazao ya biashara kama vile *Kilimanjaro Native Planters Association* (KNPA) ambacho baadaye kilibadilishwa jina kuwa *Kilimanjaro Natives Cooperative Union* (KNCU), *Victoria Federation of Cooperative Union* (VFCU), *Bukoba Bahaya Union* (BBU), *Ngoni Matengo Cooperative Union* (NGOMAT), *Rungwe Union* na *Meru Union*. Aidha, kulikuwa na vyama vya wafanyakazi katika maeneo mbalimbali wakiwemo wafanyakazi wa bandari, reli na watumishi wa Serikali. Mwaka 1955, umoja mkubwa zaidi wa wafanyakazi uliojulikana kama *Tanganyika Federation of Labour* (TFL) uliundwa kuunganisha vyama vyote vya wafanyakazi.


Baadhi ya vyama vya kupigania maslahi vilikuwa na mwelekeo wa kisiasa tangu kuanzishwa kwake. Miongoni mwa vyama hivyo ni *Tanganyika African Association* (TAA) kilichoanzishwa mwaka 1929, na baadaye mwaka 1954 kilibadilishwa jina na kuwa *Tanganyika African National Union* (TANU). Chama cha TANU kikiongozwa na wazalendo na wanaharakati maarufu ndicho kilichoongoza mapambano ya kudai uhuru kutoka kwa Waingereza.

Tarehe 1 Mei, 1961, Tanganyika ilipata Serikali ya Ndani, na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akawa Waziri Mkuu na hatimaye Uhuru kamili wa Tanganyika ulipatikana tarehe 9 Desemba, 1961. Tarehe 9 Desemba, 1962 Tanganyika ilitangazwa kuwa Jamhuri na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akawa Rais Mtendaji, Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Baada ya Uhuru wa Tanganyika, viongozi waliweka mazingira mazuri ya kujenga misingi mikuu ya utaifa ambayo ni utambulisho wake miongoni mwa mataifa. Misingi hiyo ni pamoja na umoja, utu, uhuru, maendeleo, usawa, haki, kujitegemea, utaifa na uzalendo, amani na maadili.

### 1.2.2 Historia ya Zanzibar

Zanzibar inajumuisha visiwa vikubwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vingine vidogo vidogo vinavyokaliwa na watu na vingine visivyokaliwa na watu ambavyo vipo katika Bahari ya Hindi mashariki mwa mwambao wa Afrika Mashariki. Wakaazi wa asili wa Zanzibar ni Waafrika wenye asili ya Wabantu ambao wengi walitoka eneo la Tanganyika. Baadhi ya Wabantu walifika Tanganyika na Zanzibar kutoka sehemu nyingine za Afrika, yakiwemo maeneo ya kati, kaskazini na kusini. Uchumi wa wakazi wa asili wa Zanzibar ulitegemea kwa sehemu kubwa kilimo cha mazao, uvuvi, ufugaji na ufundi wa zana za kufanyia kazi.

Wageni walianza kukaa Zanzibar karne nyingi zilizopita. Baadhi ya wageni hao ni Washirazi kutoka Iran ambao katika miaka ya 1200 walifika Kilwa, Mafia na maeneo mengine ya Pwani ya Afrika Mashariki. Katika miaka ya 1500 Kisiwa cha Zanzibar kilikuwa kimegawika katika wilaya mbalimbali za kifalme kila wilaya ikiwa na mfalme wake ikiwemo Kisiwa cha Tumbatu. Baadaye ndipo alipotawala Mwinyi Mkuu ambaye ndiye alama ya utawala wa kienyeji kisiwani Unguja na Mkamandume Kisiwani Pemba. Wageni wengine ni Wareno ambao walitawala Zanzibar kwa takriban karne mbili kabla ya kuondolewa na Waomani. Utawala rasmi wa Sultani wa Oman katika visiwa vya Zanzibar chini ya Said bin Sultan ulianza mwaka 1828 ambapo alihamishia Makao Makuu yake Zanzibar mwaka 1832. Said bin Sultan aliendelea kutawala Zanzibar hadi mwaka 1856 alipofariki. Waomani walijishughulisha pia na biashara mbalimbali ikiwemo biashara ya utumwa.



*Msafara wa Watumwa kutoka Bara ukielekea Pwani ya Afrika Mashariki mwanzoni mwa karne ya 19*

Pamoja na Zanzibar kuwa chini ya utawala wa Sultani wa Oman katika kipindi chote hicho, mwaka 1886 Uingereza na Ujerumani walipatana juu ya ugawaji wa maeneo ya Afrika ya Mashariki. Chini ya makubaliano hayo, mwaka 1890 Zanzibar iliwekwa rasmi chini ya himaya ya Waingereza.

Kama ilivyokuwa kwa nchi nyingi za Bara la Afrika, harakati za kujikomboa pia zilianza Zanzibar. Harakati hizo zilipata nguvu kutokana na kuanzishwa vyama vya siasa baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia iliyotokea kati ya mwaka 1939 na 1945. Kabla ya hapo, kulikuwa na jumuiya mbalimbali kama vile Jumuiya ya Waarabu (Arab Association), Jumuiya ya Wahindi (Indian Association), Jumuiya ya Waafrika (African Association), na Jumuiya ya Washirazi (Shirazi Association). Baadhi ya jumuiya hizo zilikuwa na wawakilishi wa kuteuliwa kwenye Baraza la Kutunga Sheria (Legislative Council) chini ya utawala wa Waingereza. Jumuiya hizo ziliwakilisha maslahi ya kila Jumuiya katika visiwa vya Unguja na Pemba. Mwaka 1955, kiliundwa Chama cha Zanzibar Nationalist Party (ZNP) chini ya Uongozi wa Bwana Ali Muhsin Baruani na mwaka 1957 Chama cha Afro-Shirazi Party (ASP) chini ya Uongozi wa Sheikh Abeid Amani Karume kiliundwa. Vyama hivyo viliendeleza mapambano ya kisiasa na viliingia katika chaguzi za mwaka 1957, 1961 na 1963, ambapo ASP ilishinda. Katika uchaguzi wa mwaka 1963, Chama cha ZNP kilipata viti 10 na ASP viti 10 na Zanzibar and Pemba People’s Party (ZPPP) kilichoundwa na baadhi

ya wafuasi waliojitoa ASP mwaka 1959 ilipata viti vitatu. ZPPP iliungana na ZNP na kuunda Serikali ambayo haikuungwa mkono na Wazanzibari walio wengi. Kutokana na hali hiyo, Sultan Jamshid Bin Abdallah aliondolewa katika Mapinduzi Matukufu tarehe 12 Januari, 1964 na kuundwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya ASP.

## 1.3 Ushirikiano kati ya Tanganyika na Zanzibar

Ushirikiano kati ya watu wa Tanganyika na Zanzibar ulianza hata kabla ya wageni kuingia kutokana na historia na udugu wa damu kati ya watu wa pande hizo mbili. Ushirikiano kati ya watu wa Tanganyika na Zanzibar ulizaa lugha na tamaduni za kiswahili ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa udugu na ushirikiano. Historia ndefu ya ushirikiano na udugu ndiyo imejenga msingi na nguzo imara ya Muungano.

### 1.3.1 Ushirikiano kabla ya Ukoloni

Ushirikiano wa kiutamaduni baina ya jamii za Kiafrika zilizoishi katika ukanda wa mashariki wa Bara la Afrika na zile za Kizanzibari daima uliambatana na ushirikiano wa kiuchumi. Katika zama za kale, watu wa pande hizo mbili walikuwa wakibadilishana mazao na bidhaa mbalimbali zinazotokana na kilimo, uvuvi, maliasili na bidhaa za mikono (uhunzi, ususi na uchongaji), kuendana na mahitaji ya kila upande na kila jamii. Katika kipindi cha kuanzia karne ya 17 hadi mwishoni mwa karne ya 19, Tanganyika na Zanzibar zilikuwa sehemu ya mfumo mkubwa wa biashara uliounganisha mabara ya Afrika, Asia na Ulaya. Kupitia mfumo huo, bidhaa muhimu kama vile chumvi, dhahabu, pembe za ndovu na vyakula zilisafirishwa kutoka maeneo ya ndani ya Bara la Afrika hadi pwani na hatimaye kwenda Uarabuni na Ulaya kupitia Zanzibar. Kwa namna hiyo hiyo, bidhaa kutoka Uchina, Uarabuni na Ulaya ziliingizwa Zanzibar na hatimaye maeneo mbalimbali ya Afrika ya Mashariki na Kati.

Katika karne ya 19, biashara ya utumwa ilianza katika eneo hilo la Afrika ambapo watu walinunuliwa kutoka sehemu za Bara na kupelekwa pwani na kutumikishwa na matajiri walioishi pwani ya Afrika Mashariki. Wengine walisafirishwa kupitia bandari ndogo ya Bwagamoyo (Bagamoyo) hadi Zanzibar na Uarabuni, ambako walinunuliwa na kutumikishwa, ama katika mashamba ya matajiri katika Visiwa vya Unguja na Pemba au katika majumba

ya matajiri Unguja, Pemba, Uarabuni na India. Biashara ya utumwa iliziathiri vibaya jamii za Kiafrika zilizokuwa Tanganyika na Zanzibar, hasa kutokana na kudhalilishwa kwa utu wa Mwafrika, mateso na kupotea kwa nguvukazi iliyohitajika kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika sehemu hii ya Bara la Afrika.

### 1.3.2 Ushirikiano wakati wa Ukoloni

Katika kipindi cha ukoloni, Watanganyika na Wazanzibari waliendeleza ushirikiano wa kidugu na kiuchumi. Waliendelea kutembeleana, kuoana na kubadilishana mazao ya vyakula na bidhaa nyingine. Hata hivyo, ushirikiano huo na maendeleo ya watu wa Tanganyika na Zanzibar kwa ujumla yaliathiriwa kwa kiasi kikubwa na tawala za kikoloni zilizoanzishwa pande zote mbili, ambazo ziliwakandamiza na kuwanyonya wananchi. Hali hiyo iliwalazimu wananchi wa Tanganyika na Zanzibar kuanzisha mapambano dhidi ya wakoloni ya kudai haki zao. Hatimaye mapambano hayo yalielekezwa zaidi kwenye ukombozi wa wananchi wa nchi hizo kutoka utawala wa kikoloni.

Vuguvugu la kudai uhuru lilipata msukumo zaidi baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, ambapo Watanganyika na Wazanzibari walianzisha jumuiya za kimaslahi na kisiasa. Jumuiya hizo zilikuwa na ushirikiano wa karibu sana katika harakati za kumkomboa Mwafrika. Mwaka 1929, Waafrika wa Tanganyika walianzisha Jumuiya ya Waafrika (*African Association* - AA). Awali Jumuiya hiyo iliwaunganisha Waafrika katika mijadala ya kisomi hadi mwaka 1948, ilipobadilishwa jina na kuitwa *Tanganyika African Association* (TAA). Jumuiya hiyo ilikuwa na ushirikiano mzuri na Jumuiya ya Waafrika wa Zanzibar (*African Association*) iliyoundwa mwaka 1934. Malengo ya kisiasa ya jumuiya hizo yalifanana na yalisisitiza kujenga utambulisho thabiti wa Waafrika katika kupigania haki zao.




*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (wa tano kutoka kulia mstari wa mbele) akiwa na baadhi ya Viongozi wa Chama cha TANU mwaka 1954 Mtaa wa Lumumba, Dar es Salaam*

Mwaka 1954, TAA ilibadilishwa jina na kuwa TANU, chama ambacho kiliongoza harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika hadi ulipopatikana tarehe 9 Desemba, 1961, chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa upande wa Zanzibar, mwaka 1957, *African Association* ilijiunga na umoja wa Washirazi wa Unguja na Pemba (*Shirazi Association - SA*) na kuunda *Afro-Shirazi Party* (ASP) chini ya uongozi wa Sheikh Abeid Amani Karume. Katika harakati za kupigania uhuru, TANU na ASP viliendeleza ushirikiano uliokuwepo kati ya Jumuiya za TAA na AA kwa kualikana katika mikutano muhimu na viongozi wao kuwasiliana mara kwa mara. Kwa mfano, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akiwa Mwenyekiti wa TANU, alihudhuria mkutano wa mwaka 1957 uliounganisha *African Association* na *Shirazi Association* na kuunda ASP. Hata baada ya Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar, vyama vya TANU na ASP viliendelea kudumisha ushirikiano wa kisiasa.



Wanachama wa Afro-Shirazi Party, wakiandamana kuunga mkono uongozi wa Chama chao



Wanachama  wa Chama cha TANU wakiandamana wakati wa harakati za kudai uhuru wa Tanganyika

Vilevile, ushirikiano miongoni mwa Watanganyika na Wazanzibari wakati wa ukoloni ulijidhihirisha katika shughuli za vyama vya michezo. Kwa mfano, kulikuwa na ushirikiano mkubwa kati ya vyama vya mpira vya *African Sports* ya Zanzibar, *African Sports Club* ya Tanga na *Young Africans Sports Club* (Yanga) ya Dar es Salaam. Kiongozi wa ASP, Sheikh Abeid Amani Karume, ndiye aliyefanikisha kuanzishwa kwa tawi la *African Sports Club* mjini Dar es Salaam, ambalo lilikuwa chimbuko la Klabu ya michezo ijulikanayo leo kama Yanga. Sheikh Karume pia alitoa misaada ya kifedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Klabu za Yanga na Sunderland za mjini Dar es Salaam, na ndiye aliyewashauri wana Sunderland kubadilisha jina hilo kuwa "Simba Mwekundu".

## 1.4 Uhusiano kati ya Muungano na Harakati za Umajumui wa Kiafrika

Jamii za Kiafrika zimepitia historia ndefu ya kunyanyaswa na kudhulumiwa na watu kutoka mataifa mengine duniani.  Historia hiyo ilianza karne ya 15 hadi 19 wakati wa biashara ya utumwa, ambapo Waafrika wengi walipelekwa mabara ya Amerika, Asia na Ulaya na kutumikishwa katika mashamba, migodi na majumba ya matajiri bila ya malipo. Kunyanyaswa na kudhulumiwa huko kwa Waafrika kuliendelea katika kipindi cha ukoloni, ambapo mataifa ya Ulaya yaliligawa bara hili na kulitawala kwa lengo la kujinufaisha kiuchumi kutokana na rasilimali zake.

Kutokana na adha ya kuwa chini ya tawala dhalimu kwa muda mrefu, Waafrika walipata mwamko na kuona umuhimu wa kuunganisha nguvu katika harakati za kupigania haki na uhuru wao. Viongozi walioanzisha harakati hizo walikuwa Waafrika na Waamerika weusi, wakiwemo William E.B. Dubois, Marcus Garvey, George Padmore na C.L.R. James. Dubois aliwahimiza Wamarekani weusi kujielimisha kuhusu kunyanyasika kwao na kuchukua hatua za kujikomboa kwa kutumia nguvu ya hoja na umoja wao. Garvey alifanya harakati kubwa ya kuwaunganisha Wamarekani weusi akitumia kauli mbiu yake ya *Back to Africa* yaani "Kurudi Afrika".

Juhudi za Waafrika waliokuwa Marekani ziliungwa mkono na Waafrika Barani Afrika wakiwemo Kwame Nkrumah wa Ghana, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa Tanganyika na Sheikh Abeid Amani Karume wa Zanzibar. Viongozi hao walikuwa miongoni mwa Waafrika mashuhuri walioshiriki katika harakati za kueneza wazo la kuwaunganisha Waafrika kama njia ya kufanikisha harakati za ukombozi kutoka kwenye makucha ya ukoloni. Katika eneo la Afrika Mashariki na Kati, juhudi hizo zilijumuisha ushirikiano wa kiharakati chini ya umoja ulioitwa *Pan-African Freedom Movement of Eastern and Central Africa* (PAFMECA). Pia, harakati kama hizo zilifanyika Afrika Magharibi chini ya makundi mawili ya Monrovia na Casablanca.

Viongozi walioongoza harakati za ukombozi wa Bara la Afrika kutoka eneo la Afrika Mashariki, wakiwemo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, walikutana mara kwa mara chini ya umoja wa PAFMECA wakijadili uwezekano wa kuziunganisha nchi zao mara baada ya kupata uhuru. Katika mikutano ya PAFMECA iliyofanyika Zanzibar mwezi Aprili na Nairobi mwezi Septemba mwaka 1959, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisisitiza na kusimamia upatanishi na umoja wa Waafrika katika harakati za kupigania uhuru, bila kujali rangi, kabila au dini zao. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulikuwa ni hatua muhimu kuelekea kwenye umoja wa Waafrika ulioanza kupiganiwa na viongozi wa Kiafrika hata kabla ya kupatikana kwa uhuru kutoka kwa wakoloni.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa na Rais wa Ghana Dkt. Kwame Nkrumah wakati wa Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika mwaka 1966*

## 1.5 Matukio Muhimu Kuelekea Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulitanguliwa na matukio kadhaa muhimu ya kisiasa yaliyotokea muda mfupi kabla ya Aprili, 1964. Kwa kiasi kikubwa matukio hayo yalichochea ari ya Watanganyika na Wazanzibari kuungana mara baada ya kupata uhuru. Tukio la kwanza lilikuwa ni uhuru wa Tanganyika uliopatikana tarehe 9 Desemba, 1961, ambao ulitoa fursa kwa viongozi wa nchi hiyo na wananchi kujiamulia mambo muhimu kuhusu nchi yao ikiwa ni pamoja na kuchukua misimamo katika masuala yanayohusu ushirikiano wa kimataifa. Viongozi wa Tanganyika huru wakiongozwa na Rais wa Kwanza Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, walikwishatambua umuhimu wa kuwaunganisha Waafrika katika jitihada za kuleta maendeleo

katika Bara la Afrika. Hivyo, uhuru wa Tanganyika ulitoa fursa kwa viongozi hao kuchangia kwa vitendo harakati za kuwaunganisha Waafrika.

Tukio la pili lilikuwa "Uhuru wa Bandia" waliopewa Wazanzibari kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza tarehe 10 Desemba, 1963. Uhuru huo haukuwaridhisha Wazanzibari walio wengi kwani kimsingi nchi ilibaki chini ya utawala wa Sultani Jemshid bin Abdalla. Badala yake, ulichochea fikra na ari miongoni mwa Wazanzibari ya kufanya Mapinduzi ili kuleta "Uhuru wa Kweli". Azma hiyo ilitimia tarehe 12 Januari 1964, ambapo Wazanzibari kwa umoja wao waliuangusha utawala wa Sultani Jemshid bin Abdalla na kutoa fursa ya kuundwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mapinduzi Matukufu yalileta uhuru wa kweli kwa Wazanzibari na kutoa fursa kwa nchi hiyo kufanya maamuzi kuhusu uhusiano na ushirikiano wake na nchi nyingine barani Afrika na kwingineko duniani kwa maslahi ya wananchi wake. Kufikia wakati huo, Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume alikwishajipambanua kuwa mwanaumajumui thabiti wa Kiafrika. Hivyo, Mapinduzi ya Zanzibar yalimpa kiongozi huyo na wanamapinduzi wenzake fursa ya kutekeleza kwa vitendo nia ya kuwaunganisha Wazanzibari na Waafrika wengine.

Fikra za kuunganisha Tanganyika na Zanzibar ziliongezeka kutokana na jitihada zilizokuwa zinafanyika katika kuanzisha Shirikisho la Afrika Mashariki mara baada ya uhuru wa Tanganyika, Kenya, Uganda na Zanzibar. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere binafsi alipendelea kuwepo kwa Muungano wa Afrika kwa kuanzia na ushirikiano wa kikanda. Baada ya kushauriana na viongozi mbalimbali chini ya muungano wa Wapigania Uhuru wa Afrika Mashariki na Kati (PAFMECA), Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitoa tamko katika mkutano wa nchi huru za Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, mwaka 1960, akisema:

> *Wengi wetu tunakubaliana bila kikwazo kwamba Shirikisho la Afrika Mashariki litakuwa ni jambo zuri. Tumesema na ni kweli kwamba mipaka inayotenganisha nchi zetu imewekwa na mabeberu na sio sisi wenyewe na kwamba tusikubali itumike dhidi ya umoja wetu lazima tuzisumbue ofisi za wakoloni kwa nia si ya kudai uhuru wa Tanganyika, kisha Kenya, na Uganda halafu Zanzibar lakini kwa nia ya kutaka uhuru wa Afrika Mashariki kama Muungano mmoja wa kisiasa.*

Kwa bahati mbaya azma hiyo haikutimia. Hata hivyo, kushindikana kuundwa mapema kwa Shirikisho la Afrika Mashariki kulichochea makubaliano ya haraka kati ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume kuasisi Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Hivyo, ingawa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kimsingi umetokana na historia ndefu ya ushirikiano kati ya watu wa nchi hizo, matukio yaliyotajwa yalichochea kwa pamoja kuundwa kwa Muungano huo muda mfupi baada ya nchi hizi mbili kupata uhuru.

## 1.6 Hatua Muhimu katika Kuundwa kwa Muungano


Kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulipitia hatua mbalimbali. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar kukubaliana kuungana mwaka 1964 na kuanzisha Dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Hatua ya pili, ilikuwa ni kwa waasisi wa Muungano Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume kuweka saini Hati ya Makubaliano ya Muungano tarehe 22 Aprili, 1964 Zanzibar.



*Rais wa Jamhuri ya Tanganyika Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Sheikh Abeid Amani Karume wakiweka saini Hati ya Makubaliano ya Muungano tarehe 22 Aprili, 1964 Zanzibar*

Hatua ya tatu ilikuwa ni kuthibitisha makubaliano hayo katika Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi tarehe 25 Aprili, 1964, ambapo tukio hilo lilifuatiwa na sherehe kubwa zilizoambatana na kitendo cha kuchanganya

udongo wa Tanganyika na Zanzibar mjini Dar es Salaam kudhihirisha Muungano huo.



*Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akichanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar ikiwa ni ishara ya kuunganisha nchi mbili wakati wa Sherehe ya Muungano Dar es Salaam tarehe 26 Aprili, 1964*



*Kikundi cha utamaduni kikitoa burudani ya ngoma wakati wa Sherehe ya Muungano tarehe 26 Aprili, 1964 Dar es Salaam*

Hatua ya nne ilikuwa ni kubadilishana Hati ya Makubaliano ya Muungano, tukio ambalo lilifanyika tarehe 27 Aprili, 1964, katika Ukumbi wa Karimjee Jijini Dar es Salaam. Katika kutekeleza makubaliano yaliyomo katika Hati ya Makubaliano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar *(Articles of Union),* Serikali zote mbili zilitunga Sheria ambazo ni: Sheria Nambari 22 ya mwaka 1964, iliyopitishwa na Bunge la Tanganyika tarehe 25 Aprili, 1964, na Sheria Nambari 243 iliyopitishwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, na kutangazwa katika Gazeti rasmi la Serikali ya Tanganyika la tarehe 1 Mei, 1964 kwa maridhiano ya pande zote mbili.



*Rais wa Jamhuri ya Tanganyika Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kushoto) akimkabidhi Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Sheikh Abeid Amani Karume (kulia) Hati ya Makubaliano ya Muungano katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam tarehe 27 Aprili, 1964*

Hati ya Makubaliano ya Muungano ilitamka uundwaji wa Jamhuri ya Muungano katika kifungu cha Kwanza (i) kuwa "Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zitaungana kuwa Jamhuri Huru.

Hatua ya tano ilikuwa ni kubadilishwa kwa jina la Jamhuri ya Tanganyika na Zanzibar kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa *The United Republic* (*Declaration of Name) Act No.61 of 1964,* kitendo ambacho kilifanyika tarehe 28 Oktoba, 1964.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Sheikh Abeid Amani Karume wakisalimia wananchi wakati wa sherehe za Muungano tarehe 27 Aprili, 1964*

## 1.7 Chimbuko la Jina la Tanzania

Jina 'Tanzania' ambalo Taifa linajivunia kuwa ni tunu muhimu, lilibuniwa miaka 50 iliyopita kufuatia shindano la kubuni jina hilo. Watu 16 walijitokeza katika shindano hilo ambapo Bwana Mohammed Iqbar Dar aliyekuwa na umri wa miaka 18, mwanafunzi wa Shule ya Agakhan - Morogoro (sasa inaitwa Forest Hill Secondary School) aliibuka mshindi. Bwana Mohammed alizaliwa Mkoa wa Tanga mwaka 1944, katika familia ya Bwana Tufal Ahmed Dar mwenye asili ya Asia. Mbinu aliyoitumia katika ubunifu wa jina hilo ni kuunganisha herufi tatu za mwanzo za majina ya Tanganyika na Zanzibar. Kwa upande wa Tanganyika alianza kwa herufi tatu yaani 'TAN', na kwa upande wa Zanzibar alianza kwa herufi tatu pia 'ZAN'. Herufi hizo kwa pamoja aliziunganisha na kuwa 'TANZAN' na baadaye kuongeza herufi mbili yaani 'IA' (kwa kurejea majina mengi ya nchi za Afrika yanavyoishia IA –mfano Zamb**ia**, Niger**ia**, Gamb**ia**, Ethiop**ia**, na Somal**ia**) na kupatikana jina 'TANZANIA'. Jina "Tanzania" lilitangazwa rasmi katika hafla maalum

ya kumtunuku Bwana Mohammed Iqbar Dar zawadi ya ngao pamoja na fedha taslim Dola za Marekani 200, alizokabidhiwa na Waziri wa Habari na Utalii kwa niaba ya Serikali Mheshimiwa Idris Abdulwakil Nombe tarehe 20 Novemba, 1964. Bwana Mohammed Iqbar Dar anaingia katika ukurasa wa historia ya kumbukumbu ya kuzaliwa Taifa la Tanzania.

## 1.8 Mipaka na Jiografia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Tanzania ipo kati ya Latitudo ya nyuzi 1 hadi 12 Kusini mwa Ikweta na Longitudo ya nyuzi 29 hadi 41 Mashariki ya Mstari wa *Greenwich.* Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina jumla ya eneo la mita za mraba 948,740. Kati ya hizo, eneo la nchi kavu ni mita za mraba 889,460. Tanzania ina pwani yenye urefu wa mita 1,404.5. Aidha, yapo maziwa matatu makubwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ambayo yapo mipakani na yakijumuishwa na maziwa mengine madogo, eneo lote la maji ni mita za mraba 59,280. Tanzania ina mito zaidi ya ishirini na asilimia kubwa ya mito hii inamwaga maji yake katika Bahari ya Hindi.

Tanzania inapakana na nchi za Kenya na Uganda upande wa Kaskazini; Burundi na Rwanda upande wa Kaskazini Magharibi; Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo upande wa Magharibi; Malawi upande wa Kusini Magharibi; Msumbiji upande wa Kusini na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Tanzania ina jumla ya watu 44,928,923 ambapo kati yao watu 43,625,354 wako Tanzania Bara na 1,303,569 wako Zanzibar. Idadi ya wanaume ni 21,869,990 kati yake 21,239,313 wako Tanzania Bara na 630,677 wako Zanzibar; na wanawake 23,058,933, kati yao 22,386,041 wako Tanzania Bara na 672,892 wako Zanzibar.

## 1.9 Muundo na Mambo ya Muungano

Hati ya Makubaliano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya tarehe 22 Aprili, 1964, ilibainisha muundo wa Muungano wa Serikali mbili. Serikali hizo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakayokuwa na mamlaka ya kushughulikia mambo yote ya Muungano na yote yasiyokuwa ya Muungano yanayoihusu Tanzania Bara, na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakayoshughulikia masuala yote yasiyo ya Muungano yanayoihusu Zanzibar. Aidha, Hati hiyo iliorodhesha mambo kumi na moja (11) ya Muungano ambayo ni Katiba na Serikali ya Muungano; Mambo ya Nchi za

Nje; Ulinzi; Polisi; Mamlaka juu ya mambo yanayohusika na hali ya hatari; Uraia; Uhamiaji; Mikopo na Biashara ya Nchi za Nje; Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano; Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha; bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, posta na simu.

### 1.10 Mabadiliko katika Orodha ya Mambo ya Muungano

Kwa nyakati mbalimbali na kwa sababu tofauti, Orodha ya Mambo ya Muungano imekuwa ikifanyiwa marekebisho kwa mujibu wa taratibu za kisheria na Kikatiba na kwa kushirikisha pande zote mbili za Muungano. Tarehe 10 Juni, 1965, jambo la 12 liliongezwa katika Orodha hiyo, nalo lilihusu mambo yote yahusuyo sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali (pamoja na noti); mabenki (pamoja na mabenki ya kuweka akiba) na shughuli zote za mabenki; fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusu fedha za kigeni. Sababu kubwa ya kuongezwa kwa jambo hilo ilikuwa ni kuwa na sarafu ya pamoja ya Tanzania baada ya Muungano, na kurahisisha usimamizi wa fedha za kigeni na mabenki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulikosababishwa na kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1964. Baada ya kuvunjika kwa Bodi hiyo, kila nchi mwanachama wa Jumuiya ililazimika kuwa na sarafu yake na mipango ya kusimamia mambo yake ya kibenki na fedha. Aidha, kufuatia kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, tarehe 11 Agosti, 1967 mambo mawili ya Muungano yaliongezwa, ambayo ni leseni za viwanda na takwimu (Jambo la 13), na elimu ya juu (Jambo la 14).

Mwaka 1968 suala la maliasili ya mafuta pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta na gesi asilia liliongezwa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano kuwa Jambo la 15. Vilevile, kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 na kutungwa kwa Katiba ya Kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mambo yafuatayo yaliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano:

(i) Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yanayohusika na kazi za Baraza hilo (Jambo la 16);

(ii) Usafiri na Usafirishaji wa Anga (Jambo la 17);

(iii) Utafiti (Jambo la 18);

(iv) Utabiri wa Hali ya Hewa (Jambo la 19); na

(v) Takwimu (Jambo la 20).

Aidha, kutokana na kuvunjika kwa Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki mwaka 1979, suala la Mahakama ya Rufani ya Tanzania nalo liliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano na kuwa Jambo la 21. Kufuatia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Nyalali, Jambo la 22 la Uandikishaji wa Vyama vya Siasa na mambo mengine yanayohusiana nayo liliongezwa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano. Hii ilifuatia kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa na uamuzi kuwa vyama vitakuwa vya kitaifa. Suala hilo hatimaye lilipitishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa Na.5 ya mwaka 1992. Utaratibu uliotumika katika kuongeza idadi ya mambo ya Muungano kutoka 11 hadi kufikia 22 ni kupitia maamuzi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.


## 1.11 Mabadiliko ya Uongozi Mwaka 1964–2014

Kabla ya Muungano, Jamhuri ya Tanganyika ilikuwa ikitumia Katiba ya Mwaka 1962 katika kuendesha shughuli zote za Serikali ambapo Zanzibar ilikuwa ikiendesha shughuli zake kupitia Amri za Katiba (Constitutional Decrees) za mwaka 1964. Baada ya Muungano 1964, Katiba ya Tanganyika ilifanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji ya Muungano na iliendelea kutumika hadi mwaka 1965, ilipotungwa Katiba ya Muda. Katika marekebisho hayo, Rais wa Zanzibar alitajwa kuwa ni Makamu wa Kwanza wa Rais, ambaye atakuwa ni Msaidizi wa Rais kwa masuala yote ya kiutawala kwa upande wa Zanzibar, na Waziri Mkuu alitajwa kuwa ni Makamu wa Pili wa Rais ambaye atamsaidia Rais kwa masuala yanayohusu upande wa Tanganyika na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Sheria zilizotungwa kutekeleza mambo yaliyomo katika Hati ya Makubaliano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yalibainisha mgawanyo wa madaraka wenye Viongozi Wakuu kutoka pande zote mbili za Muungano, yaani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wawili wa Rais ambao, kati yao mmoja alitoka Zanzibar.

### Awamu ya Kwanza (1964 – 1985)

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheikh Abeid Amani Karume alikuwa Makamu wa

Kwanza wa Rais na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hadi 1972. Aidha, Mheshimiwa Rashid Mfaume Kawawa alikuwa Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi tarehe 13 Februari, 1977.



*Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (1964 - 1985)*


Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliongoza Taifa hadi alipoacha madaraka kwa hiyari mwaka 1985. Katika kipindi hicho baada ya Sheikh Abeid Amani Karume kufariki mwaka 1972, Zanzibar iliongozwa na Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi ambaye pia alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 7 Aprili, 1972 hadi tarehe 30 Januari, 1984, na baadaye alifuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi mara baada ya Mheshimiwa Jumbe kujiuzulu uongozi. Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alishika wadhifa huo kuanzia tarehe 30 Januari, 1984 hadi tarehe 24 Oktoba, 1985.

Makamu wa Pili wa Rais wengine katika kipindi hicho baada ya Mheshimiwa Kawawa, walikuwa Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine kuanzia tarehe 13 Februari, 1977 hadi 7 Novemba, 1980, na baadaye kuanzia tarehe 24

Februari, 1983 hadi tarehe 12 April, 1984 alipofariki. Aidha, Mheshimiwa Cleopa David Msuya alishika wadhifa huo kuanzia tarehe 7 Novemba, 1980 hadi 24 Februari, 1983. Makamu wa Pili wa Rais wa mwisho katika uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim aliyeongoza kuanzia tarehe 24 Aprili, 1984 hadi tarehe 5 Novemba, 1985.

**Awamu ya Pili (1985-1995)**

Rais wa Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi aliyeongoza kuanzia Novemba, 1985 hadi Novemba 1995. Katika kipindi hicho, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walikuwa Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba aliyeshika wadhifa huo kuanzia tarehe 5 Novemba, 1985 hadi tarehe 9 Novemba, 1990. Vilevile Mheshimiwa John Samwel Malecela alishika wadhifa huo kuanzia tarehe 9 Novemba, 1990 hadi tarehe 5 Desemba, 1994. Baadaye alifuatiwa na Mheshimiwa Cleopa David Msuya aliyeshika nafasi hiyo hadi tarehe 28 Novemba, 1995.



*Rais wa Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
*Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi (1985 -1995)*

Kwa upande wa wadhifa wa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Idris Abdulwakil Nombe alishika wadhifa huo kuanzia tarehe 24 Oktoba, 1985 hadi tarehe 25 Oktoba, 1990 na kufuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Salmin Amour Juma aliyeshika wadhifa huo kuanzia tarehe 25 Oktoba, 1990 hadi tarehe 28 Novemba, 1995.

Kutokana na mageuzi ya kiuchumi na kisiasa yaliyotokea katika miaka ya 1990, Tanzania iliamua kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa. Kufuatia mabadiliko hayo, mwaka 1994, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 ilifanyiwa marekebisho na kuweka utaratibu mpya wa kumpata Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kwa mujibu wa marekebisho hayo, mgombea Urais anakuwa na mgombea mwenza. Endapo mgombea Urais atatoka Tanzania Bara, mgombea mwenza atatoka Zanzibar, na endapo mgombea Urais atatoka Zanzibar mgombea mwenza atatoka Tanzania Bara. Mgombea wa Urais atakapochaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mgombea mwenza atakuwa Makamu wa Rais. Kutokana na mabadiliko hayo, utaratibu wa kuwa na Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulikoma.

**Awamu ya Tatu (1995-2005)**

Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alikuwa Rais wa tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia Oktoba, 1995 hadi Novemba, 2005. Katika kipindi hicho, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma aliyeshika wadhifa huo kuanzia Oktoba, 1995 hadi Julai, 2001 alipofariki dunia na nafasi yake kuchukuliwa na Dkt. Ali Mohamed Shein aliyeshika wadhifa huo kuanzia Julai, 2001 hadi Novemba, 2005.



*Rais wa Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
*Mheshimiwa Benjamin William Mkapa (1995 – 2005)*

**Awamu ya Nne (2005- 2014)**

Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ndiye Rais wa Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameshika wadhifa huo kuanzia mwaka 2005 hadi sasa. Katika kipindi hiki, Makamu wa Rais walikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein aliyeshika tena wadhifa huo kuanzia mwaka 2005 hadi 2010 na kufuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal anayeshika wadhifa huo kuanzia 2010 hadi sasa.



*Rais wa Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
*Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete (2005 hadi sasa)*

# Utekelezaji na Mafanikio ya Muungano

## 2.1 Utangulizi

Mambo ya Muungano kama yalivyoorodheshwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, yanatekelezwa na Wizara na Taasisi zenye jukumu la kusimamia Mambo hayo. Mambo hayo ya Muungano yanahusu Katiba, Sheria na Utawala Bora; Uchumi; Fedha na Biashara; Ulinzi na Usalama; Diplomasia na Ushirikiano wa Kimataifa; Usafiri na Usafirishaji; Utabiri wa Hali ya Hewa; na Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, katika kuimarisha ustawi wa jamii na kuleta uwiano wa maendeleo, Serikali zote mbili (SMT na SMZ) zimepanua wigo kwa kuwa na ushirikiano katika mambo ya Muungano yanayotekelezwa kwa mujibu wa Sheria na mambo yasiyo ya Muungano. Kwa kipindi cha miaka 50, Serikali zote mbili zimefanikiwa kusimamia utekelezaji wa mambo hayo kwa ufanisi mkubwa. Usimamiaji makini wa utekelezaji wa mambo hayo unathibitishwa na mafanikio yaliyopatikana yakijumuisha utaifa na umoja, amani na utulivu na kuimarika kwa hali ya maisha ya wananchi kutokana na ukuaji wa uchumi wa pande mbili za Muungano.

## 2.2 Sera, Mipango, Mikakati na Programmu Mbalimbali za Utekelezaji wa Mambo ya Muungano

### 2.2.1 Maendeleo ya Uchumi mwaka 1961-1966

Katika miaka ya 1960, changamoto kubwa zilizoikabilli Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilikuwa ni namna ya kutimiza malengo ya kuleta maendeleo katika Jamhuri yenye ufinyu wa rasilimali watu na fedha, mapato kidogo ya Serikali na uchumi wenye maendeleo hafifu ya viwanda. Hivyo, mipango mbalimbali ya maendeleo ilihitajika kama mbinu ya kuwa na matumizi bora ya rasilimali kwa maendeleo ya Watanzania wote. Kaulimbiu mbalimbali zilitumiwa na viongozi wetu kama *kupanga ni kuchagua* na *kukubali kutokuwa na mipango ni kukubali kutokuwa na maendeleo.* Sera mbalimbali za Maendeleo, Mipango na Mikakati iliandaliwa pande zote mbili za Muungano ili kukabiliana na changamoto za maendeleo.

Aidha, mipango ya muda mfupi, kati na mrefu na mikakati iliandaliwa. Kwa upande wa Tanzania Bara, mipango ya maendeleo iliweka msisitizo wa kuboresha kilimo ili kutumia zana bora badala ya jembe la mkono. Aidha, maendeleo ya viwanda na rasilimali watu vilipewa kipaumbele. Mpango wa miaka mitatu ulioshia mwaka 1964 ulilenga sekta ya viwanda kukua kwa asilimia 15 ili kuongeza thamani ya uzalishaji wa msingi na pato la wastani la kila mwananchi kuongezeka kutoka Dola za Marekani 34 mwaka 1961 hadi Dola za Marekani 50.8 mwaka 1970. Matokeo ya mpango huo ni kuimarishwa vyama vya ushirika na ilipofika mwaka 1966, kulikuwa na vyama vya ushirika 33 na vya msingi 1,500. Kwa upande wa viwanda, hazikutengwa rasilimali za kutosha kwenye mipango ya awali kutokana na uwezo mdogo wa kifedha. Hivyo ukuaji wa sekta hiyo, haukuwa wa kuridhisha kwani viwanda hasa vya kusindika mafuta ya kula, matunda na nguo vilihitajika ili kusaidiana na Sekta ya Kilimo iliyokuwa inakua kwa kasi kuwezesha upatikanaji wa malighafi jambo ambalo halikutokea.

Kwa mujibu wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (1964-1969), Sekta ya Viwanda iliendelea kuwa hafifu na mchango wake uliongezeka kidogo tu kufikia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa ilipofika mwaka 1966. Uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda ulikuwa mdogo. Hata hivyo, vilikuwepo viwanda vikubwa na vya kati kama vile *British American Tobacco*, *East African Breweries*, *Coca Cola*, *Tanganyika Packers Limited*, *Metal Box,* na *Bata Shoe Company*. Aidha, kulikuwa na juhudi za kuongeza viwanda vingine vikubwa kama vile *Matsushita Electric Company*, *Philips (T) Limited* na *General Tyre East Africa*, viwanda ambayo vilimilikiwa na wawekezaji kutoka nje.

Kwa upande wa Zanzibar, SMZ ilitaifisha viwanda vidogo vidogo 14 vilivyokuwa vinazalisha bidhaa mbalimbali wakati wa ukoloni. Viwanda hivyo vilitawanyika katika maeneo ya mijini na vijijini. Bidhaa zilizozalishwa ni mafuta ya nazi, usumba na bidhaa zake, sabuni ya chokaa, na soda (Potello). Baada ya Mapinduzi, viwanda vipya tisa vilijengwa ili kuimarisha sekta ya viwanda. Bidhaa zilizozalishwa ni sigara; ngozi na viatu; soda; maziwa na bidhaa za maziwa; chakula cha mifugo; mafuta ya karafuu na makonyo; sukari na manukato; dawa na mbao. Halikadhalika, Serikali ilianzisha eneo maalum la viwanda vidogo vidogo ili kutoa ajira kwa wananchi na kuzalisha vifaa vya matumizi ya nyumbani. Viwanda 15 vilijengwa katika eneo hilo ambavyo vilizalisha nguo, vyombo vya nyumbani, samani za chuma na mbao, vifaa vya

umeme, sabuni za kuogea na za kufulia, mafuta ya kupikia na siagi, vitasa na bawaba, rangi, na vipuri. Mbali ya juhudi za Serikali za kuendeleza viwanda, sekta binafsi ilianzisha viwanda vya kutengeneza bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na nje. Kiwanda cha COTEX kilichotengeneza kanga na vitambaa na kiwanda cha Afro-Chem cha magodoro vilianzishwa.

Katika Sekta ya Fedha, mipango ya awali kabla ya Azimio la Arusha ilibadilisha kwa kiwango kikubwa shughuli za uchumi na maendeleo. Juhudi za kutoa fursa sawa kwa watu kupata mikopo bila ubaguzi ziliwezesha kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika mwaka 1964 na Benki ya Taifa ya Biashara mwaka 1965 ambayo Serikali ilimiliki asilimia 60 ya hisa. Serikali iliongeza nyumba bora na majengo ya kisasa kwa kuanzisha Benki maalum ya Nyumba mwaka 1965 kwa upande wa Tanzania Bara. Aidha, Benki ya Watu wa Zanzibar ilianzishwa mwaka 1966 na inaendelea kumilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Mwaka 1966, Serikali ilianzisha Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kusimamia upatikanaji na usambazaji wa huduma za kifedha katika sekta za uchumi pamoja na kusimamia shughuli za benki na taasisi za fedha nchini.

Mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, Zanzibar ilitekeleza ahadi ya Chama cha ASP za kutaifisha ardhi yote na kuwa mali ya Serikali ambayo iligawiwa kwa wananchi mwaka 1965. Jumla ya hekta 26,714 ziligawiwa kwa koo 22,262 Unguja na Pemba. Utaifishaji wa ardhi uliofanyika Zanzibar uliwezesha kila mwananchi aliyestahiki kupata ekari tatu. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitaifisha shule zote za kitabaka na kidini na kuwa mali ya Umma na kuamua wananchi wote watasoma bila ya malipo katika ngazi zote za elimu, pia huduma za afya kutolewa bure kwa watu wote.

### 2.2.2 Maendeleo ya Uchumi mwaka 1967-1985

Mwaka 1967 lilitangazwa Azimio la Arusha, na lilitoa ufafanuzi wa utekelezaji kwa vitendo Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Utaratibu wa kutumia rasilimali za ndani na kusisitiza nafasi kubwa ya kazi za kujitolea katika ujenzi wa Taifa ulipewa kipaumbele na kubadilisha mwelekeo wa sera na mipango ya utekelezaji wa shughuli za uchumi. Utekelezaji wa Azimio la Arusha uliambatana na kutaifisha njia kuu zote za uchumi kwa lengo la kuweka uchumi mikononi mwa umma. Utaifishaji huu ulihusisha taasisi za fedha na viwanda, vikiwemo *Tanganyika Packers*, na *General Tyre* kwa upande wa

Tanzania Bara na kampuni za *Auto Sales and Exchange Ltd, Kapadia Motor Mart, M. Takim and Company na Mussa Jusanbhani* kwa upande wa Zanzibar vilitaifishwa.

Kipindi cha mwaka 1967 hadi 1969 kilikuwa cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulioanza mwaka 1964. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (1969-1974), ulishirikisha zaidi wananchi na wawakilishi wao hasa kupitia Chama Tawala. Utekelezaji wake uliweka msukumo kwenye kilimo na madaraka mikoani, pamoja na kuinua hadhi ya baadhi ya miji kuwa vitovu vya ukuaji wa uchumi. Kwa upande wa rasilimali watu, Mpango huo ulilenga kuliwezesha Taifa kujitosheleza kwa wataalam katika nyanja zote za uchumi ifikapo mwaka 1980 na kumpatia kila mtoto wa Tanzania elimu ya msingi ifikapo mwaka 1989. Katika kipindi cha Mpango huo, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 3.7 ikilinganishwa na malengo ya ukuaji wa asilimia 6.7. Uliandaliwa pia mkakati wa kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya rasilimali fedha za kutekeleza Mpango huo zinatoka ndani ya nchi, hivyo kutekeleza kwa vitendo dhana ya kujitegemea. Katika utekelezaji wake, viwanda vingi vilijengwa, shughuli za kilimo zilipanuka na miundombinu zaidi ilijengwa.

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulianza mwaka 1976 hadi 1981 na ulilenga kuchochea zaidi maendeleo katika Sekta ya Viwanda kupitia mkakati wa ujenzi wa viwanda vya msingi. Vilevile, umuhimu wa kushirikisha wananchi katika mipango ulizidi kusisitizwa. Kwa hiyo, uandaaji wa Mpango huo ulishirikisha wadau wengi kuanzia ngazi ya kijiji hadi Taifa. Mpango huo ulisisitiza pia kujitosheleza kwa chakula ifikapo mwaka 1981 na ujenzi wa viwanda mama na uwezo wa kuzalisha malighafi za viwandani hapa nchini. Ukuaji wa uchumi katika Mpango huo ulilengwa uwe asilimia 6 kwa mwaka. Kilimo kilitegemewa kukua kwa asilimia 5.1 na viwanda kwa asilimia 9.3.

Mpango huo ulikuwa sehemu ya Mpango wa Muda Mrefu wa Mwaka 1969 hadi 1980, ambao ulikuwa na mwelekeo wa kufungamanisha sekta zote muhimu katika kuleta maendeleo na kuwapatia wananchi huduma za jamii. Lengo la Mpango wa muda mrefu lilikuwa kufikia asilimia 6.7 katika ukuaji wa Pato la Taifa na kuongeza mchango wa viwanda katika Pato la Taifa kutoka asilimia 13 hadi 26.7.

Utekelezaji wa Mpango huo haukwenda kama ilivyokusudiwa kutokana na kuibuka kwa msukosuko wa uchumi kufuatia kupanda sana kwa bei za mafuta na chakula duniani mwaka 1973/74, kushuka kwa bei za kahawa, pamba na katani katika soko la dunia, Vita vya Kagera (1978/79) pamoja na ukame. Zaidi ya hayo, kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (1977), Serikali ilitumia fedha nyingi kununua ndege kwa ajili ya kuanzishia Shirika la Ndege la Tanzania na kujenga karakana ya ndege na ya magari moshi. Yote hayo yaliathiri vibaya utekelezaji wa mipango katika vipindi vilivyohusika.

Utekelezaji wa Azimio la Arusha na mipango ya maendeleo ya miaka mitano ulifuatiwa na mabadiliko mengi katika kila nyanja ya uchumi na maendeleo ya watu. Katika Sekta ya Kilimo, mashamba makubwa ya vijiji vya ujamaa yaliyoendeshwa kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora yalianzishwa na mashamba mengi ya wakulima binafsi yalitaifishwa. Mwaka 1974 kulikuwa na kampeni ya *Kilimo cha Kufa na Kupona* iliyolenga kuongeza uzalishaji wa chakula katika ngazi ya kaya ili kuepuka njaa iliyokuwa imeukumba ukanda wa Afrika ya Mashariki kutokana na ukame (1973/74). Katika kipindi hicho, kilimo cha "Bega kwa Bega" katika Vijiji vya Ujamaa vilisisitizwa kama njia sahihi za kuongeza ufanisi katika uzalishaji. Mwaka 1982, kulikuwa na kampeni ya *Kilimo ni Uti wa Mgongo* ikiwa na lengo la kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kilimo katika uchumi na maisha ya Watanzania.

Katika kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa Jamii, Zanzibar iliandaa Mpango wa Maendelo (1978 – 1986). Malengo ya Mpango huo yalikuwa ni kuimarisha uchumi, kufuta umaskini na kuleta maendeleo endelevu.

### 2.2.3 Sera, Mipango na Maendeleo mwaka 1985-2013

Mfumo wa mabadiliko ya kiuchumi duniani pamoja na sababu za ndani yalileta mageuzi ya kiliberali nchini yaliyoambatana na mapinduzi ya kiteknolojia, usambazaji wa nguvukazi (labour mobility), mitaji na utandawazi. Mabadiliko hayo yalileta uchumi wa soko huria na utungaji wa sera zilizoendana na mfumo huo. Chini ya mfumo huo, Serikali ilijitoa katika shughuli za moja kwa moja za uzalishaji na kubaki na jukumu la kutunga sera na usimamizi kwa kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuwekeza na kufanya biashara. Kufuatia mabadiliko hayo ya mwishoni mwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980, Serikali ilitekeleza Programu za Kufufua Uchumi mwaka 1986 hadi 1992. Programu hizo zililenga kupunguza thamani ya fedha ili iendane

na bei halisi ya soko; kupunguza ruzuku; na kuondoa vikwazo katika biashara ili kuchochea biashara huria. Hatua nyingine muhimu zilizochukuliwa chini ya programu hizo ni pamoja na mageuzi katika Sekta ya Fedha yaliyofuatia miaka michache baadaye na hatimaye ubinafsishaji wa mashirika ya umma. Mageuzi mengine yaliyoambatana na Programu za Kufufua Uchumi ni kuweka ushindani katika ununuzi wa mazao kwa kuruhusu sekta binafsi kununua mazao kutoka kwa wakulima.

Aidha, Programu hizo zililenga kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa uchumi kwa kulegeza masharti katika uwekezaji na biashara; kupunguza ukubwa wa Serikali na kudhibiti matumizi na kubinafsisha Mashirika ya Umma. Programu hizo pia zilianzisha utaratibu wa kuchangia gharama za huduma za afya, elimu na maji, na kuondoa ruzuku, isipokuwa katika maeneo maalum. Utekelezaji wa Programu hizo uliweza kunusuru anguko la uchumi na kurudisha ukuaji wa uchumi kwa kiwango chanya, kuondoa uhaba mkubwa wa chakula, kuongeza ukwasi wa fedha za kigeni na kuimarisha uwezo wa Serikali kutoa huduma. Aidha, utekelezaji wa programu hizo ulileta mabadiliko makubwa katika bei ya bidhaa na pembejeo. Kwa mfano, bei za mazao ya chakula kama vile mchele, mihogo, mtama, na maharage zilishuka na bei kwa mzalishaji wa mazao ya biashara kuanza kuongezeka kufuatia ushindani katika ununuzi. Kuondolewa kwa ruzuku ya pembejeo hususan mbolea kulileta changamoto kadhaa ikiwemo kuongezeka kwa bei ya mbolea kwa takriban asilimia 400 kati ya mwaka 1989 na 1992. Hali hiyo ilisababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao na uhakika wa chakula kwa baadhi ya watu na kupungua kwa uwezo wa watu kupata mahitaji muhimu kama elimu, afya na maji.

### 2.2.4 Urekebishaji wa Mashirika ya Umma

Katika miaka ya 1980, Serikali pia ilianza mageuzi makubwa ya kurekebisha mashirika ya umma kwa kutumia mbinu mbalimbali. Moja ya mbinu hizo ni ubinafsishaji wa mashirika ya umma, Sera ambayo ilipata msukumo mkubwa kutoka kwenye vyombo vya kimataifa vya fedha hususan Shirika la Fedha Duniani na Benki ya Dunia. Hapa nchini, ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ulianza rasmi mwaka 1993 kwa lengo la kupanua mchango wa Sekta Binafsi katika uchumi na kuwawezesha wananchi kumiliki na kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizokuwa zikifanywa na mashirika ya umma.
Serikali ilipitisha utaratibu wa kubinafsisha mashirika kwa njia ya ubia kati ya

Serikali na wawekezaji binafsi; kubinafsisha mashirika kwa menejimenti na wafanyakazi; wafanyakazi kuuziwa shirika linalohusika; na kwa Serikali kuuza hisa zake zote kwa wawekezaji binafsi. Kutokana na uamuzi huo, Serikali ilijikita zaidi katika utoaji wa huduma za msingi na kuweka mazingira wezeshi na kanuni za usimamizi kwa sekta binafsi kushiriki ipasavyo katika shughuli za kiuchumi. Sera ya ubinafsishaji inabaki kuwa ni nyenzo muhimu ya kukuza uchumi, kuongeza ufanisi, upatikanaji wa rasilimali na ongezeko la ajira kwa nchi nyingi duniani. Pamoja na changamoto zilizopo katika ubinafsishaji, uzoefu umeonesha kuwa ubinafsishaji umeweza kusaidia upatikanaji wa mitaji mipya katika rasilimali na uzalishaji.

Katika uchumi wa Tanzania, umeongeza uwekezaji mpya kutokana na ongezeko la ushiriki wa sekta binafsi na kuwezesha faida na mishahara kuchangia mapato ya Serikali na kuwaongezea wananchi uwezo wa kumudu maisha. Aidha, ubinafsishaji umesaidia kupanuka zaidi kwa sekta ya benki na kuwezesha watu wengi zaidi kupata mikopo na kuanzisha shughuli za kiuchumi. Vilevile, umewezesha viwanda na mashirika kuuza hisa ili kuongeza fursa za kiuchumi kwa wananchi na kushiriki katika uwekezaji. Pia, viwanda vingi zaidi vimeweza kuuza bidhaa nje ya nchi na hivyo kuongeza mapato ya fedha za nje.

Kupanuliwa kwa wigo wa kodi kumeongeza mapato na hivyo kuimarisha uwezo wa Serikali katika utoaji huduma za jamii. Ajira katika sekta binafsi zimeongezeka kwa zaidi ya asilimia 10 kila mwaka kuanzia miaka ya 1990. Utafiti wa ajira na nguvu kazi wa mwaka 2006 unaonesha kuwa ajira katika sekta binafsi ilifikia watu milioni 1.5 ikilinganishwa na 45,975 kabla ya mageuzi kwa takwimu za mwaka 1980.

Miongoni mwa Mashirika ya Umma na Viwanda yaliyobinafsishwa kwa upande wa Tanzania Bara ni mgodi wa Almasi Mwadui (Shinyanga), Kiwanda cha Nguo (Morogoro), Kampuni ya Bia Tanzania, (Dar es Salaam). *National Food Corporation* (NAFCO), Viwanda vya Sukari (Kilombero, Mtibwa), *Tanganyika Plantation Company* - TPC (Moshi na Kagera). Kwa upande wa Zanzibar ni Kiwanda cha Sukari na Manukato (Mahonda) na Mashamba la Mpira (Mwakaje, Unguja, na Maziwani, Pemba).

### 2.2.5 Dira ya Maendeleo

Mwaka 1999, Serikali iliandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 yenye lengo kuu la kuifanya Tanzania Bara kuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati na kuondokana na umaskini ifikapo mwaka 2025. Kwa upande wa Zanzibar, Dira ya Maendeleo ya 2020 ilipitishwa mwaka 2000 ikiwa na malengo sawa na yale ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Dira hizo zimezingatia misingi na mazingira ya uchumi wa mfumo wa soko na maendeleo ya teknolojia duniani na zinalenga kujenga uchumi imara wa kisasa na kuwa na maisha bora kwa wananchi wa Tanzania.

### 2.2.6 Programu na Mikakati Mingine ya Maendeleo

Katika kufikisha huduma karibu na wananchi, mikakati mingine ya maendeleo ilianzishwa na Serikali. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

Mpango wa Kuweka Mazingira mazuri ya uwekezaji wa nje ujulikanao kama *Mini Tiger* kutokana na uzoefu uliopatikana kutoka nchi za Kusini mwa Asia, hususan China, India na Vietnam ambazo zimefanikiwa kukuza ajira na mauzo ya nje kwa kujenga kanda maalum za kiuchumi. Malengo ya Mpango huo ni kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kutoka asilimia 6 hadi 10; kuongeza mauzo nje kutoka dola bilioni 1 hadi dola bilioni 3 katika kipindi cha miaka mitatu na hadi dola bilioni 20 ifikapo mwaka 2020 kwa kujenga jumla ya kanda maalum za kiuchumi 25 hadi 30. Mpango huo pia umelenga kuongeza uwekezaji katika Sekta ya Nishati, maji na usafirishaji. Malengo mengine ni pamoja na ujenzi wa miradi mikubwa ya viwanda vya kutengeneza bidhaa ili kuongeza thamani ya bidhaa zinazouzwa ndani na nje ya nchi, kuongeza ajira mpya na kuongeza kipato cha Mtanzania hadi zaidi ya Dola 1,000 kwa mwaka itakapofika mwaka 2020. Mwaka 2009, uzinduzi wa Kanda Maalum ya Uwekezaji ya Benjamin William Mkapa iliyopo Mabibo ulifanyika ambapo wawekezaji 10 walipewa leseni za kuwekeza. Maeneo Maalum ya Viwanda vya Uzalishaji ya *Millennium Business Park* (Dar es Salaam), Hifadhi (Dar es Salaam), Kisongo (Arusha) na *Kamal Industries Estate I* (Bagamoyo) yalipewa leseni.

Kwa upande wa Zanzibar, SMZ iliamua kuanzisha taasisi mbalimbali kwa madhumuni ya kuimarisha uwekezaji kutoka nje ya nchi na kuwa na uchumi imara na endelevu. Miongoni mwa taasisi zilizoanzishwa ni Mamlaka ya

Kukuza Vitega Uchumi Zanzibar (Zanzibar Investment Promotion Authority - ZIPA), Mamlaka ya Maeneo Huru ya Kiuchumi Zanzibar (ZAFREZA) na Mamlaka ya Bandari Huru Zanzibar (Zanzibar Free Port Authority - ZFPA). Kwa ujumla Mamlaka hizo zimepewa majukumu ya kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, kukuza mapato ya Serikali kwa kuingiza utaalamu na teknolojia mpya, kuwapatia masoko wazalendo katika miradi ya uwekezaji, kukuza ajira na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

Kupitia Mamlaka hizo na taasisi nyingine za Serikali, Zanzibar imepiga hatua kubwa katika uwekezaji ambapo wawekezaji wa ndani na nje wamewekeza katika miradi ya hoteli na mikahawa, viwanda vidogo vidogo, mawasiliano, kilimo na sekta ya fedha. Kutokana na jitihada za Serikali za kuitangaza Zanzibar, mashirika na makampuni mengi yameonesha nia ya kuwekeza Zanzibar. Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uwekezaji ya Hamriya kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu imeonesha nia ya kujenga kiwanda kikubwa cha usafishaji wa mafuta ya vyombo vya moto na baharini, Zanzibar.

### 2.2.7 Mfuko wa Maendeleo ya Vijana

Katika kuongeza fursa na kuimarisha miradi ya kuwaendeleza vijana, Serikali ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana mwaka 1993/94 kwa lengo la kutoa mikopo midogo yenye masharti nafuu kwa vijana. Hadi kufikia mwaka 2007/08, Mfuko huo umeshatoa shilingi bilioni 2.9. Huduma za Mfuko zimepelekwa kwa Halmashauri za Manispaa, Wilaya na Miji nchini kote na vijana wameibua miradi iliyo endelevu. Mfuko huu umejenga na kuimarisha dhana ya kukopa na umewezesha vijana kuanzisha na kujiunga na SACCOS.

### 2.2.8 Mfuko wa Dhamana wa Mikopo kwa Wanawake

Mfuko wa Dhamana na Mikopo kwa Wanawake katika Sekta isiyo Rasmi ulianzishwa mwaka 2000. Mfuko umelenga katika kuwaondoa wanawake katika ajira hatarishi kwa kuanzisha na kuendeleza ajira binafsi kupitia miradi midogo; kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu; kuwawezesha kuanzisha vikundi na kujiunga kwenye SACCOS; kuimarisha SACCOS zilizoanzishwa baada ya mradi kukua na kuunda shirikisho la SACCOS zao. Huduma za mfuko huu zimewafikia wanawake wapatao 2,000 wa kipato cha chini wanaojiajiri kupitia miradi midogo ya kujikimu katika sekta isiyo rasmi. Vilevile, wanawake walioajiriwa kwenye mashamba ya chai na wanawake

500 ambao wanatoka katika mazingira magumu, hatarishi na yasiyo salama wamenufaika na huduma za mfuko huu.

### 2.2.9 Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Mauzo Nje

Mfuko huo ulianza mwaka 2002 kwa lengo la kutoa udhamini kwa mabenki ya biashara ili yaweze kutoa mikopo kwa wakulima, wafanyabiashara na Vyama vya Ushirika vinavyouza bidhaa nje na kwa wawekezaji kwenye miradi mikubwa. Hadi kufikia mwaka 2008, mtaji wa Mfuko ulikuwa shilingi bilioni 30.5 na ulitoa udhamini wa shilingi bilioni 273 na kuwezesha kupatikana mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 362.

### 2.2.10 Mfuko wa Kudhamini Mabenki na Taasisi za Fedha

Mwaka 2005, Mfuko wa Kudhamini Mabenki na Taasisi za Fedha kwa ajili ya Kuboresha Utoaji wa Mikopo kwa Miradi Midogo na ya Kati ulianzishwa chini ya Benki Kuu ya Tanzania kwa lengo la kukuza na kuendeleza miradi midogo na ya kati kwa kuwapa wajasiriamali wa Tanzania uwezo wa kifedha na kimtaji ili kuimarisha kipato chao, kuinua hali zao za maisha na kuongeza mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa. Mfuko umeongeza mitaji kutoka shilingi milioni 500 mwaka 2005 hadi shilingi bilioni 5.8 mwaka 2010.

### 2.2.11 Mifuko ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi

Serikali imeanzisha Mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wananchi ili kuinua kipato na kupunguza umaskini. Mifuko hiyo ni pamoja na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (Presidential Trust Fund), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi (Mwananchi Empowerment Fund). Kwa ujumla wake Mifuko hiyo imechochea maendeleo ya Watanzania na kutoa mchango mkubwa ikiwemo ajira, kuongeza kipato na hatimaye kupunguza umaskini.

## 2.3 Utekelezaji wa Mambo ya Muungano

### 2.3.1 Katiba, Bunge na Utawala Bora

***Katiba ya Jamhuri ya Muungano***

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ndiyo Sheria Mama ambapo Sheria, Kanuni, taratibu na mipango mbalimbali ya nchi hupata uhalali wa kutungwa, kurekebishwa, kufutwa na kutekelezwa. Kabla

ya Muungano, kulikuwa na Katiba ya Tanganyika ya mwaka 1962 na Amri za Katiba *(Constitutional Decrees)* za mwaka 1964 kwa upande wa Zanzibar. Mwaka 1964, Katiba ya Tanganyika ilifanyiwa marekebisho kukidhi mahitaji ya Muungano na iliendelea kutumika hadi mwaka 1965 ilipotungwa Katiba ya Muda. Katiba hiyo iliainisha mambo kumi na moja (11) ya Muungano ambayo ni Katiba na Serikali ya Muungano; Mambo ya Nchi za Nje; Ulinzi; Polisi; Mamlaka juu ya mambo yanayohusika na hali ya hatari; Uraia; Uhamiaji; Mikopo na Biashara ya Nchi za Nje; Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano; Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha; Bandari; mambo yanayohusika na usafiri wa anga; posta na simu.

Katiba ya mwaka 1965 iliainisha muundo wa Serikali mbili (SMT na SMZ) na Uwakilishi wa Zanzibar katika Bunge la Muungano. Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanganyika yaliwekwa chini ya Serikali ya Muungano. Mambo yasiyo ya Muungano yahusuyo Zanzibar yaliwekwa chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mambo ya Muungano yaliongezeka na kufikia ishirini na mbili (22) kutokana na mahitaji ya ndani ya nchi na mabadiliko yaliyotokea ulimwenguni baada ya Muungano. Mwaka 1965, mambo yote yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali (pamoja na noti); mabenki (pamoja na mabenki ya kuweka akiba) na shughuli zote za mabenki; fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusika na fedha za kigeni yaliongezwa katika mambo ya Muungano. Lengo likiwa ni kurahisisha usimamizi wa fedha za kigeni na mabenki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, mwaka 1967, leseni za viwanda na takwimu; na elimu ya juu ziliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano kufuatia kuundwa kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mwaka 1968, suala la maliasili ya mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta na gesi asilia pia liliongezwa kwenye orodha hiyo. Vilevile, Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yanayohusika na kazi za Baraza hilo; Usafiri na Usafirishaji wa Anga; Utafiti; Utabiri wa Hali ya Hewa; na Takwimu yaliongezeka katika orodha ya mambo ya Muungano kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki

na kutungwa kwa Katiba ya Kudumu mwaka 1977. Suala la Mahakama ya Rufani ya Tanzania liliongezwa katika orodha hiyo kufuatia kuvunjika kwa Mahakama ya Rufaa ya Afrika Mashariki mwaka 1979. Vilevile, mwaka 1992 suala la uandikishaji wa vyama vya siasa na mambo mengine yanayohusiana nayo, liliongezwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano.

Kwa ujumla Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imefanyiwa marekebisho mara 12 tangu ilipotungwa mwaka huo. Kutokana na hali hiyo, pamoja na mageuzi mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yaliyokuwa yakifanyika nchini tangu miaka ya 1960 hadi hivi sasa, umuhimu wa kuwa na Katiba Mpya ili kwenda sambamba na mageuzi hayo ulionekana. Wakati huu ambapo Tanzania inatimiza miaka 50 ya Muungano, nchi inaandaa Katiba Mpya ambayo utaratibu wake umehusisha makundi yote ya jamii. Utaratibu huu tofauti na utaratibu uliotumika kuandaa Katiba ya muda ya mwaka 1965 na Katiba ya kudumu ya mwaka 1977 ambazo ziliandikwa na kamati maalum zilizoteuliwa kutoka pande zote mbili za Muungano. Mwaka 2012, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83 ili kuruhusu taratibu za kuandaa Katiba Mpya. Kupitishwa kwa Sheria hiyo kulimwezesha Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Tume hiyo imepewa jukumu la kusikiliza maoni ya wananchi mmoja mmoja na kwa makundi yao ya maslahi, taasisi zao na kupitia Mabaraza ya Katiba. Tume hiyo iliundwa na wajumbe 30 ambapo kila upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliteuliwa wajumbe 15. Tume ilitakiwa kuandaa Rasimu ya Katiba Mpya itakayofikishwa kwenye Bunge Maalum la Katiba kujadiliwa na Katiba Mpya kutungwa. Mchakato wa Katiba utahitimishwa kwa wananchi kupiga kura ya maoni ya kuamua kama wanaikubali au kuikataa Katiba Mpya.

Tarehe 6 Aprili 2012, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar aliwateua Wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na kuwaapisha tarehe 13 Aprili, 2012. Tume ilianza kazi tarehe 2 Mei, 2012 na kuikamilisha Rasimu ya Katiba ambayo ilikabidhiwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar tarehe 30 Desemba, 2013.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akipokea Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba tarehe 30 Desemba, 2013*




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein akipokea Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba tarehe 30 Desemba, 2013*

Rasimu ya Katiba ilichapishwa kwenye Gazeti la Serikali na pia kwenye magazeti mengine yanayosomwa na wananchi kama ilivyoagizwa katika Kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Hatimaye, Mwenyekiti wa Tume, Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba aliwasilisha Rasimu hiyo mbele ya Bunge Maalum la Katiba tarehe 18 Machi, 2014. Bunge Maalum la Katiba linaundwa na Wabunge wa Bunge la Tanzania, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Wajumbe 201 walioteuliwa kutoka makundi mbalimbali yaliyoainishwa katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Bunge hilo lina jukumu la kujadili, kuamua na kutunga Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hatimaye wananchi watapata fursa ya kuipigia kura ya NDIYO au HAPANA.

***Bunge***

Katika kipindi cha Miaka 50 ya Muungano, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limetekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni kuwakilisha matakwa ya wananchi, kutunga Sheria za nchi, kusimamia utendaji wa Serikali na kupitisha Bajeti ya kila mwaka ya Serikali. Kimuundo, Bunge lina aina sita za Wabunge ambao ni Wabunge wa kuchaguliwa kuwakilisha majimbo ya uchaguzi; Wabunge wa Viti Maalum; Wabunge watano wa kuchaguliwa na Baraza la Wawakilishi; Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Wabunge wa kuteuliwa na Rais; na Spika iwapo hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa

Wabunge. Tangu kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria zinazopitishwa na Bunge hutiwa saini na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika miaka ya mwanzo ya Muungano, Bunge limepita katika vipindi mbalimbali vya uendeshaji wake kuanzia mwaka 1965. Bunge lilitekeleza majukumu yake chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa kilichokuwa na maamuzi ya juu kwa pande zote za Tanzania Bara na Zanzibar. Marekebisho ya Katiba ya Mpito yaliyofanyika mwaka 1975, yaliweka wazi kuwa utendaji wa Taasisi zote za Serikali likiwemo Bunge utatekeleza Sera za Chama kinachotawala. Aidha, mwaka 1979 Baraza la Wawakilishi la Zanzibar liliundwa likiwa na majukumu ya kutunga Sheria kwa mambo yasiyo ya Muungano kwa upande wa Zanzibar na kuisimamia na kuishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyokuwa kwa Bunge kwa upande wa Serikali ya Muungano.



*Jengo la Karimjee lililotumika kama Ukumbi wa Bunge mara baada ya Muungano mwaka 1964 mpaka mwaka 1994*



*Jengo Jipya la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma linalotumika sasa*

Kupatikana kwa Katiba ya Kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na kuungana kwa vyama vya TANU na ASP na kuzaliwa CCM mwaka 1977, kulileta demokrasia ya Chama Kimoja cha Siasa kulikoendeleza msingi wa chama kushika hatamu na kukifanya chama kuisimamia Serikali.
Kufuatia mabadiliko ya Katiba ya mwaka 1984, muundo wa Bunge ulibadilika

kwa kumuongeza Katibu wa Bunge na Sekretarieti ya Bunge pamoja na kutaja majukumu yao. Aidha, katika kipindi cha mwaka 1981 hadi 1995 idadi ya wabunge iliongezeka kutoka 225 na kufikia 254.


Kuanzishwa rasmi kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1992, kulisababisha kufanyika kwa marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweka utaratibu utakaoendana na mfumo huo. Mabadiliko ya Katiba yaliwaondoa Wakuu wa Mikoa kuwa Wabunge na pia yaliongeza idadi ya Wabunge kufikia 275 ambapo idadi ya Wabunge wanawake ilikuwa asilimia 15 ya Wabunge wote. Aidha, kutokana na marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977, Bunge nalo lilibidi lifanye marekebisho ya Kanuni na Taratibu zake ili kukidhi mahitaji ya mfumo wa Bunge la vyama vingi vya siasa. Marekebisho ya kanuni yalitambua uwepo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Pia, Bunge lilitunga Sheria ya Huduma za Bunge *(Parliamentary Service Commission Act, 1997)* inayotoa uhuru kwa Bunge kuwa na nguvu katika masuala ya ajira na utumishi wa wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge na masharti ya kazi za Wabunge.

Kupitia Uchaguzi Mkuu wa kwanza wa Vyama Vingi uliofanyika mwaka 1995, kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, Bunge lilipata Wabunge kutoka vyama tofauti vya siasa ambavyo ni CCM, NCCR-Mageuzi, CUF, CHADEMA na UDP. Hali hiyo ilibadili kwa kiasi kikubwa taswira ya Bunge la Tanzania. Idadi ya Wabunge iliendelea kuongezeka katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2005 na kufikia 295, huku Wabunge wanawake wakiwa 62. Kanuni za Bunge zilifanyiwa tena marekebisho ambapo Chama cha Upinzani kiliruhusiwa kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani iwapo kitafikisha asilimia 12.5 ya Wabunge wote.

Idadi ya Wabunge iliongezeka katika kipindi cha mwaka 2005 na 2010 hadi kufikia 323 huku idadi ya Wabunge wanawake ikifikia 100. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliongozwa na Chama cha CUF ambacho kilikuwa na idadi ya wabunge waliozidi asilimia 12.5. Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2010, Bunge limekuwa na jumla ya wabunge 357 kati yao, 239 ni wa kuchaguliwa kutoka katika majimbo ya uchaguzi, watano waliochaguliwa kutoka Baraza la Wawakilishi, 102 ni Wabunge wa Viti Maalum kutoka pande zote mbili za Muungano, 10 wa kuteuliwa na Rais, na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vyama vyenye uwakilishi katika Bunge hilo ni CCM, CHADEMA,

CUF, NCCR-Mageuzi, TLP na UDP. Kwa mara ya kwanza katika Miaka 50 ya Muungano, Bunge linaongozwa na Spika mwanamke, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda (Mb) kuanzia Desemba, 2010.

**Mchoro Na. 1:** Mgawanyo wa Wabunge wa Kuchaguliwa 2010




**Chanzo** *Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa*

***Utawala Bora***

Misingi mikuu ya utawala bora ni pamoja na utawala wa Sheria, haki za binadamu, mabadiliko ya uongozi, demokrasia ya vyama vingi, uwazi, uwajibikaji na maridhiano. Tangu kuasisiwa kwa Muungano, Tanzania imekuwa ikizingatia misingi ya utawala bora. Tanzania imekuwa na mabadiliko ya uongozi wa kidemokrasia ambapo kila baada ya miaka mitano hufanyika uchaguzi wa viongozi wa kitaifa na wa Serikali za Mitaa. Utaratibu huo umeijengea heshima na sifa Tanzania kwa kuwa na uchaguzi unaofanyika kwa uhuru, haki na amani. Tunapoadhimisha Miaka 50 ya Muungano, Taifa limeshuhudia awamu nne za Uongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na awamu saba za Uongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hupatikana kupitia chaguzi huru zinazofanyika kila baada ya miaka mitano.

Vilevile, katika kudhihirisha nafasi ya Taifa letu katika masuala ya utawala Bora kimataifa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alichaguliwa kuwa Kiongozi mwenye mchango

mkubwa zaidi katika maendeleo Barani Afrika kwa mwaka 2013 na kutunukiwa tuzo ya *Africa's Most Impactful Leader of the Year*. Tuzo hiyo ilitolewa na jarida la *African Leadership Magazine Group* la Marekani tarehe 9 Aprili, 2014. Tuzo hiyo hutolewa kwa viongozi wa Afrika ambao hutoa mchango mkubwa zaidi wa kiuchumi na kijamii kila mwaka kwa watu wao. Tukio hilo limeipa Tanzania sifa kimataifa na imeifanya kuwa nchi ya mfano na kituo cha uhakika cha uwezeshaji kutokana na mageuzi makubwa yaliyofanywa katika sera na mifumo ya uchumi. Huo ni ushahidi thabiti wa uwepo wa utawala bora na demokrasia nchini.

***Vyama vya Siasa***

Kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuruhusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini mwaka 1992 na kutungwa kwa Sheria Na.5 ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992, suala la uandikishaji wa vyama vya siasa liliorodheshwa miongoni mwa mambo ya Muungano. Mara baada ya mfumo wa vyama vingi kuanzishwa, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilianzishwa rasmi kwa mujibu wa Sheria Na.5 ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992, ambayo ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 1992.

Kufikia mwanzoni mwa mwaka 2014, vyama 21 vimepata usajili wa kudumu. Vyama hivyo ni *African Farmers Party* (AFP), APPT-Maendeleo, Chama Cha Mapinduzi (CCM); Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA); Chama Cha Haki na Ustawi Tanzania (CHAUSTA), *Civic United Front* (CUF), Demokrasia Makini, *Democratic Party* (DP), Jahazi Asilia, NCCR-Mageuzi, *National League for Democracy* (NLD), *National Reconstruction Alliance* (NRA), Sauti ya Umma (SAU), *Tanzania Democratic Alliance* (TADEA), *Tanzania Labour Party* (TLP), *United Democratic Party* (UDP), *Union for Multiparty Democracy* (UMD), *United Peoples Democratic Party* (UPDP), Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) na *Alliance for Democratic Change* (ADC). Kati ya Vyama hivyo, vyama 18 vilishiriki katika Uchaguzi Mkuu wa 2010. Aidha, vyama vifuatavyo vilianzishwa na baadaye kufutwa kutokana na kutokidhi masharti ya usajili. Vyama hivyo ni *Forum for the Restoration of Democracy* (FORD), *Popular National Alliance* (PONA) na *Tanzania Peoples Party* (TPP).

### 2.3.2 Ulinzi na Usalama

Ulinzi na usalama wa nchi ni muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii.  Kutokana na uwepo wa hali ya utulivu na amani nchini imewawezesha wananchi kuendelea na shughuli zao za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

***Ulinzi wa Nchi na Mipaka yake***

Tanzania imejijengea heshima na kupata sifa nyingi ndani na nje ya nchi kutokana na umahiri wa utendaji uliotukuka na nidhamu ya hali ya juu ya vyombo vyake vya ulinzi. Wakati tukisherekea Miaka 50 ya Muungano, Tanzania ina kila sababu za kujivunia umahiri wa Taifa katika ulinzi wa nchi na mipaka yake kutokana na kazi kubwa inayofanywa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). JWTZ liliundwa mwaka 1964 baada ya kuunganisha lililokuwa Jeshi la Ugombozi (JLU) Zanzibar na *Tanganyika Rifles* lililorithiwa toka kwa wakoloni wa Kingereza.

Tangu kuanzishwa kwake, JWTZ limetekeleza ipasavyo majukumu yake yakijumuisha kulinda mipaka ya nchi; kuwaandaa wananchi kushiriki katika shughuli za ulinzi wa Taifa; kushiriki katika ulinzi wa amani katika nchi zenye migogoro duniani; kusaidia Mamlaka za Kiraia kupambana na majanga; kufanya utafiti na kuendeleza teknolojia kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia; na kuimarisha amani na utangamano na nchi nyingine duniani.

Katika utekelezaji wa majukumu hayo, mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na ardhi, anga na bahari yake, imeendelea kuwa salama kutokana na ulinzi madhubuti wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Mifano hai ni jitihada za JWTZ kupambana na uvamizi uliokuwa ukifanywa na Wareno katika mipaka ya Tanzania na Msumbiji. Pia mfano mwingine ni jinsi JWTZ ilivyopambana katika vita dhidi ya nduli Idi Amini Dada aliyekuwa Rais wa Uganda alipoivamia nchi yetu mwaka 1978–79 na hatimaye kumng’oa.



*Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akipokea maelezo ya maendeleo ya Vita vya Kagera kutoka kwa Kamanda wa vita Meja Jenerali David Musuguri mwaka 1978 na huku Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Luteni Jenerali Abdallah Twalipo akifuatilia maelezo hayo*

Aidha, JWTZ lilitoa mchango mkubwa katika ukombozi wa Bara la Afrika katika kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje ya Ukombozi wa Bara la Afrika. Kufuatia kuundwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) mwaka 1963, Tanzania iliteuliwa kuwa mwenyeji na Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi ya OAU. Kutokana na uteuzi huo, JWTZ ilikabidhiwa jukumu la kushughulikia masuala ya ukombozi. Katika kutekeleza jukumu hilo, JWTZ iliunda kikosi maalum kwa ajili ya kuratibu na kutoa mafunzo ya kijeshi kwa wapigania uhuru wa vyama vya ukombozi vya nchi mbalimbali vikiwemo FRELIMO, MPLA, ZANU-PF, SWAPO, PAC na ANC ambavyo vilianzisha ofisi zao hapa nchini. Pia, Vikosi vya JWTZ kwa uamuzi wa Umoja wa Afrika lilishiriki kumuondoa Kanali Mohamed Bakar wa Anjouan katika Visiwa vya Comoro kufuatia kusudio lake la kutaka kujitenga na Muungano wa Visiwa hivyo. Hadi sasa JWTZ inashiriki katika operesheni ya kulinda amani huko Darfur, Lebanon, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo chini ya uongozi wa Umoja wa Mataifa.



*Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama akimkabidhi bendera kiongozi wa Batalioni ya wanajeshi wa JWTZ wanaokwenda kujiunga na jeshi la Umoja wa Mataifa la Kulinda Amani Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, mwaka 2013*

JWTZ imeshiriki pia katika kukabiliana na maafa yaliyoathiri maisha na mali za Watanzania. Hii ni pamoja na kushiriki katika shughuli za uokoaji na kusaka miili ya waathirika wa ajali ya meli ya MV Bukoba (21 Mei, 1996); ajali kubwa ya Treni ya Reli ya Kati Dodoma (1998); ajali ya meli ya MV Spice Islanders (10 Septemba, 2011); ajali ya Boti ya MV Skargit (18 Julai, 2012) huko Zanzibar; ajali ya jengo la ghorofa 16 lililoporomoka Dar es Salaam (29 Machi, 2013); ajali ya maporomoko ya machimbo ya moramu Arusha (01 Aprili, 2013); na kukabiliana na mafuriko mikoa ya Morogoro na Dodoma (Januari, 2014). Aidha, JWTZ imekuwa ikishiriki katika ujenzi wa miundombinu muhimu ikiwemo barabara na madaraja.

Katika kukidhi mahitaji ya wakati ya Jeshi katika ulinzi wa mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, masuala ya kufanya tafiti za teknolojia hayakwepeki. Mashirika ya MZINGA na NYUMBU yamekuwa kiini na chachu muhimu katika tafiti hizo. Shirika la MZINGA lililoko Morogoro lililoanzishwa Januari, 1971 ili kufanya tafiti mbalimbali za kijeshi pamoja na kuzalisha mazao ya kijeshi ili kuondokana na utegemezi wa upatikanaji wa mazao hayo kutoka nchi za nje. Shirika la MZINGA, mbali ya shughuli zake za msingi za

kijeshi, linaendelea kutoa huduma na bidhaa nyinginezo kwa matumizi ya kiraia kama vile vipuri vya mashine, mashine kwa matumizi ya wajasiriamali wadogo na wa kati, samani za kisasa na marisau za milimita 12.

Kwa upande wa Shirika la NYUMBU lililoko Kibaha Mkoa wa Pwani, liliundwa rasmi tarehe 14 Desemba, 1985 kwa lengo la kufanya utafiti na kuendeleza teknolojia ambazo zitalisaidia Jeshi kutekeleza majukumu yake na kuleta mapinduzi ya kiteknolojia nchini kwa kubuni na kuzalisha mitambo na magari ili kuwa na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Tangu kuanzishwa kwake, Shirika la NYUMBU limewajengea uwezo wataalamu 66 kwa kuwawezesha kupata mafunzo nje ya nchi katika ngazi na fani mbalimbali za teknolojia ya usanifu na uzalishaji wa magari pamoja na viambata vyake, kukalibu chuma, kudhibiti ubora wa bidhaa, utawala, uhandisi mitambo, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Teknolojia ya kusanifu na kuunda magari ya kijeshi na magari kwa ajili ya matumizi maalum imehaulishwa kama miradi ya utafiti.  Katika tafiti hizo, mradi wa gari la NYUMBU ulioanza mwaka 1978 umezalisha jumla ya magari 50 ya majaribio katika miundo mbalimbali kwa ajili ya mahitaji ya kijeshi ya kubeba askari na mizigo, kusomba maji na kubeba malighafi za ujenzi wa barabara na nyumba za askari. Shirika linaendelea kuzalisha magari ya Nyumbu ambayo yanatumika na Jeshi kwa kutumia uwezo wake wa ndani.




*Gari aina ya Nyumbu lililoundwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania*

Vilevile, kati ya mwaka 1986 hadi 1991 yalitengenezwa magari ya zimamoto aina tatu (*Municipal Fire Tender - MFT)* kwa ajili ya maeneo ya miji, (*Rapid Intervention Vehicle - RIV)* kwa ajili ya viwanja vya ndege na (*Crash Fire Tender - CFT)* kwa ajili ya viwanja vikubwa vya ndege na vituo vya mafuta. Magari hayo yamejaribiwa na kuonesha uwezo na ufanisi mkubwa na yalinunuliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kukabidhiwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa Dar es Salaam. Vifaa hivyo vyenye uwezo mkubwa, vimewezesha uwanja huo wa ndege kupandishwa daraja na hivyo kuwezesha ndege ambazo zilizuiliwa kuweza kutua.

Kupitia ushirikiano wa kijeshi na nchi mbalimbali duniani, Serikali imeanzisha na kuendesha shughuli mbalimbali zenye manufaa kwa pande zote za Muungano. Kwa mfano, kupitia Serikali ya Ujerumani, huduma za afya zimeimarishwa katika hospitali za Jeshi kama vile Bububu (Zanzibar), Lugalo (Dar es Salaam) na nyingine za kanda na hivyo kuzifanya kuwa hospitali muhimu kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Aidha, Serikali ya China imeliwezesha JWTZ kuongeza uwezo wa ulinzi baharini kwa kutoa vifaa na mafunzo ili kuimarisha uwezo wa kupambana na vitendo vya uharamia vilivyokuwa vimekithiri. Hivi sasa vitendo hivyo vimedhibitiwa.

### *Usalama wa Raia Ndani ya Nchi*

Jukumu la usalama wa raia na mali zao na usimamizi na utekelezaji wa Sheria za nchi linatekelezwa na Jeshi la Polisi Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura 322. Jeshi hilo limetokana na kuunganishwa kwa Jeshi la Polisi Zanzibar na Jeshi la Polisi Tanganyika. Katika kipindi cha Miaka 50 ya Muungano, Jeshi la Polisi limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuzuia na kupambana na uhalifu; kuwakamata wahalifu; kupeleleza makosa ya jinai; kuhakikisha Sheria za nchi zinafuatwa; na kudumisha usalama na amani ya nchi.

Katika kuimarisha ushiriki wa wananchi katika masuala ya ulinzi na usalama wa watu na mali, mipango ya ulinzi shirikishi na Polisi Jamii imeanzishwa. Mipango hiyo imesaidia sana kupunguza uhalifu nchini. Mipango ya Polisi Jamii inayoendelea ni ulinzi jirani, usalama wetu kwanza, Polisi kata/shehia, safiri salama, ukamataji salama, programu ya vijana mitaani/vijiweni ni miongoni mwa mbinu zinazotumika katika pande mbili za Muungano kushirikisha jamii katika kupunguza uhalifu.




*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Oysterbay, Dar es Salaam wakiwa katika Mafunzo kwa Vitendo katika Somo la* ***Usalama Wetu Kwanza*** *linalofundishwa na Jeshi la Polisi Tanzania*

Jeshi la Polisi linaendelea na jitihada za kujijengea uwezo chini ya Programu ya Maboresho ya Jeshi hilo kwa lengo la kuimarisha utendaji, maslahi na upatikanaji wa nyumba bora za kuishi askari. Programu hiyo imelenga kuimarisha mifumo ya utendaji kazi za Polisi katika kuzuia uhalifu, upelelezi wa makosa ya jinai na Vikosi vya kuitikia kwa haraka wito, taarifa za wananchi kuhusu uhalifu na wahalifu, na kuimarisha doria nchini. Mafunzo kwa askari polisi yameimarishwa kwa kuinua hadhi ya Vyuo vya Polisi na kuvisajili kuwa *Police Academies.* Pia, kupitia Programu hiyo mifumo ya Sheria, Kanuni, muundo wa taasisi, teknolojia ya habari na mawasiliano, miundombinu na vitendea kazi vimeimarishwa.

### *Huduma za Uhamiaji*

Masuala ya udhibiti wa wahamiaji yalianzishwa mwaka 1924, chini ya Sheria ya Uhamiaji *Immigration Ordinance* Sura 37 ya mwaka 1924 ili kusimamia uhamiaji ndani ya Tanganyika. Sheria hiyo ilianza kutumika tarehe 1 Februari, 1925. Kuanzia mwaka 1924 hadi mwaka 1948, shughuli za udhibiti wa wahamiaji na utoaji wa pasipoti zilifanywa na kitengo maalum ndani ya Idara ya Polisi. Idara ya Uhamiaji ilianzishwa rasmi tarehe 13 Julai, 1949 na mwezi Oktoba, 1949 ilibadilishwa jina na kuitwa Idara ya Uhamiaji na Pasipoti

*(Immigration and Passport Department).* Baada ya Tanganyika kupata uhuru tarehe 09 Desemba, 1961, Idara iliendelea kuitwa Idara ya Uhamiaji na Pasipoti ikiwa na majukumu ya utoaji wa Viza kwa wageni walioomba kuingia Tanganyika kwa shughuli mbalimbali, kufanya misako, doria pamoja na shughuli nyingine za upelelezi.

Baada ya Muungano, majukumu ya Idara ya Uhamiaji yalipanuka. Kwa upande wa Tanzania Bara, utendaji kazi wa Idara ya Uhamiaji kuhusu masuala ya uraia uliendelea kusimamiwa na Sheria ya Uraia Na.3 ya Mwaka 1961 *(The Tanganyika Citizenship Act. No.3 of 1961)* na Sheria ya Uraia ya Mwaka 1962 *(The Tanganyika Citizenship Act No.15 of 1962).* Kwa upande wa Zanzibar, masuala ya Uraia yalisimamiwa na Sheria ya Uraia ya Zanzibar *(The Zanzibar Nationality Decree of 1952).* Sheria zote hizo zilifutwa baada ya kutungwa kwa Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 *(the Tanzania Citizenship Act No. 6 of 1995).* Masuala ya udhibiti wa wahamiaji yaliendelea kusimamiwa na Sheria ya Uhamiaji *(Immigration Ordinance of 1961)* iliyofutwa na Sheria Na. 41 ya mwaka 1963 *(Immigration Act No.41 of 1963)* ambayo pia ilifutwa na Sheria ya Uhamiaji Na.8 ya Mwaka 1972 *(The Immigration Act No. of 1972).* Majukumu ya Idara ya Uhamiaji yalisimamiwa na Tamko la Kanuni na Udhibiti wa Uhamiaji la mwaka 1923 *(Immigration Regulation and Restriction Decree, Cap 43 of 1923)* huko Zanzibar.



*Maafisa wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar wakitoa huduma kwa wananchi*

Mwaka 1995, Sheria zilizokuwa zinasimamia majukumu ya uhamiaji, Tanzania Bara na Zanzibar zilifutwa na kutungwa Sheria mpya ya Uhamiaji Na.7 ya Mwaka 1995 na Kanuni zake za mwaka 1997. Aidha, Sheria zilizokuwa zinasimamia masuala ya Uraia ziliunganishwa na kuwa Sheria ya Uraia Na.6 ya Mwaka 1995 na Kanuni zake za Mwaka 1997. Ili kuboresha huduma za pasipoti, Serikali ilitunga Sheria ya Kusimamia Utoaji wa Pasipoti na Hati za Safari mwaka 2002 *(Tanzania Passport and Travel Document Act No. 20 of 2002)* na Kanuni zake za mwaka 2004.

Idara ya Uhamiaji imeendelea kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu nchini; kusimamia ukaazi wa wageni nchini kwa mujibu wa Sheria; kutoa Pasi za Kusafiria na Hati nyingine za safari kwa raia wenye sifa; na kuratibu maombi ya uraia wa Tanzania kwa wageni wanaoishi nchini. Maboresho hayo yamejumuisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika uchukuaji, utunzaji wa kumbukumbu za wageni wanaoingia na kutoka nchini, utoaji wa Viza kwa wageni wanaoomba kuingia nchini na uchapishaji wa Pasipoti.

***Utambulisho wa Uraia wa Tanzania***

Kwa kipindi kirefu tangu kuasisiwa kwa Muungano, utambulisho wa raia wa Tanzania na wasio raia ulikuwa unafanyika kwa kutumia Hati za Kusafiria, Hati za Vizazi na Vifo, Serikali za Mitaa (nyumba kumi-kumi). Tarehe 30 Julai, 2008, Serikali iliunda Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa Hati Maalum ya Rais, Tangazo la Serikali Na.122. Majukumu ya Mamlaka hiyo ni kuhakiki uraia wa watu waishio nchini na kusajili taarifa zao, kuwapatia vitambulisho na kutengeneza Daftari la Kudumu lenye taarifa za utambuzi wa watu ambazo pia zitatumiwa na wadau wengine pamoja na kujenga mfumo wa utambuzi na usajili wa watu kitaifa. Hata hivyo, kwa upande wa Zanzibar kuna vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ambavyo vinatumika kama hati ya utambulisho.

Serikali kupitia NIDA imeanzisha Kituo cha Uchambuzi ambacho kinafanya kazi ya uhakiki na uingizaji wa taarifa za watu kwenye Mfumo wa Utambuzi na Usajili na kutoa Vitambulisho vya Taifa tangu Februari, 2013. Mamlaka hii imesajili wafanyakazi wa Serikali wanaoishi Dar es Salaam na Zanzibar ambao jumla ni takriban 290,000. Wafanyakazi wa Taasisi za Serikali wamekwisha-kamilisha usajili na kupewa vitambulisho vyao. Aidha, Mamlaka

imesajili wananchi waishio Dar es Salaam wapatao 2,159,822 katika awamu ya kwanza.

Usajili wa awamu ya pili wa uchukuaji wa alama za kibaiolojia umefanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo hadi mwezi Machi 2014, wananchi wapatao 1,511,875 sawa na asilimia 70 ya wananchi waliosajiliwa awali walikuwa wamechukuliwa alama za vidole na kupigwa picha. Kwa upande wa Zanzibar hadi kufikia Machi, 2014, Mamlaka ilikuwa imekamilisha utambuzi na usajili wa wakazi 184,296 na wageni 180. Uchukuaji wa alama za kibaiolojia na picha umekamilika kwa Mikoa yote ya Unguja na zoezi linaendelea katika mikoa ya Pemba.




*Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akipokea Kitambulisho cha Taifa kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Emmanuel John Nchimbi mwaka 2013*

### 2.3.3 Diplomasia na Ushirikiano wa Kimataifa

Kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulikuwepo uhusiano na ushirikiano wa kimataifa ambapo pande zote mbili za Muungano zilikuwa zimeshaanzisha uhusiano wa kidiplomasia na ushirikiano na nchi kadhaa ulimwenguni. Mara baada ya muungano, masuala ya mambo ya nje yaliorodheshwa katika Hati ya Muungano na Wizara ya Mambo ya Nje ilianzishwa kwa lengo la kuratibu masuala yote ya mambo ya nje.

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 1964 hadi miaka ya 1980, Tanzania ilijishughulisha sana na suala la uhuru, ulinzi wa mipaka na harakati za ukombozi wa nchi ambazo zilikuwa hazijapata uhuru. Tanzania ilifanya hivyo kwa kutumia njia za kidiplomasia zikiwemo ushawishi mkubwa na misimamo thabiti katika taasisi za kikanda na za kimataifa. Taasisi hizo ni pamoja na Nchi za Mstari wa Mbele (*Front Line States*); Klabu ya Mulungushi; Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (OAU); Umoja wa Wakereketwa wa Uhuru na Utu wa Mwafrika na Watu Weusi (*Pan-African Movement*); Nchi zisizofungamana na Upande Wowote (*Non-Aligned Movement*); Jumuiya ya Madola na Umoja wa Mataifa. Wakati wote, Tanzania ilifanya jitihada kubwa ili kupata sauti ya pamoja katika masuala yote yaliyohusu maslahi ya nchi na Afrika. Jitihada hizo zilifanywa kwa lengo la kuimarisha amani, usalama na haki katika Jumuiya yote ya Kimataifa.



*Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa na Viongozi Wakuu wa Nchi zisizofungamana na upande wowote mwaka wa 1970*

Katika miaka ya 1990, Sera ya Mambo ya Nje ilibadilika kufuatia kukamilika kwa mchakato wa ukombozi katika Bara la Afrika, kukomeshwa kwa siasa za kibaguzi nchini Afrika Kusini; kumalizika kwa vita baridi; kuibuka kwa utandawazi na mageuzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, hususan mfumo wa vyama vingi vya siasa. Mabadiliko hayo yalilazimisha Sera ya Mambo ya Nje kuhuishwa mwaka 2001 ili kuzingatia changamoto na mabadiliko ndani na nje ya nchi. Pamoja na kuendeleza misingi ya sera ya awali ya mambo ya nje, kwa sasa msisitizo umewekwa katika diplomasia ya kiuchumi kuweka mikakati endelevu ya kuwavutia wawekezaji, kuongeza biashara na utalii kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuchochea maendeleo.

Kwa upande wa ushirikiano wa Afrika Mashariki, Tanzania ilikuwa mwanachama mwanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyoundwa mwaka 1967. Lengo la kuanzishwa kwa Jumuiya hiyo ilikuwa kuimarisha na kuongeza uhusiano uliopo kati ya nchi wanachama katika masuala ya Biashara, Uchumi na shughuli nyingine ili kuleta maendeleo ya haraka ambayo matunda yake yatagawanywa kwa uwiano kati ya nchi wanachama. Hata hivyo, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilivunjika mwaka 1977, kutokana na itikadi tofauti za kisiasa zilizokuwa zikifuatwa na nchi wanachama; kutoelewana katika mgao wa mapato kutoka katika mashirika ya huduma za pamoja na kukosekana kwa sera ya kushughulikia tatizo hilo. Kuvunjika kwa Jumuiya hiyo kulizilazimu nchi wanachama kuchukua jukumu la kutoa huduma zilizokuwa zikitolewa na iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mambo yaliyoingizwa kwenye Muungano baada ya kuvunjika kwa jumuiya hiyo ni Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yanayohusika na kazi za Baraza hilo; usafiri na usafirishaji wa anga; takwimu; utabiri wa hali ya hewa na utafiti. Aidha, kutokana na kuvunjika kwa Mahakama ya Rufaa ya Afrika Mashariki mwaka 1979, suala la Mahakama ya Rufani Tanzania nalo liliongezwa katika orodha hiyo.

Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki kati ya nchi za Uganda, Kenya na Tanzania iliundwa mwaka 1999. Tofauti na jumuiya ya awali iliyovunjika, Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki yenye watu milioni 122 imejielekeza katika kutoa fursa mbalimbali kama vile utalii, biashara na uwekezaji kupitia Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja na Umoja Sarafu. Wakuu wa nchi hizo walisaini Mkataba wa Jumuiya hiyo mpya tarehe 7 Julai, 2000 na kuanza kazi rasmi mwaka huo. Hadi Machi, 2014, Jumuiya ilikuwa imefikisha wanachama

watano baada ya Burundi na Rwanda kujiunga mwaka 2007. Mataifa mengine ya ukanda wa Afrika Mashariki yanaendelea kuomba kujiunga na Jumuiya hiyo. Kutokana na makubaliano ya nchi wanachama, nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilitakiwa kuanzisha wizara za kushughulikia masuala ya ushirikiano wa Afrika Mashariki. Tanzania ilianzisha rasmi wizara hiyo mwaka 2006 ili kushughulikia masuala ya mtangamano wa Jumuiya na kubaini fursa za uchumi zinazopatikana katika nchi nyingine wanachama kwa maslahi ya Taifa. Kutokana na umuhimu wa lugha ya Kiswahili, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya kwa lengo la kukuza lugha hiyo katika ukanda huu. Makao Makuu ya Kamisheni hiyo yako Zanzibar.

Kwa upande wa Kusini, Tanzania ilijiunga na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (Southern Africa Development Community - SADC) ambayo ilianza kama klabu ya Mulungushi na baadaye ikawa Tume ya Nchi za Mstari wa Mbele ya kuratibu ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. Jumuiya hii yenye idadi ya watu milioni 250 inatoa fursa za utalii, biashara na uwekezaji na ipo katika hatua ya mwanzo ya kuanzisha Umoja wa Forodha (Free Trade Area - FTA). Wakati huo huo, mchakato wa kuasisi Soko Huru la Pamoja litakalohusisha Jumuiya tatu za COMESA, EAC na SADC ambao ulianza mwaka 2008 unaendelea na litahusisha watu wanaokadiriwa kuwa milioni 530.

***Umoja wa Nchi za Afrika***

Tanzania ilikuwa mwanachama wa mstari wa mbele wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) na inaendelea kuwa hivyo katika Umoja wa Afrika. Katika vipindi tofauti Tanzania imeongoza Umoja wa Afrika katika ngazi mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka 1984-1985 Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa Mwenyekiti wa OAU na Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete alishika wadhifa huo mwaka 2008. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Umoja huo na kuongoza mfululizo kuanzia mwaka 1989-2001. Ni katika kipindi hicho, wazo la kuufanyia mabadiliko makubwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika lilipoanza. Pamoja na viongozi hao wakuu kuongoza Umoja wa Afrika kwa vipindi hivyo, Mheshimiwa Getrude Mongela alichaguliwa kuwa Spika wa Kwanza wa Bunge la Afrika mwaka 2004 na Mheshimiwa Amina Salum Ali alishika wadhifa wa Balozi wa Umoja wa Afrika kwenye Umoja wa Mataifa mwaka 2006.
Pamoja na Mchango mkubwa uliotolewa na Viongozi wa Tanzania walioongoza

Umoja wa Afrika, Umoja wa Nchi Huru za Afrika na hatimaye Umoja wa Afrika umetumika kama Jukwaa la Tanzania kutoa sauti yake kuendeleza utamaduni wa kupigania haki, usawa na maendeleo ya watu wa Bara la Afrika na dunia nzima. Katika miaka ya 1970 na 1980, Tanzania ilitumia kikamilifu jukwaa la Umoja wa Nchi Huru za Afrika kuwasilisha na kuendeleza fikra za kupigania ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika na kujenga umoja, mshikamano na ushirikiano wa kiuchumi na kijamii barani Afrika. Kwa upande wa ukombozi chini ya wakuu wa nchi za kiafrika, na hasa nchi za mstari wa mbele, Kamati Ndogo ya Ukombozi ilianzishwa. Makao Makuu ya Kamati hiyo yalikuwa nchini Tanzania na kazi yake kubwa ni kuratibu juhudi za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika zikiwemo, Zimbabwe, Namibia, Msumbiji, Angola, Sao Tome na Principe na Guinea Bissau na kutokomeza ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini. Baada ya kazi ya ukombozi wa Bara la Afrika kukamilika, kazi kubwa imeendelea kufanywa na Tanzania chini ya Umoja wa Afrika kwa kushiriki kutatua migogoro mbalimbali inayolikumba Bara hili na pia kuchangia katika jitihada za kuinua hali ya uchumi kwa waafrika wote.

Baada ya mjadala wa kina na wa muda mrefu, nchi za Afrika zilikubaliana kujenga umoja hatua kwa hatua badala ya kufanya uamuzi wa kuungana mara moja. Aidha, ilikubalika kuwa umoja huo utajengeka kupitia ushirikiano na mtangamano wa kikanda kama vile EAC, SADC, COMESA na ECOWAS.

Tanzania pia imekuwa mshiriki mzuri wa kuandaa mipango ya kiuchumi ya Umoja wa Afrika na kuitekeleza hapa nchini. Mipango hiyo ni pamoja na *The New Partneship for Africa's Development* (NEPAD) na *Comprehensive Africa's Agriculture Development Programme* (CAADP). Kufuatia kukamilika na kuidhinishwa mpango wa CAADP kila nchi mwanachama ilitakiwa kuandaa mpango wake wa utekelezaji utakaohakikisha usalama wa chakula kwa kuongeza uwekezaji kwenye Sekta ya Kilimo. Tanzania ni miongoni mwa nchi za kwanza barani Afrika kuandaa mpango wa usalama wa chakula na uwekazaji kwenye kilimo unaojulikana kama *Tanzania Food Security Investment Plan* (TAFSIP).

***Umoja wa Mataifa***

Kama ilivyo katika Umoja wa Afrika, Tanzania imeendeleza msimamo wake katika Umoja wa Mataifa kwa kupigania haki, usawa wa binadamu, maendeleo ya nchi changa na kupinga ukoloni. Kutokana na msimamo wake, Tanzania

ilipewa heshima ya kuwa mwanachama wa muda wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa katika vipindi viwili tofauti, mwaka 1975 na mwaka 2006.

Baadhi ya Watanzania wameweza kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi wa juu na za kawaida katika Ofisi za Umoja wa Mataifa na mashirika yake. Baadhi yao ni Mheshimiwa Dkt. Asha Rose Migiro, ambaye alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim ambaye alikuwa Rais wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka ambaye alikuwa Msaidizi Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Makazi Duniani, na Balozi Getrude Mongela ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Mkutano wa Wanawake Duniani uliofanyika Beijing, China mwaka 1995. Pia, Tanzania ilipewa jukumu la kuwa Mwenyekiti Mwenza, sambamba na China, wa Kundi la Nchi 77 mwaka 1998 ambapo iliifanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa. Pia Balozi Alli Mchumo aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Mazao Duniani *(Common Fund for Commodities – CFC),* ambao ni moja ya taasisi za Umoja wa Mataifa, na Dkt. Frannie Leautier ambaye alikuwa Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia kwa miaka 7 na baadaye Katibu Mtendaji wa Mfuko wa Ujenzi wa Uwezo Barani Afrika hadi mwaka 2013.

Baada ya kwisha kwa ukoloni, Sauti ya Tanzania kwenye Umoja wa Mataifa kupitia hotuba za kila mwaka za Viongozi kwenye Mkutano mkuu wa Umoja huo na mabalozi wetu zimesisitiza umuhimu wa kuheshimu haki za watu wote duniani na uhuru wa mataifa yote. Mara nyingi, Tanzania imesisitiza umuhimu wa kuheshimiwa kwa haki za watu wa Palestina na Sahara Magharibi pamoja na jamii nyingine zote zinazokandamizwa duniani. Tanzania pia imeshiriki kutekeleza mipango na mikataba mbalimbali ya Umoja wa Mataifa ikiwemo Malengo ya Milenia, Mikataba kuhusu Mazingira na Tabia Nchi, Mipango ya Utawala Bora nakadhalika. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka utaratibu mzuri wa kutekeleza makubaliano hayo ya kimataifa ambapo mpango wa nchi wa utekelezaji huandaliwa kwa kushirikisha pande zote za muungano. Mipango hiyo huwekewa muda maalum, mtekelezaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal akishiriki Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Ukimwi uliofanyika jijini New-York tarehe 10 Juni 2011*

### 2.3.4 Masuala ya Kiuchumi ya Muungano


***Usimamizi wa Kodi ya Mapato, Ushuru wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa***

Kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, usimamizi wa Kodi ya Mapato kwa Tanganyika na Zanzibar ulikuwa chini ya Kodi ya Mapato ya Afrika Mashariki. Kwa wakati huo tafsiri ya Afrika Mashariki ilikuwa inajumuisha nchi za Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar. Mwaka 1965, tafsiri hiyo ilifutwa na tafsiri mpya ikawa Kenya, Uganda na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kufuatia tafsiri hiyo mpya, Kodi ya Mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania iliwekwa chini ya usimamizi wa Idara ya Forodha na kuwa miongoni mwa Mambo ya Muungano.

Hadi mwaka 1977, baadhi ya kodi za ndani zilikuwa zinakusanywa na Serikali wakati kodi kubwa kama Kodi ya Mapato na Ushuru wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa zilikuwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya hiyo mwaka 1977, majukumu ya usimamizi wa kodi yaliwekwa chini ya Serikali. Kutokana na kukosekana kwa wafanyakazi wenye utaalam na uzoefu mkubwa wa ukusanyaji mapato ya kodi, Serikali ilifanya maboresho yaliyochangia kuanzishwa kwa Idara ya Mapato ya Ndani na Mauzo, na Idara ya Ushuru wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa.

Mwaka 1996, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilianzishwa kwa Sheria Na.11 ya mwaka 1995. Mamlaka hiyo imepewa majukumu ya kutathmini, kukusanya na kusimamia mapato yote ya Serikali Kuu; kuishauri Serikali katika mambo yote yanayohusiana na Sera za Fedha na uhamasishaji wa ulipaji wa kodi kwa hiari; kutoa takwimu za kibiashara na machapisho. Vilevile, TRA imepewa jukumu la kuboresha huduma kwa walipa kodi na kusimamia ipasavyo Sheria zote zinazohusu Mapato ya Serikali kuu. Wakati Mamlaka ya Mapato Tanzania inasimamia Kodi ya Mapato na Ushuru wa Forodha ambayo ni mapato ya Muungano kwa Tanzania Bara na Zanzibar, Bodi ya Mapato Zanzibar *(Zanzibar Revenue Board – ZRB)* husimamia kodi zisizo za Muungano kwa upande wa Zanzibar. TRA imeweka mfumo wa ulipaji kodi kuwa wa kielektroniki ikiwemo mfumo wa kompyuta wa leseni za udereva na mfumo wa kulipa ada za mwaka za magari kwa kutumia simu za mkononi. Pia, TRA inatumia Mifumo ya kulipa kodi kwa Mtandao, taarifa za kuingiza na kuuza bidhaa nje ya nchi, kufuatilia magari ya mizigo yanayosafirishwa nje ya nchi, udhibiti wa bidhaa bandarini na maabara ya utambuzi wa nyaraka zinazohusishwa na ukwepaji wa kodi kwa ajili ya uchunguzi. Kutokana na jitihada hizo, ukusanyaji wa mapato umeongezeka kutoka shilingi bilioni 506 mwaka 1996/97 hadi shilingi bilioni 7,906 mwaka 2012/13.

**Mchoro Na. 2:** Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato Kuanzia Mwaka 1996/97-2012/13




**Chanzo:** *Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)*

Vilevile, malipo ya kodi yanafanywa kwa njia ya mtandao na hivyo kuimarisha huduma kwa walipakodi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Aidha, maboresho yamefanywa katika forodha na kuwezesha kuwa na mfumo mzuri wa taarifa za kuingiza na kuuza bidhaa nje ya nchi. Uhusiano na ushirikiano kati ya Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania umezidi kuimarishwa.



*Jengo jipya la Makao Makuu ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) lililoanza kutumika mwaka 2013*

### *Mfumo wa Uhusiano wa Kifedha wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar*

Nadharia ya Mifumo ya Uhusiano wa Kifedha kwa nchi zinazounda Muungano au Shirikisho duniani, inabainisha aina tatu za mifumo ya uhusiano wa kifedha inayoweza kutumiwa na nchi zinazoamua kuunda Muungano au Shirikisho. Mifumo hiyo ni:

a) Mfumo unaotoa mamlaka makubwa ya Sera za Kodi kwa nchi zenye kuunda Muungano *(High Fiscal Autonomy).* Katika mfumo huo,

kila nchi yenye kuunda Muungano inayo mamlaka makubwa katika kusimamia Sera za Kodi, hususan mipango ya mapato na matumizi ikiwemo kuanzisha na kutoza kodi kwa mujibu wa Sheria. Mfumo huo huwa na akaunti ya fedha ya pamoja ambayo huchangiwa na nchi zenye kuunda Muungano na fedha hizo hutumika kugharamia Mambo ya Muungano. Uwiano wa idadi ya watu katika nchi zenye kuunda Muungano ni kigezo kikuu kinachotumika kuchangia kwenye akaunti ya fedha ya pamoja. Mfumo huo unatumika Hong Kong, Bosnia na Herzegovina.

b) Mfumo unaotoa mamlaka ya wastani kwa Sera za Kodi kwa nchi zenye kuunda Muungano *(Moderate Fiscal Autonomy).* Chini ya mfumo huo, kila nchi inayounda Muungano hupokea mgao unaotokana na vyanzo vyote vya mapato ya Muungano isipokuwa misaada au mikopo inayoelekezwa katika miradi maalum. Nchi husika zina mamlaka ya kupanga na kusimamia mapato yatokanayo na vyanzo visivyo vya Muungano na matumizi kwa mambo yasiyo ya Muungano. Mfumo huo unatumika katika nchi za Kanada, India, Marekani na Uswisi.

c) Mfumo wa tatu ni ule unaoainisha Sera za Kodi kwa nchi zenye kuunda Muungano *(Full Harmonization of Fiscal Regime).* Chini ya mfumo huo, viwango vya kodi huwa sawa kwa nchi zote zenye kuunda Muungano. Uandaaji na usimamizi wa Sera za Kodi, hususan Sera za Mapato na Matumizi hufanyika kwa ushauriano wa pamoja. Lengo ni kuondoa ushindani wa kodi ambao unaweza kuathiri uchumi wa nchi zinazounda Muungano. Mfumo huo unatumika katika nchi za Australia, Finland na Ujerumani.

Mfumo wa uhusiano wa kifedha unaotumika na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sasa ni wa aina tofauti na aina tatu ya mifumo ya uhusiano wa kifedha inayojulikana kwa nchi zinazounda muungano au shirikisho. Mfumo uliopo sasa unabainisha kuwa pande zote mbili za Muungano zinapata mapato yake kutokana na vyanzo vya kodi na visivyo vya kodi, misaada kutoka nje na gawio kutoka kwenye mashirika. Kila upande wa Muungano hukusanya mapato hayo na kuyaingiza kwenye Mfuko wake Mkuu. Kwa upande wa SMT, mapato hayo hutumika kugharamia mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa Tanzania Bara. Kwa upande wa SMZ, mapato

hayo hugharamia mambo yasiyo ya Muungano. Aidha, SMZ imekuwa ikipata mgao wa asilimia 4.5 ya misaada isiyo ya masharti kutoka nje na mgao wa asilimia 4.5 ya gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Taratibu za ukopaji na ulipaji madeni zinasimamiwa na Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada Namba 30 ya mwaka 1974, kama ilivyorekebishwa mwaka 2004. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, SMT ndiyo yenye mamlaka ya kutekeleza Sheria hiyo. Hivyo, SMZ hupata mikopo ya nje kupitia SMT kwa kutumia mikataba ya ndani (*on lending agreement).* Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaweza kukopa ndani ya nchi bila idhini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika kuhakikisha kuwa kuna uhusiano bora wa kifedha kati ya pande mbili za Muungano, Serikali iliunda Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Finance Commission)* kwa Sheria Na.140 ya mwaka 1996. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Pamoja ya Fedha imepewa majukumu ya kuchambua mapato na matumizi yanayotokana na, au yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali zote mbili kuhusu mchango na mgao wa kila Serikali. Tume pia ina jukumu la kuchunguza mfumo wa shughuli za fedha za Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha katika Serikali mbili. Katika kutekeleza majukumu hayo, Tume imechambua na kubaini gharama za uendeshaji wa Wizara na Taasisi za Muungano; imechambua madeni na misaada kati ya SMT na SMZ; imependekeza marekebisho ya Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Sura ya 140 na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa; na kubainisha vyanzo vya mapato ya Muungano, kuchambua vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za mambo ya Muungano.

### *Sarafu, Benki na Fedha za Kigeni*

Kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1964, kulisababisha nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa na sarafu zake na mipango yake ya kusimamia mambo ya kibenki na fedha. Hivyo, tarehe 10 Juni 1965, jambo la sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yote halali, benki na shughuli zote za benki, fedha za kigeni na usimamizi wa mambo yote yanayohusu fedha za kigeni liliingizwa katika mambo ya Muungano.

Mwaka 1966, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha Benki Kuu ya Tanzania kupitia Sheria ya Mabenki ya mwaka 1965. Jukumu la msingi la Benki hiyo ni kuandaa na kutekeleza Sera za Fedha zinazolenga

kutunza thamani ya fedha na kudhibiti mfumuko wa bei ili kuchochea ukuaji uchumi nchini. Majukumu mengine ni pamoja na kutunza akiba ya fedha za kigeni, kuwa mkopeshaji mkuu kwa Serikali zote mbili pamoja na Benki za Kibiashara, kuchapisha noti na kutengeneza sarafu.

Katika kipindi cha mwaka 1967 hadi 1991, Benki Kuu ilijielekeza zaidi kutimiza malengo ya kukuza uchumi uliohodhiwa na dola katika mwelekeo wa ujamaa na kujitegemea. Katika kipindi hicho, Sera za Fedha zilitegemea maelekezo kutoka Serikali Kuu na zilitekelezwa kwa kutumia miongozo ya fedha na mikopo sanjari na udhibiti wa riba na upatikanaji wa mikopo na fedha za kigeni. Mwaka 1986, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilichukua hatua za kukabiliana na ongezeko kubwa la ujazi wa fedha, mfumuko wa bei, kuporomoka kwa thamani ya shilingi na kudhoofu kwa kasi ya ukuaji uchumi uliolenga kuipa Sekta Binafsi nafasi kubwa ya kuchangia ukuaji wa uchumi.

***Usimamizi wa Shughuli za Benki na Sekta ya Fedha***

Tangu Benki Kuu ilipopewa jukumu la kusimamia benki na taasisi za fedha nchini mwaka 1991, imesimamia na kuhakikisha sekta ya fedha inakuwa imara, salama na inakua. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Desemba, 2013, kulikuwa na jumla ya benki na taasisi za fedha 53 zenye matawi 622 nchini kote ikilinganishwa na mwaka 1980 ambapo kulikuwa na benki sita (6) tu ikiwemo Benki ya Watu wa Zanzibar *(People's Bank of Zanzibar)* iliyoanzishwa mwaka 1966. Benki nyingine zilikuwa ni Benki ya Rasilimali Tanzania *(Tanzania Investment Bank - TIB ),* Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini *(Tanzania Rural Development Bank - TRDB)*, Benki ya Nyumba Tanzania *(Tanzania Housing Bank),* Benki ya Akiba ya Posta *(Postal Office Savings Bank)* na Benki ya Taifa ya Biashara *(National Bank of Commerce).* Kuongezeka kwa idadi ya benki na kupanuka mtandao wa matawi kumewezesha benki nyingi kufungua matawi yake Tanzania Bara na Zanzibar. Baadhi ya benki ambazo zina matawi pande zote mbili za Muungano ni *NMB Bank Plc, CRDB Bank Plc, EXIM Bank (T) Ltd, Tanzania Postal Bank, Federal Bank of the Middle East Ltd, Barclays Bank Tanzania Ltd* na *KCB Bank Ltd*.



*Jengo la Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Sekta ya Benki nchini imeendelea kuimarika kimtaji, ukwasi na amana. Pia utoaji mikopo kwenye sekta binafsi umezidi kuongezeka. Kufikia mwishoni mwa Desemba, 2013, sekta hiyo ilikuwa na jumla ya mtaji unaofikia shilingi bilioni 2,523.33 ikilinganishwa na shilingi bilioni 154.64 mwishoni mwa Desemba, 2000. Tathmini inaonesha kuwa benki nchini zina mitaji ya kutosha, ni salama na zinaweza kuhimili misukosuko ya kifedha. Kiwango cha mitaji kilifikia wastani wa asilimia 17.6 ikilinganishwa na kiwango cha chini cha asilimia 10 kinachotakiwa kisheria. Vilevile, takwimu zinaonesha kuwa mabenki mengi yametimiza masharti mapya ya kuongeza mtaji kutoka shilingi bilioni 5 hadi shilingi bilioni 15 hata kabla ya tarehe ya mwisho ambayo ni Februari 2015.


Sheria ya Fedha za Kigeni (The Foreign Exchange Act) Na. 1 ya mwaka 1992 imeipa mamlaka Benki Kuu kusimamia maduka ya kubadilisha fedha za kigeni. Mwishoni mwa mwaka 1992, Tanzania ilikuwa na maduka ya kubadilishia fedha za kigeni 84 ambayo yote yalikuwa Tanzania Bara. Maduka ya kubadilisha fedha za kigeni Zanzibar yalianza kufunguliwa Januari, 2002.

Hadi Desemba, 2013, maduka ya kubadilisha fedha yalikuwa yameongezeka na kufikia 233. Kati ya hayo maduka 206 yalikuwa Tanzania Bara na 27 Zanzibar.

### *Mwenendo wa Mfumuko wa Bei*

Kwa upande wa Tanzania Bara, mwenendo wa mfumuko wa bei umekuwa ukiathiriwa kwa kiasi kikubwa na kuyumba kwa bei za vyakula mbalimbali na fahirisi ya bei ya nishati na mafuta. Kwa miaka ya 1970 hadi 1972 kiwango cha mfumuko wa bei kilikuwa tarakimu moja kabla ya kuongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka ya 1973 hadi 1998. Kufuatia maboresho yaliyofanyika katika sekta ya fedha kiwango hicho kilishuka tena na kufikia wastani wa tarakimu moja mwaka 2013.

**Mchoro Na. 3:** Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Tanzania Bara Kuanzia Mwaka 1970-2013





**Chanzo:** *Benki Kuu ya Tanzania*

Mfumuko wa bei kwa upande wa Zanzibar umesababishwa zaidi na bei za mafuta na vyakula (mchele, sukari na ngano) katika soko la dunia kwani Zanzibar huagiza bidhaa hizo toka nje ya nchi. Mfumuko wa bei umekuwa chini ya asilimia kumi katika miaka mingi, ingawa ulipanda kwa kiwango cha juu zaidi mwaka 2008 kutokana na kupanda kwa bei za vyakula na mafuta

katika soko la dunia kufuatia msukosuko wa kifedha duniani. Katika mwaka 2013, mfumuko wa bei ulishuka sana na kufikia asilimia 4.6 kutokana na kushuka tena kwa bei za mchele, sukari, ngano pamoja na mafuta katika soko la dunia.

**Mchoro Na. 4:** Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Zanzibar Kuanzia Mwaka 2001-2013




**Chanzo:** *Benki Kuu ya Tanzania*

## Mikopo na Biashara ya Nje

### *Mikopo na Madeni*

Mwaka 1965, Serikali zote mbili zilikubaliana kujumuisha suala la mikopo nchini katika Orodha ya Mambo ya Muungano. Dhamana ya usimamizi na uratibu liliwekwa chini ya Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwaka 1966, Benki Kuu ya Tanzania ilianzishwa kwa lengo la kupunguza vizingiti vya ukopaji na Benki za Biashara kutaifishwa kusaidia ukopaji wa Serikali kutoka vyanzo vya ndani. Mwaka 1974, Serikali ilianza kutekeleza Sheria ya Mikopo, Madeni, Dhamana na Misaada *(the Government Loans, Guarantee and Grants Act, 1974).* Katika kutekeleza Sheria hiyo, Serikali ilikusudia kuwa mikopo mipya ya ndani au ya nje haisababishi gharama za ulipaji wa deni lolote la Serikali katika mwaka wa fedha husika na miaka minne inayofuata kuzidi asilimia 30 ya wastani wa mapato ya kila mwaka ya Serikali. Aidha, kwa ukopaji wa nje, Serikali ilihakikisha kuwa mikopo mipya inaidhinishwa endapo haisababishi gharama za ulipaji wa mikopo yote ya nje katika mwaka wa fedha husika na miaka minne inayofuata kuzidi asilimia

15 ya wastani wa mapato ya fedha ya kila mwaka. Pamoja na jitihada hizo, deni lilianza kukua kwa kasi katika kipindi cha miaka ya 1970-1980 kutokana na athari za ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia (1974-1979), gharama ya vita vya Kagera (1978-1979), kuyumba kwa bei ya mauzo nje, kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1977 kulikosababisha kuundwa kwa mashirika mapya ya umma yakiwemo reli, bandari na ndege.

Sheria ya 1974 ilifanyiwa marekebisho na kupitishwa mwaka 2004. Sheria hiyo, pamoja na mambo mengine, inamtaka Waziri wa Fedha kukopa baada ya kushauriwa na Kamati za Usimamizi wa Madeni. Sheria pia iliainisha mgawanyo wa majukumu ya kitaasisi katika usimamizi wa madeni ya Serikali na kubainisha na kuweka ukomo wa mikopo yenye unafuu isiwe chini ya asilimia 35. Vilevile, Sheria mpya zikiwemo za Huduma za Kibenki na Taasisi za Kifedha, Masoko na Mitaji, na Benki Kuu ziliidhinishwa ili kuleta ufanisi katika ukopaji wa ndani.

Sanjari na jitihada hizo, Mkakati wa Taifa wa Kusimamia Madeni uliandaliwa ukielekeza vyanzo nafuu ambavyo Serikali inaweza kukopa. Serikali pia iliandaa Mkakati wa Kusimamia Deni la Taifa kwa Muda wa Kati mwaka 2010/11 ambao umeainisha na kukokotoa gharama na athari za kila aina ya mikopo ambayo Serikali inatarajia kukopa na hivyo kushauri aina bora ya mikopo ili Deni la Taifa liendelee kuhimilika. Serikali hufanya Tathmini ya Ustahimilivu wa Deni la Taifa *(National Debt Sustainability Analysis)* kila baada ya miaka miwili. Tathmini iliyofanyika hivi karibuni inaonesha kwamba kwa sasa Deni la Taifa linahimilika. Kwa upande wa udhibiti wa madeni ya ndani, Serikali zote zinaruhusiwa kukopa kwa uhuru kwa kuzingatia pia Sheria ya Mikopo, Madeni, Dhamana na Misaada.

Jedwali 1: Uhimilivu wa Deni la Nje kwa Mwaka 2012

| Kiashiria | Matokeo (Asilimia) | Ukomo |
|---|---|---|
| Deni la Taifa kwa sasa/Pato la Taifa | 18.9 | **50** |
| Deni la Taifa kwa sasa/mauzo ya bidhaa nje | 56.2 | **200** |
| Deni la Taifa kwa sasa/mapato ya ndani | 111.3 | **300** |
| Malipo ya madeni nje/ mauzo ya bidhaa nje | 2.5 | **25** |
| Malipo ya madeni nje/ mapato ya ndani | 5 | **35** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha*

### *Biashara ya Nje*

Biashara ya nje ni suala lililoingizwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano mwaka 1964. Kabla ya Muungano, shughuli za biashara ya nje zilikuwa zikiendeshwa na taasisi maalum kwa pande zote mbili. Kwa upande wa Zanzibar, uagizaji wa bidhaa kutoka nje ulisimamiwa na Shirika la Biashara za Nje (BIZANJE). BIZANJE pia ilikuwa ikihusika na uuzaji wa mazao na bidhaa za Zanzibar nje ya nchi kwa kushirikiana na Shirika ya Taifa la Biashara Zanzibar (Zanzibar State Trading Corporation – ZSTC) ambalo lilihusika zaidi na usambazaji wa bidhaa zilizoagizwa nje na zile zilizozalishwa ndani ya nchi na kuzisambaza kwa walaji. ZSTC lilihusika na linaendelea kuhusika na kutafuta masoko ya karafuu nje ya nchi. Kwa upande wa Tanzania Bara, *General Agricultural Products Export Company (GAPEX*) ilihusika na uuzaji nje wa mazao na pia kuagiza bidhaa kutoka nje. Aidha, Halmashauri ya Biashara ya Ndani (Board of Internal Trade – BIT) ya Tanzania Bara, ilikuwa na jukumu la kusimamia biashara ya ndani hususan uagizaji, ukusanyaji na usambazaji wa bidhaa.

Halmashauri ya Biashara ya Nje (Board of External Trade – BET) iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bodi ya Biashara ya Nje (Board of External Trade Act) Na. 5 ya mwaka 1978 kwa upande mwingine ilihusika na uratibu, kusimamia ukuzaji wa biashara ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nje ya nchi na kuhamasisha biashara ya nje kupitia maandalizi na ushiriki katika maonesho ya kimataifa ndani na nje ya nchi.

Halmashauri ya Biashara ya Nje ilifutwa chini ya Sheria Na. 4 ya mwaka 2009 na kuanzishwa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*The Tanzania Trade Development Authority - TANTRADE*). Mamlaka hiyo ilianzishwa baada ya kufutwa kwa Halmashauri ya Biashara ya Ndani (BIT) na Halmashauri ya Biashara ya Nje (BET). Uanzishwaji wa TANTRADE mwaka 2009 ulilenga kuimarisha usimamizi wa biashara ya ndani na kuhamasisha biashara ya nje kupitia maonesho ya kibiashara ndani na nje ya nchi; uzalishaji kwa kuzingatia wingi na ubora wa bidhaa na huduma; usindikaji kwa kuongeza thamani kwenye mnyororo wa thamani; kufanya tafiti za masoko na bidhaa kwa maendeleo ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa; kuwajengea wajasiriamali uwezo ili watambue fursa zinazowazunguka na zilizoko kwenye masoko ya kanda na nchi nyingine. Katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka imeandaa na kusimamia ushiriki wa Tanzania katika maonesho ya

biashara ya nchi mbalimbali zikiwemo Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia, Malawi na Msumbiji. Nchi nyingine ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Afrika Kusini, Botswana, China, India, Dubai, Abu Dhabi, Misri, Uingereza, Ujerumani na Hong Kong.


Aidha, Serikali imesimamia ushiriki wa Tanzania katika maonesho makubwa na ya muda mrefu (EXPO) yakiwemo EXPO 70 Japan, 1998 *Lisbon World Exposition,* Expo 99 Kunming China, *Expo 2000 Hannover Ujerumani,* Aichi Japan 2005, Expo 2008 Zaragoza Spain, *Expo 2010* Shanghai *China na Expo Korea 2012 Yeosu.* Vilevile, imeandaa maonesho madogo katika Nchi ya Ugenini (Solo Exhibition) katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Comoro pamoja na kushauri misafara ya wafanyabiashara inayotembelea nchi mbalimbali. Serikali pia imebadili yaliyokuwa Maonesho ya Kilimo (National Agricultural Trade Fair) na kuwa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Dar es Salaam International Trade Fair - DITF). DITF ya sasa imekua kutoka Maonesho ya Kilimo ya Taifa, yaliyokuwa na washiriki wa ndani na kuanza kushirikisha makampuni ya nje. Mwaka 1996, DITF ilijiunga kuwa mwanachama wa Waandaaji wa Maonesho Duniani na kufanya maonesho hayo pamoja na miundombinu yake ya Uwanja wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kutambulika kuwa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. Juhudi za kuanzisha viwanja vingine vya maonesho Zanzibar na sehemu nyingine zinafanyika.

Katika kuimarisha Muungano hususan katika masuala ya biashara ya nje na ndani, Serikali imeanzisha Ofisi ya TANTRADE Zanzibar ili kuhudumia wananchi kwa karibu. Hatua hiyo ni muhimu katika kuunganisha nguvu ya kuitangaza Tanzania na fursa zake za uwekezaji, utalii na biashara kwa ujumla zinazofanywa katika Vituo vya Biashara vilivyoanzishwa London na Dubai.

Kutokana na juhudi za kutangaza bidhaa za Tanzania nje ya nchi pamoja na kuwajengea uwezo wajasiriamali, mauzo ya Tanzania nje ya nchi yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Mauzo ya nje yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 170 mwaka 1963 hadi Dola za Marekani milioni 248.45 mwaka 1985. Hata hivyo, kuanzia mwaka 1986 kiwango cha ukuaji wa mauzo nje ya nchi kilikuwa kidogo hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990. Hali hii ilisababishwa na uzalishaji mdogo na kushuka kwa bei ya mazao ghafi

katika Soko la Dunia. Katikati ya miaka ya 1990, mauzo yalianza kuongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 679.2 na kufikia takribani Dola za Marekani milioni 5,912 mwaka 2012.

**Mchoro Na. 5:** Mwenendo wa Thamani ya Mauzo Nje Kuanzia Mwaka 1963-2012




**Chanzo:** *Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania*

Aidha, biashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar imeimarika na wananchi wa pande zote mbili wameweza kutumia fursa zilizopo bila ya vikwazo. Katika kuimarisha zaidi ushirikiano wa kibiashara, masuala ambayo yalikuwa kinzani katika kufanya biashara kwa tija kama vile upatikanaji wa leseni ya biashara, upatikanaji wa ardhi na hatimiliki ya ardhi kuwezesha upatikanaji wa mikopo yamekuwa yakitatuliwa hatua kwa hatua.

### *Mafuta na Gesi asilia*

Utafutaji wa mafuta na gesi nchini ulianza mwanzoni mwa miaka ya 1950. Kabla ya mwaka 1964, utafutaji wa mafuta na gesi katika mwambao wa bahari ulikuwa unafanywa na kampuni za SHELL na BP ambazo kwa pamoja ziliruhusiwa kufanya utafiti huo mwambao wa Tanganyika pamoja na visiwa vilivyo karibu na mwambao huo. Mwaka 1957, kampuni hizo zilichimba kisima cha Zanzibar - 1 chenye kina cha mita 4,353 na kugundua uwepo wa gesi asilia. Mwaka 1962 kisima cha Pemba -5 chenye kina cha mita 3,886

kilichimbwa na kugunduliwa kuwepo kwa mafuta katika tabaka la *Oligocene* na gesi katika tabaka la *Middle Eocene.* Pamoja na kuwepo kwa viashiria chanya vya haidrokaboni vilivyothibitisha kuwepo kwa miamba ya vyanzo vya mafuta na gesi, Kampuni za SHELL na BP zilisitisha shughuli zao na kwenda *Niger Delta* ambako SHELL na kampuni nyingine zaligundua mafuta kabla. Hivyo utafutaji wa mafuta na gesi ulisitishwa kwa miaka 7 mfululizo na uliendelea tena mwaka 1969 baada ya kuundwa kwa Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (Tanzania Petroleum Development Corporation - TPDC) kwa Sheria ya Makampuni Na.17 ya mwaka 1969 na kupewa jukumu la kuratibu shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi Tanzania nzima.

Mwaka 1964, maeneo yote yaliyokuwa chini ya SHELL yaligawiwa Kampuni za AGIP/AMOCO na kanuni za kugawana mapato ya uzalishaji *(Production Sharing Agreement - PSA)* zilitengenezwa. Hivyo, AGIP/AMOCO waliamua kuachia maeneo yote ambayo yalikuwa hayazalishi kwa faida kulingana na makubaliano yao. Mwaka 1982, AGIP iliachia maeneo pamoja na nyaraka zote na kuipatia TPDC. Kampuni nyingine zilizohusika kutafuta mafuta Tanzania ni IEDC na TEXACO.

Ugunduzi wa kwanza wa miamba yenye gesi/mafuta ulikuwa mwaka 1974 katika Kisiwa cha Songo Songo mkoani Lindi. Ugunduzi ulibaini kuwa kulikuwa na akiba ya gesi ya 1TCF. Ugunduzi wa pili ulifanyika katika eneo la Mnazi Bay katika Mkoa wa Mtwara mwaka 1982 na ulibaini kuwa na akiba ya gesi ya kiasi cha 4TCF. Uchimbaji wa gesi ya Songosongo ulianza mwaka 2004 na Mnazi Bay mwaka 2006. Ugunduzi mwingine umefanyika Mkuranga (2007), Kilwa Kaskazini (2008) na Ntoria -1 (2012). Kwa sasa maeneo hayo yako katika hatua za upembuzi ili kutambua kiasi cha akiba ya gesi kilichopo.

Kuanzia mwaka 2010 hadi 2013, utafutaji wa gesi uliendelea katika eneo la Bahari Kuu. Utafiti huo umebaini kuwa kiasi kikubwa cha gesi asilia kiko katika Kitalu Na.1 ambacho kinajumuisha maeneo ya Chaza, Jodari, Mzia na Mkizi; Kitalu Na.2 ambacho kinajumuisha maeneo ya Zafarani, Lavan, Tangawizi, Mlonge – 1 na Bizari – 1; Kitalu Na.3 ambacho ni Papa -1; na Kitalu Na.4 ambacho ni Pweza, Chewa na Ngisi. Kampuni zinazofanya tafiti katika maeneo hayo ni BG/OPhir ambazo ziko katika Kitalu 1, 3 na 4 na kampuni za Statoil/Exon Mobil ambazo ziko Kitalu 2. Hadi kufikia Desemba

2013, utafiti ulikuwa umegundua kuwa katika vitalu hivyo kuna kiasi cha gesi chenye futi za ujazo trilioni 46 (46TCF).

Kutokana na kuongezeka kwa utafiti wa gesi na ugunduzi wa gesi katika bahari kuu mwaka 2010, Serikali imeandaa Sera ya Gesi ili kutoa mwongozo katika maendeleo na ukuaji wa sekta hii na kuhakikisha kunakuwa na maslahi ya kutosha kwa Taifa na wananchi wote. Maandalizi ya Sera hiyo yalikuwa shirikishi na kuhusisha kampuni za utafutaji wa gesi, vikundi vya kiraia, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine. Sera ya Taifa ya Gesi Asilia ilipitishwa rasmi Oktoba, 2013. Hivi sasa Serikali inaandaa Sheria ya Gesi Asilia.

Katika kuhakikisha gesi asilia inatumika kuleta maendeleo ya nchi ikiwa ni pamoja na kuzalisha umeme, Serikali inajenga bomba la gesi kutoka Mtwara na Songo Songo kupitia Somanga Fungu hadi Dar es Salaam. Serikali inajenga mtambo wa kuchakata gesi katika eneo la Madimba (Mtwara). Hadi Machi, 2014 uunganishaji wa bomba la gesi kwa urefu wa kilomita 212 ulikuwa umekamilika na tayari kiasi cha kilomita 49 za bomba zilikuwa zimelazwa ardhini. Vilevile, ulazaji wa bomba katika Bahari ya Hindi kutoka kwenye Kisima hadi Songo Songo umeanza kufanyika. Pia, uchimbaji wa mtaro wenye urefu wa kilomita 60 kwa ajili ya kulaza bomba umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kujenga mtambo wa kupokea gesi hiyo katika eneo la Kinyerezi, Dar es Salaam utakaotumika kuzalisha umeme.

Kwa upande wa Zanzibar, baada ya tafiti zilizofanyika na kupatikana viashiria chanya vya haidrokaboni vilivyothibitisha kuwepo hifadhi na miamba ya vyanzo vya mafuta, SMZ imechukua hatua mbalimbali za kuendeleza tafiti hizo na kuhakikisha nishati hiyo itanufaisha wananchi kwa jumla. Mwaka 1990, SMZ ilitoa kibali cha utafutaji mafuta kwa kampuni ya *Antrim Resources International* ya Kanada ambapo mwaka 1997 walitia saini Mkataba wa miaka kumi na moja (11) na SMT kwa ajili ya utafutaji wa mafuta Zanzibar. Hata hivyo, mkataba huo haukutekelezeka kutokana na kukosekana kwa makubaliano ya mgao wa mapato ya mafuta kwa pande mbili za Jamhuri.

### 2.3.5 Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu

Uvuvi wa Bahari Kuu ulikuwa ukisimamiwa na Idara ya Uvuvi ya SMT na ya SMZ katika ukanda wa kiuchumi wa Tanzania hadi mwaka 1998 ilipoonekana

umuhimu wa suala hili kuratibiwa kimuungano. Hali hiyo ilisababisha kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kwa mujibu wa Sheria Na.1 ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 1998 iliyorekebishwa kwa Sheria Na.4 ya mwaka 2007 na kuiwezesha Mamlaka kuanza kazi zake rasmi mwaka 2010 na makao makuu yake yakiwa Zanzibar.

Mamlaka hiyo ina majukumu ya kutoa leseni za uvuvi katika Bahari Kuu, kudhibiti viwango vya uvuvi, kusimamia rasilimali ya uvuvi na hifadhi ya mazingira ya bahari, na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi Bahari Kuu. Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake, inashirikiana na Idara za Uvuvi za SMT na SMZ pamoja na Jeshi la Polisi (Wanamaji), Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), *Zanzibar Maritime Authority* (ZMA), *Surface and Marine Transport Regulatory Authority* (SUMATRA), *Institute of Marine Sciences* (IMS) na *Tanzania Fisheries Research Institute* (TAFIRI). Vilevile, Mamlaka inashirikiana na mashirika ya kikanda kama vile *Indian Ocean Tuna Commission* (IOTC), *Indian Ocean Commmission* (IOC), *South West Indian Ocean Fisheries Commission* (SWIOFC) na SADC katika kudhibiti uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira ya bahari. Mamlaka hiyo kwa kutoa leseni za uvuvi wa Bahari Kuu imechangia katika Pato la Taifa kwa kukusanya Dola za Marekani 4,720,167 katika kipindi cha 2009 hadi 2013.

**Jedwali 2:** Mchango wa Uvuvi wa Bahari Kuu katika Pato la Taifa kwa Mwaka 2009/10-2012/13

| Mwaka | Idadi ya vyombo vilivyopewa leseni | Thamani katika Dola za Marekani |
|---|---|---|
| 2009/2010 | 23 | 702,000 |
| 2010/2011 | 49 | 1,406,180 |
| 2011/2012 | 39 | 1,276,177 |
| 2012/2013 | 38 | 1,335,810 |
| **JUMLA** | **149** | **4,720,167** |

***Chanzo:*** *Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu*

### 2.3.6 Usafiri wa Anga

Baada ya kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, shughuli za usafirishaji wa anga ziliwekwa chini ya Kurugenzi ya Usafiri wa Anga ya Afrika Mashariki kwa kufanya shughuli za kiufundi katika masuala ya usafiri wa anga. Hata hivyo, shughuli za utoaji wa huduma za matengenezo, uangalizi

wa viwanja na zimamoto zilikuwa chini ya Serikali za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, masuala ya usafiri wa anga yalifanywa kuwa ya Muungano na hivyo kuanzishwa Kurugenzi ya Usafiri wa Anga *(Directorate of Civil Aviation - DCA)* kwa Sheria ya Usafiri wa Anga ya mwaka 1977. Vilevile, Shirika la Ndege la Tanzania *(Air Tanzania Corporation - ATC)* lilianzishwa mwaka 1977 ili kutoa huduma ya usafiri wa anga badala ya Shirika la Ndege la Afrika Mashariki ambalo shughuli zake zilikoma baada ya kuvunjika kwa Jumuiya hiyo.

Mwaka 1999, Kurugenzi ya Usafiri wa Anga ilifutwa na Wakala wa Serikali wa Masuala ya Usafiri wa Anga *(Civil Aviation Agency)* ilianzishwa mwaka 2003. Aidha, mwaka 2003 Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(Tanzania Civil Aviation Authority - TCAA)* ilianzishwa kwa Sheria ya Usafiri wa Anga Na.10 ya mwaka 2003 kama ilivyorekebishwa mwaka 2006, ili kutoa huduma za anga, huduma za uongozaji ndege, huduma za viwanja vya ndege, usalama wa anga, huduma za uendeshaji ndege, kuendeleza miundombinu ya anga, usajili wa ndege, uchunguzi wa ajali ya ndege na huduma za uokoaji.

Serikali kupitia Mamlaka hiyo imeanzisha Chuo cha Usafiri wa Anga kinachotoa mafunzo ya uongozaji wa ndege, taarifa za usafiri wa anga na masuala ya usalama katika usafiri wa anga. Hadi kufikia mwaka 2012, Chuo cha Usafiri wa Anga kimetoa mafunzo ya kuongoza ndege, usalama, taarifa za usafiri wa anga na kozi mbalimbali zinazohusu usafiri wa anga kwa wanafunzi 3,865 kutoka Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi, Namibia, Botswana, Zambia, Nigeria na Liberia. Vilevile, ajali na matukio hatarishi yamepungua kwa kiasi kikubwa kama ilivyobainishwa kwenye Jedwali Na.2. Idadi ya abiria wanaotumia usafiri wa anga kuingia nchini na kuondoka imeongezeka kutoka abiria 2,172,519 mwaka 2005 hadi kufikia abiria 4,056,925 mwaka 2012.

**Jedwali 3:** Mwenendo wa Ajali na Matukio katika Usafiri wa Anga kwa Mwaka 2004-2012

| Ajali katika safari 1,000,000 | | | | Matukio katika safari 1,000,000 | | | Idadi ya Abiria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Ajali** | **Safari** | **Kipimo cha Ajali** | **Matukio** | **Safari** | **Kipimo cha Matukio** | |
| 2004 | 3 | 149,161 | 2.0 | 16 | 149,161 | 10.7 | |
| 2005 | 2 | 155,052 | 1.3 | 16 | 155,052 | 9.0 | 2,172,519 |
| 2006 | 4 | 160,766 | 2.5 | 10 | 160,766 | 6.2 | 2,470,127 |
| 2007 | 3 | 179,455 | 1.7 | 8 | 179,455 | 4.5 | 2,780,989 |
| 2008 | 4 | 181,434 | 2.2 | 11 | 181,434 | 6.1 | 2,910,533 |
| 2009 | 0 | 167,610 | 0.0 | 13 | 167,610 | 7.8 | 2,754,355 |
| 2010 | 5 | 181,240 | 2.8 | 8 | 181,240 | 4.4 | 3,027,512 |
| 2011 | 2 | 206,334 | 1.0 | 10 | 206,334 | 4.9 | 3,605,532 |
| 2012 | 2 | 222 430 | 0.9 | 14 | 222, 430 | 6.3 | 4,056, 925 |

**Chanzo:** *Mamlaka ya Usafiri wa Anga*

Mamlaka imeendelea kutoa huduma zake kwa watoa huduma za usafiri wa anga kwa kushirikiana na Mamlaka za Viwanja vya Ndege.

### 2.3.7 Takwimu

Kabla ya uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar, huduma za ukusanyaji, uchambuzi, usambazaji na uhifadhi wa takwimu zilikuwa zikitolewa tofauti kwa kila upande. Mara baada ya uhuru wa Tanganyika mwaka 1961, Idara ya Takwimu ilianzishwa chini ya Sheria ya Takwimu Sura 443 ikiwa na jukumu la kufanya sensa ya watu; kukusanya, kuhifadhi, kuchambua na kuchapisha takwimu zinazohusiana na uchumi, jamii na utamaduni; na kuratibu mfumo wa takwimu za kiuchumi na kijamii.


Mwaka 1967, mara baada ya kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki masuala ya takwimu kwa Tanganyika na Zanzibar, yalikuwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, na mwaka huo huo Sensa ya kwanza ya watu na makazi ilifanyika. Matokeo ya Sensa hiyo yalionesha kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa na watu 12,313,469 ambapo kati ya hao Tanzania Bara ilikuwa na watu 11,958,654 na Zanzibar ilikuwa na watu 354,815. Mara

baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 miongoni mwa mambo yaliyokuwa yakishughulikiwa katika ngazi ya Jumuiya ikiwemo takwimu yaliingizwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano.

Katika kuboresha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu nchini, Serikali ilianzisha Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuwa Wakala wa Serikali, na mwaka 2002 ilitunga Sheria mpya ya takwimu na kuipa majukumu ya kuendesha sensa ya watu na Makazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, Wakala una jukumu la kuratibu shughuli zote za kitakwimu nchini; kuwa kitovu cha utunzaji wa takwimu zote rasmi nchini; na kuwa kitovu cha rejea kwa mashirika ya kimataifa na kampuni za kigeni zinazohitaji taarifa za kitakwimu kuhusu Tanzania. Ofisi ya Taifa ya Takwimu inashirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kwenye masuala yote ya takwimu yanayohusu Zanzibar.

Tangu mwaka 1964, Serikali imefanya Sensa ya Watu na tafiti mbalimbali na kutoa viashiria vya kiuchumi na kijamii vilivyowezesha kuandaliwa mipango mbalimbali ya maendeleo ya Kitaifa. Katika kipindi cha Miaka 50 ya Muungano, Sensa ya Watu na Makazi zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012. Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Tanzania ina watu 44,928,923, ambapo kati yao watu 40,640,425 (sawa na asilimia 90.6) ni wenye umri wa mwaka sufuri (0) hadi hamsini (50) waliozaliwa baada ya Muungano. Kwa upande wa Tanzania Bara, takwimu zinaonesha kuwa kuna idadi ya watu 43,625,354, kati ya hao watu 39,456,065 (sawa na asilimia 90.5) wamezaliwa baada ya Muungano na kwa Zanzibar kati ya watu 1,303,569, watu 1,184,360 (sawa na asilimia 90.9) wamezaliwa baada ya Muungano.

**Mchoro Na. 6:** Mwenendo wa Ongezeko la Idadi ya Watu Tanzania Kuanzia Mwaka 1965-2012




**Chanzo:** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu.*

### 2.3.8 Elimu ya Juu

Elimu ya Juu ilikuwa ni mojawapo ya maeneo yaliyopewa kipaumbele baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kabla ya hapo Zanzibar haikuwa na Chuo Kikuu hata kimoja wakati Tanganyika ilikuwa na Chuo Kikuu kimoja tu ambacho ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilichoanzishwa tarehe 25 Oktoba, 1961 kikiwa Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha London, Uingereza. Hali hiyo ilisababisha wananchi wa pande mbili kutafuta fursa za masomo nje ya nchi, hususan Makerere – Uganda, Royal Technical College Nairobi – Kenya, na wachache katika nchi za Ulaya, India na Afrika Kusini. Mwaka 1963 Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam kilijiunga na Vyuo Vikuu Vishiriki vya Makerere na Nairobi na kuunda Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki. Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwa na wataalam wazalendo wa fani mbalimbali na kujenga uwezo wa ndani kielimu, iliamua kuingiza suala la Elimu ya Juu katika orodha ya mambo ya Muungano mwaka 1967. Ilipofika tarehe 1 Julai, 1970 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipandishwa hadhi kuwa Chuo Kikuu kamili na kuanza na wanachuo 1,283 baada ya kuvunjwa kwa Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki mwaka 1970. Aidha, katika miaka ya 1970 na 1980 vyuo vya elimu ya juu viliongezeka ambapo, Chuo cha Maendeleo ya Uongozi (IDM) Mzumbe kilianzishwa mwaka 1972, na kilipandishwa hadhi kuwa Chuo Kikuu Mzumbe mwaka 2001. Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kilianzishwa mwaka 1984

na Chuo Kikuu cha Dodoma mwaka 2006. Kwa upande wa Zanzibar Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kilianzishwa tarehe 26 Septemba, 2001.



*Jengo la Utawala la Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA)*




*Jengo la Utawala la Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)*

Hadi kufikia mwaka 2014, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweza kuwa na jumla ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki 50, kati ya hivyo 15 ni vya Serikali na 35 ni vya binafsi. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya Vyuo Vikuu, idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo hivyo imeongezeka, kutoka wanafunzi 14 mwaka 1961 hadi kufikia wanafunzi zaidi ya 200,000 mwaka 2013/14. Kupitia vyuo vya ndani Serikali imetoa wataalam wa fani nyingi zikiwemo za udaktari, uhandisi, uchumi, uanasheria na ualimu. Pamoja na fursa za elimu ya juu zinazopatikana katika Vyuo vya Elimu ya Juu nchini, Serikali inasimamia masuala ya ufadhili (*scholarships*) unaotolewa na nchi na mashirika mbalimbali kwa Watanzania kuongeza fursa za masomo.

**Jedwali 4:** Udahili wa Wanafunzi kwa Programu Mbalimbali Kuanzia Mwaka 2009/10 - 2013/14

| Kundi la Programu | Udahili 2009/2010 | | | Udahili 2010/2011 | | | Udahili 2011/2012 | | | Udahili 2012/2013 | | | Udahili 2013/2014 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KE | ME | JUMLA | KE | ME | JUMLA | KE | ME | JUMLA | KE | ME | JUMLA | KE | ME | JUMLA |
| Kilimo | 104 | 455 | 559 | 142 | 564 | 706 | 130 | 369 | 499 | 189 | 732 | 921 | 215 | 620 | 835 |
| Biashara na Utawala | 2104 | 3631 | 5735 | 3148 | 5549 | 8697 | 2818 | 4816 | 7634 | 3493 | 5046 | 8539 | 4544 | 5857 | 10401 |
| Elimu ya Sanaa | 6068 | 9311 | 15379 | 7441 | 11054 | 18495 | 6840 | 10456 | 17296 | 6444 | 11388 | 17832 | 6476 | 11939 | 18415 |
| Elimu ya Sayansi | 504 | 1745 | 2249 | 556 | 1827 | 2383 | 439 | 1426 | 1865 | 601 | 2110 | 2711 | 1161 | 3173 | 4334 |
| Sayansi za Uhandisi | 113 | 920 | 1033 | 114 | 1126 | 1240 | 170 | 1307 | 1477 | 391 | 2158 | 2549 | 558 | 2640 | 3198 |
| Sheria na Sayansi za Jamii | 4245 | 5708 | 9953 | 6279 | 8339 | 14618 | 3864 | 6068 | 9932 | 2301 | 3236 | 5537 | 2843 | 3399 | 6242 |
| Sayansi za Matibabu | 563 | 991 | 1554 | 794 | 1209 | 2003 | 701 | 1152 | 1853 | 737 | 1404 | 2141 | 1029 | 1670 | 2699 |
| Sayansi Asilia | 107 | 410 | 517 | 111 | 488 | 599 | 111 | 382 | 493 | 178 | 447 | 625 | 266 | 729 | 995 |
| Sayansi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano | 810 | 2690 | 3500 | 1239 | 3339 | 4578 | 1206 | 3343 | 4549 | 1054 | 2806 | 3860 | 1677 | 3554 | 5231 |
| **Jumla Kuu:** | **14618** | **25861** | **40479** | **19824** | **33495** | **53319** | **16279** | **29319** | **45598** | **15388** | **29327** | **44715** | **18769** | **33581** | **52350** |

***Chanzo:*** *Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania*

Mwaka 2005, Serikali ilianzisha Tume ya Vyuo Vikuu ili kudhibiti ubora wa elimu ya juu nchini kwa kusimamia ubora wa mazingira ya kufundishia, majengo, mitaala, walimu na taratibu za mitihani. Aidha, Tume hiyo inaratibu udahili wa wanafunzi katika Vyuo Vikuu na taasisi za elimu ya juu nchini na nje ya nchi na kutoa ithibati (accreditation) kwa shahada, stashahada na vyeti kutoka taasisi mbalimbali za elimu ya juu ulimwenguni. Tangu kuanzishwa kwake, udahili wa wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu kutoka pande zote za Muungano hufanyika kwa kuzingatia vigezo muhimu vinavyowawezesha kusoma vyuo wanavyopata nafasi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.3.9 Uchangiaji Gharama za Elimu ya Juu

Kwa kipindi kirefu, baada ya uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar, elimu kwa ngazi zote iligharamiwa na Serikali. Kufuatia mageuzi ya kiuchumi yaliyofanyika nchini katika miaka ya 1990 ambayo yalibadilisha mfumo wa uchumi wa nchi kutoka uchumi hodhi kuwa uchumi wa soko, Serikali ilianzisha utaratibu wa uchangiaji wa gharama za elimu ya juu kwa awamu tatu ili kupunguza gharama za uendeshaji za Serikali. Awamu ya Kwanza ilianza kutekelezwa kuanzia Julai, 1992 ambapo wanafunzi walianza kugharamia nauli, ada ya maombi, ada ya usajili, fedha ya tahadhari, ada ya serikali ya wanafunzi, matibabu, gharama za vitambulisho na ada ya mitihani. Awamu ya Pili ilitekelezwa kuanzia Julai, 1994 ambapo, pamoja na gharama zilizohamishiwa kwa wanafunzi na wazazi wao katika awamu ya kwanza, wanafunzi walianza kugharamia pia mahitaji ya chakula na malazi. Kwa kuwa gharama hizo zilionekana kuwa kubwa, Serikali ilianzisha utaratibu wa utoaji mikopo kwa wanafunzi kwa ajili ya gharama za chakula na malazi.

Kupitia utaratibu wa kuchangia gharama za elimu ya juu, wanafunzi wengi zaidi waliweza kujiunga na vyuo jambo ambalo liliongeza mzigo kwa Serikali wa kugharamia elimu. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Awamu ya Tatu, ya uchangiaji wa gharama za elimu ya juu ilianza ambapo wanafunzi wanachangia gharama za ada ya mafunzo, utafiti, mahitaji maalum ya vitivo na mafunzo kwa vitendo. Katika awamu hii, Serikali ilianzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 ambayo ilirekebishwa kwa Sheria Na. 9 ya mwaka 2007. Malengo ya kuanzishwa kwa Bodi hiyo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji waliodahiliwa katika masomo ya shahada au stashahada ya juu katika taasisi za elimu ya juu

zinazotambuliwa na Serikali nchini na nje ya nchi. Vilevile, imepewa jukumu la kukusanya mikopo inayotolewa kwa wahitimu walionufaika na mikopo husika kuanzia mwaka 1994 ili itumike kuwanufaisha waombaji wengine wanaohitaji. Katika kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu, Bodi hiyo inafanya kazi pande zote mbili za Muungano na imefungua Ofisi ya Kanda Zanzibar ambayo inatoa huduma kwa Wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu Zanzibar. Uchangiaji katika Elimu ya Juu ulitekelezwa kwa awamu tofauti.

Katika kipindi cha miaka 50 ya Muungano, Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuongeza fursa ya wananchi wa pande zote mbili za Muungano kupata elimu ya juu. Hadi kufikia Machi 2014, jumla ya wanafunzi 260,150 wamenufaika na mikopo kutoka Serikalini kwa ajili ya elimu ya juu. Upatikanaji wa mikopo ni moja ya sababu za ongezeko la Vyuo vya Elimu ya Juu kutoka 25 mwaka 2004/2005 hadi 63 mwaka 2013/2014. Mikopo yenye thamani ya Sh.1,843,483,926,686.58 imetolewa tangu mwaka wa masomo 1994/1995 hadi mwezi Desemba 2013, ambapo Sh.51,103,685,914 zilitolewa na iliyokuwa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na kiasi cha Sh.1,792,380,240,772.58 zimetolewa na Bodi kuanzia Julai, 2005.

### 2.3.10 Usimamizi wa Mitihani

Usimamizi wa mitihani ya elimu ya Sekondari unafanywa na Serikali kupitia Baraza la Taifa la Mitihani ambalo ni chombo cha Muungano. Baraza la Taifa la Mitihani lilianzishwa kwa Sheria Na. 21 ya mwaka 1973, kufuatia kujitoa kwa Zanzibar katika Bodi ya Mitihani ya Afrika Mashariki mwaka 1970 na Tanzania Bara mwaka 1971. Kufuatia uamuzi wa kujitoa katika Bodi hiyo, nchi hizi mbili ziliendelea kushirikiana katika masuala ya mitihani hadi mwaka 1977 ilipoamuliwa kuwa miongoni mwa mambo ya Muungano. Baraza la Mitihani la Taifa, limefanikiwa kuendesha mitihani ya kumaliza elimu ya msingi, kidato cha nne na kidato cha sita, walimu ngazi ya cheti, stashahada na mitihani ya maarifa kwa ufanisi na limeweza kutunuku vyeti kwa watahiniwa wote waliofaulu mitihani hiyo. Aidha, Baraza limefanikiwa kusimamia mfumo wa kusimamia mitihani na utoaji vyeti kwa kuimarisha miundombinu husika ikiwemo Kituo cha Kusahihisha Mitihani Mbezi - Dar es Salaam, na mfumo wa kompyuta (*optical mark reader*) unaotumia karatasi

maalum katika usahihishaji wa mitihani. Mfumo huo umepunguza idadi ya wasahihishaji mitihani kutoka 4,000 hadi 301 mwaka 2013 mfumo huo ulipoanza.

### 2.3.11 Utafiti

Kutokana na umuhimu wa kuendeleza ubunifu, sayansi na teknolojia na kuratibu shughuli za utafiti zinazofanywa na taasisi mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar, Serikali iliamua kuingiza masuala ya utafiti katika Orodha ya Mambo ya Muungano mwaka 1977. Kwa kuzingatia umuhimu wa tafiti katika kuweka mipango na mikakati ya nchi, Serikali ilianzisha Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(Commission of Science and Technology - COSTECH),* kwa mujibu wa Sheria Na.7 ya mwaka 1986. Tume hiyo ina ofisi zake Dar es Salaam na Zanzibar ambazo zinasimamia, kuendeleza na kuratibu tafiti za kisayansi kwa kukusanya, kutunza, na kusambaza taarifa za sayansi na teknolojia na kuwezesha maendeleo na uhaulishaji wa teknolojia.

Serikali pia imeanzisha taasisi nyingine za sayansi na teknolojia kwa lengo la kuendeleza wananchi katika fani za uhandisi na ufundi na hivyo kuchangia katika maendeleo ya Tanzania. Miongoni mwa taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Nelson Mandela, Arusha. Vilevile, idadi ya vituo na taasisi za utafiti za umma imefikia 79 kwa mchanganuo ufuatao: Kilimo (18); mifugo na uvuvi (10) viwanda na nishati (8); maliasili (10); afya (8); na vyuo vikuu (32). Kutokana na kuongezeka kwa taasisi hizo kumekuwa na ongezeko kubwa la watafiti nchini; kiasi kwamba kwa kila watu milioni moja kuna watafiti 674 na hivyo kuifanya Tanzania kuwa kati ya nchi saba za Afrika zenye watafiti wengi.

Serikali kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia, inashirikiana na takriban taasisi 68 zinazofanya tafiti katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, maliasili, afya, uchumi, elimu ya juu, sayansi ya jamii, nishati na viwanda. Aidha, Tume kupitia fedha za utafiti imefanikiwa kuwaendeleza watafiti zaidi ya 500 kitaaluma katika ngazi za shahada ya uzamili na uzamivu. Kupitia tafiti katika maeneo mbalimbali ya kipaumbele kwa sekta ya kilimo, Serikali imefanikiwa kugundua mambo kadhaa ikiwemo ugunduzi wa chanjo inayostahimili joto *(thermostable trivalente)* kwa ajili ya udhibiti wa magonjwa makubwa ya kupumua kwa kuku. Pia, tafiti zimeleta mafanikio katika kudhibiti inzi wanaoharibu matunda kwa kutumia njia ya kibaiolojia *(Oecophylla longinoda)*

na njia ya kemikali *(pheromone)* na hivyo kupunguza uharibifu wa matunda kwa asilimia 90 na kuongeza mapato ya wakulima. Maeneo mengine ni pamoja na utafiti katika miradi inayolenga kuendeleza kilimo cha viazi vitamu, mihogo na mwani. Miradi hiyo inalenga kupata mbegu bora na kuimarisha afya ya walaji. Aidha, zipo taasisi za kisekta na za kitaaluma ambazo zinafanya tafiti mbalimbali zenye manufaa kwa Taifa.



*Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi akiangalia aina ya udongo unaofanyiwa utafiti katika Maabara ya Utafiti wa Udongo ya Chuo cha Kilimo, Kizimbani, Unguja mwaka 2012.*

Eneo lingine la utafiti linalotekelezwa kimuungano, ni usimamizi na matumizi salama ya nguvu za atomiki na usalama wa mionzi nchini. Kutokana na maendeleo makubwa ya matumizi ya teknolojia duniani, Serikali ilianzisha Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kama chombo cha Muungano kwa Sheria Na.7 ya mwaka 2003. Lengo ni kusimamia, kudhibiti, kutafiti na kuendeleza matumizi yote salama ya vyanzo vya mionzi kwa manufaa ya jamii ya Watanzania.

Serikali kupitia Tume hiyo imesimamia vyema na kuendeleza matumizi salama ya nguvu za atomiki katika sekta za afya, kilimo, viwanda, madini na nishati (gesi asilia). Katika sekta ya afya, upimaji wa mionzi na utoaji wa vibali hufanyika kwa vyakula vyote vinavyoingia nchini pamoja na ukaguzi na




*Jengo la Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, Arusha*

### 2.3.12 Utabiri wa Hali ya Hewa

Huduma za utabiri wa hali ya hewa kabla ya Muungano zilifanywa chini ya *British East African High Commission* ambayo mwaka 1963 ilibadilishwa muundo na kuwa *East African Common Services Organisation (EACSO).* Taasisi hiyo ilibadilika na kuwa *East African Meteorological Department (EAMD)* mwaka 1964 na ilikuwa na jukumu la kuhudumia nchi za Afrika Mashariki ikijumuisha Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar katika masuala ya hali ya hewa. Baada ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 1977, huduma za utabiri wa hali ya hewa ziliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano. Huduma hizo ziliwekwa chini ya Idara Kuu ya Hali ya Hewa iliyoanzishwa kwa Sheria Na.6 ya mwaka 1978. Hata hivyo, mwaka 1999 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ilianzishwa.

Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imeweza kutoa kwa ufanisi huduma ya utabiri wa hali ya hewa na ushauri stahiki kwa wananchi kwa kila siku kwa kipindi chote. Ushauri huo umekuwa ukisaidia kutoa tahadhari juu ya mvua kubwa, upepo mkali na ukubwa wa mawimbi baharini na kwenye

maziwa kwa wanaotumia usafiri na shughuli nyingine za kila siku. Hadi Machi, 2014, Tanzania ina vituo vikuu 28 vya kupima hali ya hewa vinavyofanya kazi kwa saa 24, kati ya vituo hivyo, vituo 2 vipo Zanzibar. Vilevile vituo vya hali ya hewa na kilimo *(Agromet stations)* kumi na tano (15) vimeanzishwa ambapo viwili vipo Zanzibar katika eneo la Kizimbani - Unguja na kingine Matangatuani, Pemba vinavyojiendesha vyenyewe *(Automatic Weather Stations).* Kwa upande wa Tanzania Bara, kuna vituo kumi na moja (11) vya hali ya hewa vinavyojiendesha vyenyewe *(Automatic weather stations)* katika maeneo ya Moshi (Kisangesangeni, Maweni, Uparo, na Masila), Lindi, Nachingwea, Tunduru, Msata (Bagamoyo), Nzega (Tabora), Makete (Njombe), na Chanika.



*Rada ya Hali ya Hewa iliyowekwa katika Kituo cha Hali ya Hewa cha Bangulo, Dar es Salaam*

Vituo vya kwanza vya hali ya hewa kuanzishwa nchini vilikuwa Kazeh Hill huko Tabora mwaka 1929 na Chukwani, Zanzibar mwaka 1930.

Kutokana na juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali, idadi ya wataalamu wa masuala ya hali ya hewa imeongezeka ikilinganishwa na wataalamu 330 waliokuwepo mwaka 1964 wakati utabiri wa hali ya hewa ulikuwa unafanywa kwa pamoja katika nchi zote za Afrika ya Mashariki. Hadi Machi,

2014, Mamlaka ya Hali ya hewa ina wataalam 574 ambapo kati yao 435 ni wanasayansi na 90 ni watabiri ambao kati yao 19 ni wanawake.

Serikali ilianzisha Chuo cha Hali ya Hewa mwaka 1999 mkoani Kigoma ambacho kilianza kwa kutoa mafunzo ya kati ya utabiri, hadi mwaka 2002 kilipoanza kutoa mafunzo ya stashahada ya utabiri. Katika mwaka 2013, Chuo hicho kilianza kutoa mafunzo ya shahada ya kwanza ya sayansi ya hali ya hewa kwa wafanyakazi na wananchi wengine.

### 2.3.13 Huduma za Posta na Simu

Kabla ya Muungano, huduma za Posta kwa upande wa Tanganyika zilisimamiwa chini ya Sheria iliyoanzisha Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki. Taasisi hiyo ndiyo ilikuwa na mamlaka pekee ya kusimamia na kutoa huduma za posta katika nchi za Kenya, Uganda na Tanganyika. Kwa upande mwingine Zanzibar ilijiunga na Umoja wa Posta Duniani (*Universal Postal Union* - UPU) mwaka 1895 hatua ambayo ni ya kipekee katika historia ya Bara la Afrika. Pamoja na kuwa mwanachama wa UPU, Zanzibar haikuwa chini ya Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na hatimaye kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, huduma za posta za Zanzibar ziliunganishwa katika Jumuiya hiyo kupitia Serikali ya Muungano.

Baada ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, ofisi nyingi zilianzishwa na nyingine kupanuliwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa ofisi hizo zinakuwa Posta kamili zinazotoa huduma ikiwa ni pamoja na Wakala wa Benki ya Posta. Kutokana na mpango huo, Makao Makuu ya Posta (Post House) pamoja na Posta Kuu (General Postal Office - GPO) zilijengwa Dar es Salaam. Kwa upande wa Zanzibar, Posta Kuu ya Kijangwani na Posta za Chakechake, Wete, Mkoani na Mkokotoni zilijengwa. Shirika jipya la Posta na Simu (*Tanzania Posts and Telecommunication Corporation* - TPTC) liliundwa kwa Sheria Na. 15 mwaka 1977 kutokana na kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977. Mwaka 1993, Shirika la Posta na Simu Tanzania lilirekebishwa na kuunda taasisi tatu zilizojitegemea, yaani Kampuni ya Simu Tanzania (Tanzania Telecomunications Limited – TTCL), Shirika la Posta Tanzania (Tanzania Posts Corporation – TPC) na Tume ya Mawasiliano Tanzania (Tanzania Communication Commission – TCC). Mabadiliko hayo

yalilenga kuboresha huduma katika sekta ya mawasiliano ili sekta hiyo ichangie vyema zaidi katika maendeleo ya Taifa.

Sheria Na. 9 ya mwaka 1993, ililipa Shirika la Posta majukumu ya kuwa mhimili mkuu wa utoaji wa huduma za posta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuratibu na kusimamia mawasiliano yote ya posta nchini. Aidha, Shirika lilipewa jukumu la kuhakikisha kuwa huduma za msingi za mawasiliano ya posta hasa za barua na vifurushi zinawafikia watu wengi zaidi mijini na vijijini. Majukumu hayo yalihusisha pia kuweka mipango endelevu ya kuwezesha huduma za posta kuchangia maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii.

Mwaka 2001 Kampuni ya Simu Tanzania ilibinafsishwa ili kuboresha utendaji kazi na kuongeza ufanisi katika utoaji huduma bora hadi vijijini. Pamoja na changamoto ambazo Kampuni hii imeendelea kukabiliana nazo kwa kipindi hicho chote, Kampuni imekuwa na mafanikio na mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya mawasiliano. Kampuni ya Simu Tanzania, ndiyo kampuni kubwa hapa nchini inayotoa huduma za mawasiliano katika teknolojia ya simu za mezani na kwa simu zisizokuwa na waya; ina mtandao wa simu za nyaya ulioenea sehemu kubwa ya Tanzania na inatoa huduma kwa taasisi nyingi muhimu katika uchumi na maendeleo ya jamii ikiwemo Serikali, benki, vyuo na shule, na ofisi za balozi. Kampuni ya Simu Tanzania ndiyo inayosimamia ujenzi na uendeshaji wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa unaoendelea kujengwa.

Katika kipindi cha miaka 50 ya Muungano, Serikali imepanua na kuimarisha mtandao wa ofisi za kutoa huduma za Posta na Simu Tanzania Bara na Zanzibar hadi ngazi za Wilaya. Vilevile, Shirika la Posta Tanzania limeunganishwa katika mtandao wa kielekroniki wa kimataifa ambao unawezesha ufuatiliaji wa nyaraka na vipeto vinavyopitia EMS, Rejista, na Vifurushi vya Kimataifa vinavyopitia mtandao wa posta. Aidha, utekelezaji wa mfumo mpya wa anuani za Makazi na Postikodi umeanza kwa miji ya Dar es Salaam, Zanzibar, Arusha na Dodoma na unalenga kila mwananchi kuwa na anuani kamili inayotambulisha makazi yake na kutoa huduma mtambuka.

## 2.4 Mambo ya Muungano kwa Mujibu wa Sheria

Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inabainisha mambo 22 ya Muungano. Aidha, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limetunga Sheria mbalimbali ambazo zinatekelezwa katika pande mbili za Muungano. Miongoni mwa Sheria hizo ni pamoja na Sheria iliyoanzisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Udhibiti wa Fedha Haramu, Uvuvi katika Bahari Kuu na Tume ya Mawasiliano.

### 2.4.1 Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Serikali iliunda Tume ya Taifa ya Uchaguzi kama ilivyowekwa na Ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Tume hiyo ina majukumu ya kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura; kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais na Wabunge; kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa wabunge; kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa uchaguzi wa madiwani Tanzania Bara; na pia kuwatangaza wabunge na madiwani wa viti maalum vya wanawake baada ya matokeo ya uchaguzi kukamilika.

Katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, Tume ya Taifa ya Uchaguzi hushauriana na Tume ya Uchaguzi Zanzibar juu ya masuala muhimu ya kuendesha na kusimamia chaguzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi huendesha Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, na kwa upande wa Zanzibar pia huandikisha wapiga Kura wenye sifa ya kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge.

Tangu kuanzishwa kwake, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeendesha Chaguzi Kuu nne za Rais na Wabunge chini ya Mfumo wa Vyama vingi vya Siasa ambazo zilifanyika kwa mujibu wa Sheria. Chaguzi hizo zilifanyika katika mazingira huru ya amani na usalama na watu wenye sifa walipewa nafasi ya kuwachagua viongozi wao kwa mujibu wa mfumo husika. Matokeo ya chaguzi hizo ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4.

**Jedwali 5:** Matokeo ya Uchaguzi wa Rais Kuanzia Mwaka 1995 hadi 2010

| Na. | Mgombea | Chama | Idadi ya kura alizopata | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| | **Uchaguzi wa mwaka 1995** | | | |
| | Benjamin William Mkapa | CCM | 4,026,422 | 61.83 |
| | Augustino Lyatonga Mrema | NCCR MAGEUZI | 1,808,616 | 27.77 |
| | Prof. Ibrahim Haruna Lipumba | CUF | 418,973 | 6.43 |
| | John Momose Cheyo | UDP | 258,734 | 3.97 |
| | | **JUMLA** | **6,512,745** | **100** |
| **Uchaguzi wa mwaka 2000** | | | | |
| | Benjamin William Mkapa | CCM | 5,863,201 | 71.7 |
| | Prof. Ibrahim Haruna Lipumba | CUF | 1,329,077 | 16.3 |
| | Augustino Lyatonga Mrema | TLP | 637,115 | 7.8 |
| | John Momose Cheyo | UDP | 342,891 | 4.2 |
| | | **JUMLA** | **8,172,284** | **100** |
| | **Uchaguzi wa mwaka 2005** | | | |
| | Jakaya Mrisho Kikwete | CCM | 9,123,952 | 80.28 |
| | Prof. Ibrahim Lipumba | CUF | 1,327,125 | 11.68 |
| | Freeman Aikaeli Mbowe | CHADEMA | 668,756 | 5.88 |
| | Augustine Lyatonga Mrema | TLP | 84,901 | 0.75 |
| | Edmund Sengondo Mvungi | NCCR Mageuzi | 55,819 | 0.49 |
| | Mchungaji Christopher Mtikila | DP | 31,083 | 0.27 |
| | Dkt. Emmanuel John Makaidi | NLD | 21,574 | 0.19 |
| | Anna Claudia Senkoro | APPT Maendeleo | 18,783 | 0.17 |
| | Leonard Kanangwe Shayo | Demokrasia Makini | 17,070 | 0.15 |
| | Paul Henry Kyara | SAU | 16,414 | 0.14 |
| | | **JUMLA** | **11,365,477** | **100** |
| | **Uchaguzi wa Mwaka 2010** | | | |
| | Jakaya Mrisho Kikwete | CCM | 5,276,827 | 62.84 |
| | Dkt. Wilbroad Peter Slaa | CHADEMA | 2,271,941 | 27.05 |
| | Prof. Ibrahim Haruna Lipumba | CUF | 695,667 | 8.28 |
| | Peter Kuga Mziray | APPT Maendeleo | 96,993 | 1.15 |
| | Rungwe Hashim Spunda | NCCR Mageuzi | 26,388 | 0.31 |
| | Mgaywa Muttamwega | TLP | 17,482 | 0.21 |
| | Dovutwa Fahmi Nassoro | UPDP | 13,176 | 0.16 |
| | | **JUMLA** | **8,398,474** | **100** |

***Chanzo:*** *Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

Serikali iliamua kuanzisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kuwa na kumbukumbu sahihi za wapiga kura. Katika kuongeza ufanisi wa daftari hilo, Serikali ilianzisha Mfumo wa Uandikishaji wa Wapiga Kura kwa kutumia kompyuta (Computerized Voters Registration System) na kutumika kwa mara ya kwanza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

### 2.4.2 Udhibiti wa Fedha Haramu

Mwaka 2006, Serikali ya Muungano, iliunda Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu *(Financial Intelligence Unit – FIU)* kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu, Sura Na. 423. Kitengo kinafanya kazi zake Tanzania Bara na Zanzibar na kinasimamia utekelezaji wa Sheria hiyo na Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu na Mali Athirika ya Zanzibar Na. 10 ya mwaka 2009. Kitengo kinahusika kupokea taarifa za miamala inayoshukiwa (*suspicious transaction reports*) kuhusu fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya kigaidi, kuzichambua na kuwasilisha matokeo ya uchambuzi kwa vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa Sheria. Sheria zimeainisha watoa taarifa kuwa ni pamoja na Benki; Kampuni za Bima; Kampuni za masoko na mitaji; Kampuni za mawakili na wanasheria; na Kampuni za wakaguzi na wahasibu. Aidha, Kitengo kinatekeleza majukumu ya usimamiaji wa watoa taarifa kwa kushirikiana na wasimamizi wa sekta husika, kama vile Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima na Bodi ya Bahati Nasibu Tanzania. Kitengo pia kinaelimisha watoa taarifa na umma kuhusu masuala ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi na kutoa miongozo ya kutekeleza sheria za udhibiti wa mambo hayo.

Katika kutekeleza majukumu yake, Kitengo kimepokea na kuchambua taarifa za miamala inayoshukiwa kuhusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi kutoka taarifa tano wakati Kitengo kilipoanza kazi hadi taarifa 50 mwaka 2013. Kitengo pia kimetoa miongozo *(Guidelines)* saba kwa watoa taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu yao ya kudhibiti fedha haramu na ufadhili wa ugaidi kulingana na matakwa ya sheria. Kitengo kimepanua wigo wa ushirikiano na taasisi mbalimbali duniani zinazohusika na kudhibiti fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na inashirikiana na vitengo vya kudhibiti fedha haramu vya Uingereza na Afrika ya Kusini.

### 2.4.3 Mawasiliano Tanzania

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilianzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Sura 172. Mamlaka hiyo ilitokana na kuunganishwa kwa Tume ya Utangazaji Tanzania *(Tanzania Broadcasting Commission – TBC)* na Tume ya Mawasiliano *(Tanzania Communication Commission – TCC).* Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilirithi na kuendeleza kazi zote zilizokuwa zinafanywa na Tume hizo. Mwaka 2010, Serikali iliidhinisha Sheria ya *Electronic and Postal Communications Act (EPOCA)* inayoipa nguvu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kudhibiti sekta ya mawasiliano hususan huduma za posta, simu na utangazaji.

Sheria hiyo inaipa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kusimamia ushindani wa haki katika utoaji wa huduma, kulinda na kuwianisha masilahi ya watoa na watumia huduma za mawasiliano nchini. Vilevile, Mamlaka inatakiwa kuhakikisha kuwepo kwa huduma bora za mawasiliano na upatikanaji wake kwa gharama nafuu na kuhamasisha uelewa wa haki na wajibu kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano. Mamlaka pia ina majukumu ya kutoa au kufuta leseni za watoa huduma za mawasiliano; kuweka viwango na masharti ya kutekelezwa na watoa huduma za mawasiliano; na kusimamia ubora, gharama, ugawaji na upatikanaji wa huduma za mawasiliano.

Katika kudhibiti sekta ya mawasiliano nchini, hususan posta, simu na utangazaji kwa Tanzania Bara na Zanzibar, Mamlaka imesimamia ushindani, kuongeza na kuimarisha huduma katika sekta hiyo. Kampuni zinazotoa huduma za mitandao ya simu zimeongezeka kutoka Kampuni moja (1) miaka ya 1990 hadi kufikia 14 mwaka 2013, na laini za simu zilizounganishwa zimeongezeka kutoka 1,445,006 mwaka 2003 hadi 27,607,822 mwaka 2013. Vituo vya redio viliongezeka kutoka 26 mwaka 2003 hadi 85 mwaka 2013, na vituo vya televisheni kutoka 13 mwaka 2003 hadi 26 mwaka 2013. Aidha, kampuni za kutoa huduma za vifurushi vya posta ziliongezeka kutoka 16 mwaka 2003 hadi 47 mwaka 2013.

Vilevile, Serikali imejenga Mkongo wa Taifa (*National Information and Communication Technology Broadband Backbone* - NICTBB) wenye takriban urefu wa kilomita 7,560 ambao umeunganishwa na mitandao mikubwa ya mawasiliano ya kimataifa ya baharini *(Submarine Cables) ya SEACOM na*

Eastern Africa Submarine Cable System (EASSy). Aidha, watoa huduma za simu za hapa nchini TTCL, Vodacom, Tigo, Airtel na Zantel zimejiunganisha katika mkongo wa Taifa wa mawasiliano na hivyo kuimarisha huduma za mawasiliano. Unguja na Pemba zimeunganishwa na mkongo huo kupitia mkongo wa umeme unaopita chini ya bahari. Vilevile, mkongo huo umeunganishwa na nchi jirani za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Zambia na Malawi. Watumiaji wa huduma za Intaneti waliongezeka kutoka 3,563,737 mwaka 2008 hadi 9,312,272 mwaka 2013. Wastani wa gharama za kupiga simu ndani ya nchi zimepungua kutoka shilingi 250 kwa dakika mwaka 2005 hadi kufikia wastani wa chini ya shilingi 100 kwa dakika mwaka 2013. Gharama za kupiga simu nje ya nchi zimepungua kutoka wastani wa shilingi 1,000 kwa dakika mwaka 2005 hadi shilingi 500 kwa dakika mwaka 2013. Vilevile, Serikali imefunga mtambo wa kusimamia na kuhakiki mawasiliano ya simu za nje (Telecommunications Traffic Monitoring System) ambao unalenga kuongeza mapato ya nchi.

### 2.4.4 Huduma za Bandari

Uendeshaji wa bandari nchini unaongozwa na Sheria ya Bandari (The Ports Act) Na. 17 ya mwaka 2004, ambayo inatumika pande zote mbili za Muungano. Kabla ya Sheria hiyo kutungwa, Tanzania Bara na Zanzibar zilikuwa zikitumia Sheria tofauti ambazo ni Sheria ya Bandari (The Revolutionary Committee Decree) Na.1 ya mwaka 1977 iliyoanzisha Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) na Sheria ya Mamlaka ya Bandari (The Tanzania Harbours Authority Act) Na. 12 ya mwaka 1977, iliyoanzisha Mamlaka ya Bandari Tanzania. Uanzishwaji wa Mamlaka hiyo ulitokana na kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mamlaka hiyo ina majukumu ya kumiliki na kuendeleza bandari zote nchini na zilizo katika Maziwa Makuu, hususan kwa kuendeleza, kuendesha, kutangaza bandari, kushirikisha na kusimamia Sekta Binafsi katika uendeshaji wa shughuli za bandari. Pamoja na Sheria ya mwaka 2004, kutakiwa kutekelezwa pande zote mbili za Muungano, Zanzibar inaendesha shughuli za bandari kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Bandari (The Zanzibar Ports Corporation (Amendment) Act) Na. 11 ya mwaka 2007 iliyorekebishwa kwa Sheria Na. 5 ya mwaka 2013.

Pamoja na kuwa kila upande unatumia Sheria yake, pande hizo mbili zinashirikiana katika kubadilishana taarifa zinazohusiana na masuala ya usafiri majini kupitia *Control Tower ya Mamlaka* na kubadilishana uzoefu kati ya Bodi

ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Shirika la Bandari Zanzibar (*Zanzibar Ports Corporation* – ZPC) na Mamlaka ya Bandari Tanzania (Tanzania Ports Authority –TPA). Aidha, Mamlaka hizo hushirikiana kuweka viwango vya ubora wa vyombo vya majini kwa kushirikiana na *Zanzibar Maritime Authority* (ZMA) na *Surface and Marine Transport Regulatory Authority* (SUMATRA). Taasisi hizo hushirikiana kwa kuweka Kanuni na taratibu za ukaguzi, utoaji wa leseni za meli, manahodha na mabaharia, na ukataji tiketi katika bandari za pande zote za Muungano. Hali kadhalika, Mamlaka ya Bandari inaendesha Chuo cha Bandari kilichopo Tandika, Dar es Salaam, kinachopokea pia wanafunzi kutoka Zanzibar.




*Meli MSC DENISSE ikiteremsha makontena yenye bidhaa mbalimbali katika Bandari ya Malindi, Zanzibar*

## 2.5 Ushirikiano katika Mambo Yasiyo ya Muungano

Kihistoria, ushirikiano wa watu wa Tanganyika na Zanzibar ni mpana na wigo wake unahusisha pia utendaji wa pamoja kwa mambo ya Muungano na yale yasiyokuwa ya Muungano. Msingi mkuu wa ushirikiano huo ni kuwepo kwa uwezo uliojengeka wa kila upande wa kutoa huduma au kutekeleza majukumu hayo kwa kuzingatia uwezo na hali halisi ya mahitaji ya pande

mbili kwa lengo la kuimarisha Muungano.

Taasisi zisizo za Muungano zimekuwa zikishirikiana kwa kubadilishana uzoefu na ujuzi, kutoa huduma, na masuala ya utamaduni. Maeneo hayo ya ushirikiano yamesheheni mafanikio, mbinu za kisasa na uzoefu. Hii inathibitisha kwamba, kuna tija ya kuendelea kubadilishana uzoefu katika mbinu na masuala yanayotekelezwa na kila upande na yale ya Muungano ili kuleta matokeo makubwa zaidi. Ushirikiano umekuwa zaidi katika sekta za afya, elimu, ustawi wa jamii, kilimo, habari, utamaduni, michezo, utalii, nishati na miundombinu. Utekelezaji wenye mafanikio makubwa katika mambo yasiyo ya Muungano umekuwa ni chachu muhimu na yenye kuleta matokeo makubwa zaidi katika kutekeleza masuala ya jamii na mengineyo ya kila siku.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi wakiongoza kikao cha Kamati ya Pamoja cha SMZ na SMT kilichofanyika tarehe 14 Januari, 2013*

Aidha, kutokana na kuimarika kwa uwezo wa kila upande katika maeneo yasiyo ya Muungano, imebainika kuwa kuna fursa ya kupanua ushirikiano katika mambo mengi zaidi. Mtazamo huo ndio ulitoa msukumo mkubwa zaidi wa kuhitaji kuwa na utaratibu rasmi wa ushirikiano ili kuleta maafanikio makubwa na pia kuchochea maeneo ya ushirikiano na hivyo kuimarisha zaidi ushirikiano wa watu, matumizi shirikishi ya rasilimali za nchi na ubadilishanaji uzoefu na matokeo ya tafiti mbalimbali ili kuharakisha mafanikio ya pande zote mbili za Muungano.

### 2.5.1 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Tanzania Social Action Fund – TASAF) unatekeleza programu za kusaidia kuondoa umaskini kwa kulenga mahitaji halisi ya wananchi. Awamu ya kwanza ya TASAF ilitekelezwa mwaka 2000 hadi 2005 katika Wilaya 40 zikiwemo 30 za Tanzania Bara na 10 za Zanzibar. Awamu ya Pili ilitekelezwa katika Halmashauri zote za Wilaya, Miji na Manispaa Tanzania Bara na Zanzibar kuanzia mwaka 2005 hadi Juni 2013. Aidha, Awamu ya Tatu ya TASAF ilizinduliwa Agosti, 2012, na utekelezaji wake utakuwa wa kipindi cha miaka kumi (10) hadi mwaka 2022.

Katika Awamu ya Kwanza na ya Pili miradi ya jamii katika sekta za afya, elimu, maji, ustawi wa jamii, uvuvi, kilimo, barabara, misitu, madini, benki na masoko ililenga kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma za jamii kwa wananchi; kuinua kipato kwa makundi maalum; kufanya kazi na kupata kipato pamoja na uundaji wa vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza.

Katika awamu mbili zilizopita, TASAF imekamilisha miradi mbalimbali ikiwemo ya madarasa 5,538; ofisi za walimu 155; nyumba za walimu 155; maabara za shule za sekondari 157; maktaba 23; majengo ya utawala katika shule za sekondari 211; mabweni ya wanafunzi 174; vyoo vya wanafunzi 1,067; mifumo ya umeme wa nguvu za jua 611; zahanati na vituo vya afya 674; nyumba za watumishi wa zahanati 308 na visima 531.

Aidha, TASAF imetekeleza miradi ambayo imeongeza au imeimarisha mifumo ya maji 41; hifadhi ya mazingira (misitu) 29; masoko 17; vituo vya mabasi 3; miundombinu ya umwagiliaji maji 11; maghala ya kuhifadhia chakula 114; vioski vya maji ya matumizi ya nyumbani 2,689; matanki ya maji 822; mabwawa madogo madogo 185; miche ya miti 5,385,000; madaraja ya watembea kwa miguu 1,192 na kuwapatia wavuvi vifaa vya kuvulia.



*Injini za Boti za Uvuvi zilizotolewa na TASAF kwa Vikundi vya Ushirika vya Wavuvi Pemba*

Utekelezaji wa awamu ya tatu utafanyika katika wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar na itahusisha utambuzi na uandikishaji wa kaya masikini; malipo na utimizaji wa masharti ya elimu na afya kwa walengwa wa mpango; na mifumo ya taarifa za uendeshaji na masijala ya walengwa.

**Jedwali 6:** Muhtasari wa Miradi ya Jamii Iliyotekelezwa na TASAF katika Awamu ya Pili

| Eneo | Idadi ya Miradi | Gharama za Utekelezaji |
|---|---|---|
| Tanzania Bara | 11,483 | 264,363,362,089 |
| Zanzibar | 814 | 13,359,598,266 |
| **Jumla** | **12,297** | **277,722,960,355** |

***Chanzo:*** *TASAF Agosti, 2013.*

### 2.5.2 Ndege za Serikali

Wakala wa Ndege za Serikali ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala namba 30 ya mwaka 1997 kwa lengo la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Viongozi wengine wa Serikali na wageni wa kitaifa. Vilevile, Wakala inalo jukumu la kutunza, kuongeza na kuendesha ndege kwa kiwango cha kimataifa.

Mamlaka ya Ndege za Serikali imeweza kununua ndege moja kubwa aina ya HS 748 na mbili ndogo za kisasa aina ya *Beechcraft King Air* 100 na kuongeza ufanisi wa huduma kwa Serikali. Vilevile, mwaka 1978 Serikali iliongeza ndege moja kubwa aina ya *Jet Fokker* 28 iliyowezesha kutoa huduma kwenda popote barani Afrika na Ulaya. Ndege hiyo iliwahudumia Viongozi Wakuu wa Serikali za pande zote mbili.

Mwaka 1984, ndege mbili (2) aina ya *Beechcraft King Air* 100 ziliuzwa na Serikali ilinunua ndege nyingine mbili aina ya *Aero Turbo Commander* 690. Aidha, ili kuziba pengo la ndege zilizouzwa, mwaka 1992 Serikali ilinunua ndege aina ya Fokker 50 kuwa mbadala wa *HS 748. Fokker* 50 ina uwezo wa kubeba abiria 50 na ina sifa ya kutua viwanja hata vya udongo, hivyo kurahisisha huduma kwa viongozi wakuu wa nchi kufika eneo ambalo lina viwanja vya udongo. Hivyo, kwa miaka mingi tegemeo la Serikali la usafiri wa anga limekuwa ni ndege ya *Fokker* 28 na *Fokke*r 50. Hali kadhalika, mwaka 2004, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilinunua ndege mpya ya kisasa aina ya *Gulfstream G550* ambayo ina uwezo wa kuruka masafa marefu, na ni salama zaidi na ina gharama nafuu za uendeshaji. Vilevile, Wakala wa ndege za Serikali inamiliki ndege ndogo ya watu 7 aina ya *PA 31, Navajo* iliyoirithi kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA).

## 2.6 Mafanikio ya Muungano

Tanzania imepitia katika mabadiliko makubwa ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Mabadiliko hayo yameiwezesha nchi kuwa na msimamo thabiti katika masuala mbalimbali, hususan yale yanayoimarisha amani, utulivu, usalama na heshima; hali ambayo imewafanya wananchi kufanya shughuli za maendeleo popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mambo yote hayo yanadhihirisha kuwa Muungano huo ni nyenzo imara na muhimu katika kuimarisha udugu na umoja.




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein akielezea mafanikio ya Muungano wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar 1 Machi, 2014*

Kimsingi yapo mafanikio makubwa yanayosaidia kuimarisha, kudumisha amani ya muda mrefu na utulivu wa Tanzania ambao ni tunu muhimu na fahari ya nchi hii.

### 2.6.1 Mafanikio ya Kisiasa

***Katiba na Sheria***

Kuwepo kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria mbalimbali ni mojawapo ya mafanikio makubwa ya Muungano. Kutungwa kwa Katiba ya kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 kumeimarisha upatikanaji wa huduma bora za kisheria katika eneo la haki za binadamu, mikataba, uandishi wa Sheria na kuhakikisha uendeshaji wa mashauri ya jinai, madai na yale ya kikatiba yanamalizika kwa wakati.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tanzania inaongozwa kwa misingi ya mihimili mikuu mitatu ambayo ni Bunge, Serikali na Mahakama. Bunge lina wajibu wa kuwawakilisha wananchi na kutunga

Sheria; Serikali ina wajibu wa kusimamia na kutekeleza sera, sheria, kanuni na miongozo ya kuendesha shughuli muhimu za umma; na Mahakama wajibu wake ni kutoa maamuzi na haki za kisheria. Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita yametokea mabadiliko na marekebisho mbalimbali ya uendeshaji wa mihimili hiyo. Kwa kiwango kikubwa kila mhimili umekuwa unatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba pasipo kuingiliwa na mhimili mwingine.

Katika kipindi cha nusu karne, Tanzania imefanikiwa kuwa na Katiba ya kudumu ambayo, imethaminiwa na kulindwa na wananchi. Sheria zimetungwa na nyingine kufutwa au kurekebishwa ili kuheshimu, kukuza na kulinda haki za binadamu; kukidhi mahitaji na matakwa ya wananchi na kurahisisha utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali. Hatua hizo zimerahisisha na kuongeza usimamizi wa haki katika vyombo vya Sheria kutokana na kuongezeka kwa mahakama, majaji na mahakimu katika ngazi zote; kupungua kwa uhalifu na ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za ulinzi na usalama. Kuanzia mwaka 2011, nchi imekuwa kwenye mchakato wa kufanya mabadiliko ya Katiba baada kuonekana kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 iliyopo, ina upungufu ambao unaweza kurekebishwa kwa kuandaa Katiba Mpya ambayo itakidhi mahitaji ya Watanzania kwa wakati huu na wakati ujao.

***Demokrasia na Vyama vya Siasa***

Mageuzi makubwa ya kisiasa yameonekana na kuongeza wigo wa demokrasia nchini. Mafanikio makubwa ya kisiasa yaliyopatikana kutokana na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni kuungana kwa vyama vya siasa vya TANU na ASP na kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM) tarehe 5 Februari, 1977. Kuunganishwa kwa vyama hivyo kuliongeza ari ya umoja na ushirikiano baina ya watu wa Tanganyika na Zanzibar. Kitendo cha kuunganisha vyama hivyo kimekuwa ni msingi muhimu katika kujenga mfumo wa kuwa na vyama vya siasa vya kitaifa. Mfumo wa vyama vya siasa umepewa nguvu na Sheria ya Usajili wa Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 inayovitaka vyama hivyo kuwa na sura ya kitaifa. Mfumo wa vyama vingi vya siasa, umeimarisha demokrasia, uhuru wa kutoa maoni na uwazi katika uendeshaji wa shughuli za umma ikiwa ni pamoja na masuala ya Muungano. Vilevile mfumo huo umeongeza ushindani thabiti wa kisiasa hasa katika vyama vya siasa (CCM, CUF, CHADEMA, TLP, NCCR-MAGEUZI na UDP) na katika shughuli za Bunge. Wananchi wanapata uhuru wa kutosha kuendesha mambo ya kisiasa hali

inayodhihirisha kukua na kuimarika kwa demokrasia na utawala bora. Utulivu na amani inayoonekana baada ya chaguzi zote zilizofanyika katika kipindi cha miaka 50 ni ushahidi tosha wa kuimarika kwa demokrasia.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akiwa na Viongozi wa Vyama vya Siasa baada ya kufungua mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa tarehe 6 Februari, 2014*

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshuhudia awamu nne za Uongozi, na awamu saba Zanzibar. Awamu hizo zilitokana na ridhaa za wananchi kwa njia ya kupiga kura. Wananchi wa Tanzania wameheshimu matokeo ya kura yanayowapa nafasi za uongozi wa kisiasa. Makabidhiano ya madaraka baina ya awamu moja kwenda nyingine yamekuwa ya ridhaa na sherehe, kuashiria kukua kwa demokrasia. Katika awamu zote hizo, ushindi ulikuwa wa chama cha CCM.

***Utaifa na Umoja***

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umeunganisha watu wa nchi mbili na kuunda Taifa moja la Tanzania. Kutokana na historia ya uhusiano wa kidugu baina ya watu wa Tanganyika na Zanzibar uliokuwepo uliwezesha watu wa nchi hizo mbili kuimarisha zaidi uhusiano na udugu kwa kuwafanya kuwa Taifa moja. Watanzania kwa ujumla wanapenda kujivunia utaifa wao popote wanapokuwa. Lugha adhimu ya Taifa - Kiswahili inayozungumzwa na Watanzania wote nayo imechangia kwa kiasi kikubwa kuwaunganisha wananchi.

***Amani na Utulivu***
Katika kipindi cha miaka 50 ya Muungano, Tanzania imekuwa na amani na utulivu vilivyowezesha shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii kutekelezwa kwa ufanisi. Nchi nyingi ulimwenguni, zikiwemo nchi jirani, katika nyakati tofauti zimejikuta katika vita, machafuko au migogoro ya wenyewe kwa wenyewe au na nchi jirani zao. Madhara ya kukosekana kwa amani na utulivu katika nchi huwa ni makubwa na huathiri maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Tanzania imekuwa nchi ya mfano ulimwenguni katika kudumisha amani na utulivu na hivyo kuwa kivutio katika shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo uwekezaji.

***Diplomasia na Uhusiano wa Nchi na Nchi, Kikanda na wa Kimataifa***
Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kudumisha na kuimarisha ujirani mwema na kufungua ukurasa mpya wa ushirikiano ambao unadumu hadi leo. Muungano unazidi kuimarika na unatoa tumaini kuwa Afrika inaweza kuungana na kuwa nchi moja. Ujirani mwema umetoa fursa mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kati ya nchi yetu na majirani zetu. Ikiwa imepakana na nchi nane, na kwa kutambua umuhimu wa nchi jirani, mara baada ya Muungano, Tanzania iliendelea kuimarisha ujirani mwema kikamilifu kupitia jitihada mbalimbali. Hivi sasa, Tanzania ina balozi 34 nje ya nchi (zikiwemo nchi za jirani), Balozi ndogo tatu, Vituo viwili vya Biashara na Balozi za Heshima 17.

Aidha, Sera ya kutofungamana na upande wowote imeliwezesha Taifa kuwa na urafiki baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa, jambo ambalo limewezesha kujenga ushirikiano endelevu kati ya Tanzania na nchi nyingi duniani na hivyo kuleta ustawi wa Taifa. Vilevile, Tanzania imeendeleza mahusiano mazuri na nchi zinazoizunguka.

### *2.6.2 Mafanikio ya Kiuchumi*
Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, Tanzania imepitia katika vipindi mbalimbali vya maendeleo ya kiuchumi kutokana na mabadiliko ya kisera ya ndani na mageuzi ya kiuchumi duniani. Katika miaka ya 1960, uchumi wa nchi ulikua kwa wastani wa asilimia 4 hadi 5 kwa mwaka, na katika miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1980, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 4.5 kwa mwaka. Kuanzia mwaka 1986, kasi ya kukua kwa uchumi imekuwa ikiongezeka hadi kufikia asilimia 6.8 mwaka 2012. Katika kipindi cha miaka

50 pato la Mtanzania kwa mwaka limeongezeka kutoka chini ya wastani wa Dola za Marekani 50 hadi kufikia Dola 683 mwaka 2012.

Kuwepo kwa Muungano kumesaidia sana kuimarisha hali za wananchi na kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano. Hali hiyo imetokana na kuwepo kwa soko la pamoja lisilokuwa na vikwazo vya kiutawala na kiuendeshaji linalojumuisha ushirikiano na utengamano wa kiuchumi ambao unasisitiza kuwepo kwa mtiririko wa rasilimali na bidhaa, mitaji, watu, na huduma baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Watanzania wa pande zote wamekuwa na haki ya kuwekeza mitaji yao popote ndani ya Tanzania. Zipo fursa nyingi za kibiashara ambapo wafanyabiashara wadogo wamewekeza katika pande zote mbili za Muungano. Hali hiyo imechangia kuongeza ajira kwa Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

***Mazingira Mazuri ya Uwekezaji na Vivutio vya Utalii***

Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta binafsi katika maendeleo ya kiuchumi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuendeleza sekta binafsi ili iwe chachu ya ukuaji wa uchumi. Kutokana na juhudi mbalimbali za Serikali za kuwezesha sekta binafsi kukua, miradi mingi na mikubwa imetekelezwa na kunufaisha nchi kimapato na kuongeza ajira.

Muungano umeunganisha rasilimali na kupanua wigo wa ushirikiano ambao umeongeza uwezo wa kukuza zaidi uchumi. Wingi na ubora wa vivutio vya utalii umetoa fursa ya pekee kwa wawekezaji kuwekeza kwenye maeneo mbalimbali katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo kuongeza Pato la Taifa. Vivutio hivyo vikiwemo Mlima Kilimanjaro, mbuga za wanyama, mandhari na fukwe nzuri za Zanzibar, Mji Mkongwe, na viungo (spices) vya aina mbalimbali vinaipa Tanzania nafasi ya pekee ulimwenguni katika kukuza utalii. Ukaribu uliopo baina ya pande mbili za Muungano unaongeza fursa za kuendeleza Sekta ya Utalii. Katika kipindi cha miaka 50 ya Muungano, Sekta hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa na kutoa ajira kwa vijana wa pande zote mbili za Muungano.

***Mfumo wa Fedha na Benki Kuu***

Mafanikio makubwa yamepatikana tangu kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Tanzania ambayo inasimamia Sera za Fedha. Utekelezaji wa sera hizo,

pamoja na mambo mengine, umelenga kutunza thamani ya fedha na kudhibiti mfumuko wa bei ambao umepungua kutoka asilimia 30 katika miaka ya 1990 hadi chini ya asilimia 10 kwa mwaka 2012/13. Pato la Taifa linaongezeka kila mwaka sanjari na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi. Aidha, Benki na taasisi mpya za fedha zimeanzishwa nchini kwa pande zote za Muungano ambapo hadi kufikia Desemba, 2013 kulikuwa na jumla ya Benki na taasisi za kifedha 53 zinazofanya kazi nchi nzima.

***Ukusanyaji wa mapato***

Ukusanyaji wa mapato nchini umekuwa ukiimarika na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kugharamia shughuli za uendeshaji wa Serikali. Kutokana na kuimarisha ukusanyaji wa mapato, mafanikio makubwa yamepatikana katika kuimarisha miundombinu ya ukusanyaji mapato; kutoa huduma za jamii hususan elimu, afya na maji; ulinzi na usalama; na kusimamia na kutoa haki kwa wananchi.

***Uvuvi wa Bahari Kuu***

Mafanikio makubwa yamepatikana katika Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu tangu ilipoanzishwa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kwa Sheria Na.1 ya mwaka 1998. Mamlaka imewezesha kukusanya Dola za Marekani 5,381,158 na hivyo kuchangia katika Pato la Taifa kutokana na mauzo ya leseni. Aidha, uwepo wa Taasisi moja inayotoza gharama za uvuvi wa Bahari Kuu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni, uwakilishi mmoja ndani na nje ya Nchi kuhusiana na mawasiliano yanayohusu Bahari Kuu ya Tanzania umeondoa kabisa tatizo la ushindani wa kibiashara kwa pande mbili za Muungano.

### 2.6.3 Mafanikio ya Ulinzi na Usalama

Vikosi vya ulinzi na usalama vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ngao muhimu ya kulinda na kutetea haki na maslahi ya wananchi wa Taifa hili. Kwa kipindi chote cha Miaka 50 ya Muungano suala la kulinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Ardhini, Angani na Majini) limepewa kipaumbele. Mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuwa salama kutokana na ulinzi madhubuti wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na vikosi vingine na wananchi wa pande zote mbili za Muungano.

Katika kudumisha moyo wa uzalendo na mshikamano wa kitaifa, vijana wameendelea kuandaliwa kwa ukamilifu katika shughuli za ulinzi na uzalishaji mali kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa Tanzania Bara na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa Zanzibar kwa Mujibu wa Sheria na kwa kujitolea. Lengo la hatua hiyo ni kuwafundisha vijana wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulitumikia Taifa katika nyanja za kijamii, uchumi na ulinzi wa Taifa.

Usalama wa raia na mali zao umeendelea kudumishwa katika kipindi cha Miaka 50 ya Muungano. Ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na wadau wake katika ngazi zote umekuwa ukiimarika. Hali hiyo imeimarisha dhana ya ulinzi shirikishi ambayo imesaidia kwa kiwango kikubwa kudumisha amani na utulivu na kwa hivyo kudumisha Muungano. Hii imejidhihirisha kutokana na juhudi za Serikali zote mbili pamoja na wananchi kuliwezesha Jeshi la Polisi kutekeleza majukumu yake kwa wananchi na kwa wadau wengine. Aidha, suala la udhibiti wa uingiaji na utokaji wa watu nchini na udhibiti wa wahamiaji haramu limefanikiwa kwa kiasi kikubwa chini ya usimamizi wa Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na wananchi.

### 2.6.4 Mafanikio ya Kijamii

Mafanikio makubwa yamepatikana katika miaka 50 ya Muungano ambapo huduma za jamii zimeimarika, hususan katika sekta za afya, maji, elimu, ustawi na maendeleo ya jamii, na makazi. Fursa katika nyanja za jamii na utamaduni ni nyingi na zinazogusa mtu mmoja mmoja, vikundi na au taasisi. Kiwango cha upatikanaji wa huduma hizo katika maeneo mengi ya nchi ni kielelezo tosha kuwa Muungano huo umesimamia utu, usawa na maendeleo ya jamii ya Watanzania. Aidha, udugu wa damu umeimarika sana kwani Watanzania wa pande hizo mbili wameungana katika misingi ya ndoa na urafiki uliojengeka na kuimarika. Hali hii imechangia kupunguza migawanyiko ya kijamii na kuondoa hisia za ukabila na ubaguzi miongoni mwao.

#### *Elimu ya Juu*

Tanzania imefanikiwa sana kumkomboa mwananchi kielimu kwa kutoa fursa za elimu kwa wananchi walio wengi na kuwawezesha kupambana na changamato zinazoikabili jamii na Taifa kwa ujumla. Ubora wa elimu ya juu umeimarika kwa kiasi kikubwa kutokana na kuwepo kwa Taasisi za Elimu za Muungano kama vile Tume ya Pamoja ya Vyuo Vikuu Tanzania, Bodi ya Mikopo

ya Elimu ya Juu na Baraza la Mitihani la Taifa. Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inatoa Mikopo kwa wanafunzi wenye sifa waliodahiliwa katika taasisi za elimu ya juu Tanzania Bara na Zanzibar. Kumekuwepo na ushirikiano mkubwa katika suala la elimu ya juu. Kwa mfano, kati ya wanafunzi 600 kutoka Zanzibar wanaodahiliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, wanafunzi 400 kati yao wanapatiwa mikopo na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Wanafunzi 200 waliosalia wanapata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Idadi ya wanafunzi kutoka sehemu moja ya Muungano kwenda kusoma katika vyuo vya elimu ya juu katika upande mwingine wa Muungano imeongezeka. Hali hiyo imeimarisha kwa kiasi kikubwa ubora wa elimu ya juu kwani kumekuwa na ongezeko la Vyuo vya Elimu ya Juu kutoka 25 vilivyokuwepo mwaka 2005 hadi 63 vilivyopo mwaka 2014.

***Uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza fursa za ajira***

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imewawezesha Wananchi kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuongeza ajira kupitia utekelezaji wa programu mbalimbali za maendeleo. Programu hizo zimefanikiwa kuinua hali za wananchi, kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii wa pande zote mbili kwa kuanzisha miradi na programu mbalimbali. Miradi na Programu hizo ni pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(Tanzania Social Action Fund - TASAF);* Programu ya Usimamizi wa Bahari na Pwani ya Tanzania *(Marine and Coastal Environmental Programme - MACEMP);* Mradi wa Kutoa Mikopo kwa ajili ya Miradi Midogo Midogo *(Small Entrepreneur Loan Facility-SELF)* na Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(Agriculture Sector Development Programme-ASDP).*

Miradi na Programu hizo zinazingatia viashiria vya malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG) kama vilivyoainishwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzíbar (MKUZA) kwa kutumia dhana ya ushirikishwaji wa jamii. Miradi hiyo kwa ujumla wake imekuwa chachu muhimu ya maendeleo ya wananchi katika pande zote za Muungano kwani imeongeza fursa za ajira, kipato, kuimarisha miundombinu ya huduma za kijamii na hivyo kupunguza umaskini nchini.

### 2.6.5 Mafanikio katika Sayansi na Teknolojia

***Utafiti***

Serikali zote mbili zimetoa kipaumbele katika masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa kuanzisha na kugharamia taasisi za utafiti kwa lengo la kufanya utafiti, kukusanya, kutunza na kusambaza taarifa za sayansi na teknolojia nchini. Serikali kupitia taasisi hizo imewezesha kupatikana kwa wataalamu na watafiti pamoja na kufanyika kwa tafiti zenye manufaa kwa nchi. Aidha, Serikali imepokea na kusambaza teknolojia mpya kutoka sehemu nyingine nje ya nchi kupitia taasisi hizo.

***Utabiri wa Hali ya Hewa***

Huduma ya utabiri wa hali ya hewa katika kipindi cha Muungano imekuwa inatolewa kwa nchi nzima, Tanzania Bara na Zanzibar. Huduma inajumuisha utabiri wa hali ya hewa kwa kila siku, siku tano na siku kumi. Aidha, tahadhari zimekuwa zikitolewa kuhusu mvua kubwa, mafuriko, upepo mkali na ukame. Huduma hii imekuwa ni ya mafanikio kwa wananchi kwa jumla, ambapo Serikali imeimarisha huduma kwa kuweka miundombinu imara na ya kisasa kama vile kuongeza idadi ya vituo na kufikia 1,600 vya kupimia mvua nchini kote. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa imefanikiwa kuanzisha vituo vya hali ya hewa na kilimo (*agromet stations*) ambavyo hutoa taarifa muhimu zinazowasaidia wakulima kwenye shughuli zao za kilimo. Vilevile, Serikali imeweka na kufunga rada mbili za hali ya hewa, mtambo wa kuchambua takwimu za hali ya hewa, mtambo wa kuhakiki vifaa vya kupima mgandamizo wa hewa ili kuimarisha huduma za utabiri wa hali ya hewa.

***Ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano***

Upo ushirikiano mkubwa baina ya taasisi zisizokuwa za Muungano kutoka pande zote mbili. Taasisi hizi hushirikiana katika kutekeleza majukumu yao ili kuongeza ufanisi. Serikali zote mbili zimeweka utaratibu wa vikao vya kisekta vya ushirikiano kwa Wizara, Idara, na Taasisi zisizo za Muungano. Lengo la kufanya vikao hivyo ni kuimarisha ushirikiano kwa manufaa ya Watanzania. Vikao hivi vimekuwa vikijadili masuala ya kisekta kwa kubadilishana uzoefu, ujuzi, utaalamu, sera, mafunzo na ushiriki katika masuala ya kimataifa. Kufanyika kwa vikao 124 vya ushirikiano katika kipindi cha mwaka 2000 hadi mwanzoni mwa mwaka 2014 ni mafanikio makubwa.

Aidha, ushirikiano katika matukio mbalimbali yanayotokea katika pande mbili za Muungano husaidia utoaji wa huduma za haraka kwa jamii. Mfano mzuri ni pale matukio ya majanga na dharura yanapotokea. Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na mamlaka za kiraia, taasisi za Muungano na watu binafsi wamedhihirisha umoja na mshikamano mkubwa katika vipindi vya majanga yaliyoikumba nchi yetu kwa vipindi tofauti. Kwa mfano, katika ajali ya kuzama Meli ya *MV Spice Islanders* iliyotokea tarehe 10 Septemba, 2011 katika Mkondo wa Nungwi, ajali ya kuzama Boti ya *MV Skargit* iliyotokea karibu na Kisiwa cha Chumbe, Zanzibar tarehe 18 Julai, 2012, tukio la jengo la ghorofa 16 lililoporomoka Dar es Salaam tarehe 29 Machi, 2013 Idara zinazoshughulika na maafa za pande mbili za Muungano zilishirikiana kwa karibu kukabili maafa hayo. Ushirikiano huo, umeimarisha upendo, mshikamano na kuaminiana na hivyo kuufanya Muungano kuwa imara zaidi.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akiwa pamoja na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein wakiwa na Viongozi wengine wakati wa maafa ya kuzama kwa meli ya MV Spice Islander iliyotokea Zanzibar Septemba, 2011.*

# Changamoto za Muungano

## 3.1 Utangulizi

Katika kipindi cha Miaka 50 ya Muungano, Tanzania imepata mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali na hivyo kuimarisha na kuleta maendeleo kwa wananchi wa pande mbili za Muungano na Taifa kwa ujumla. Aidha, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, zimejitokeza changamoto mbalimbali za kisiasa, kiuchumi, ulinzi na usalama, kijamii, na katika sayansi na teknolojia; ambazo Serikali zote mbili kwa kushirikiana na wananchi wamezikabili kwa weledi na ujasiri mkubwa. Tunapoelekea kuanza awamu ya pili ya Miaka 50 ya Muungano, Serikali zote mbili na wananchi wake zimedhamiria kuendeleza kwa kasi, nguvu na ari zaidi, jitihada za kukabiliana na changamoto hizo ili kukuza ustawi na maendeleo ya wananchi na kulinda, kuimarisha na kudumisha Muungano.

## 3.2 Changamoto za Ujumla

### 3.2.1 Kisiasa

*Kukua na kupanuka kwa demokrasia nchini:* Tanzania imeshuhudia kukua na kupanuka kwa demokrasia kulikoendana na kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992. Mfumo huo umetoa nafasi na uhuru kwa watu kutoa maoni na kuhoji utendaji wa Serikali kwa uwazi zaidi na hivyo kuimarisha utendaji wa Serikali. Aidha, kukua na kupanuka kwa demokrasia kumetoa mwanya kwa baadhi ya wanasiasa kuhimiza wananchi juu ya maendeleo na wengine kupotosha juu ya masuala mbalimbali yanayohusu Muungano ikiwemo utendaji wa Serikali.

*Uhuru wa Vyombo vya Habari:* Kukua kwa demokrasia kumeongeza uhuru wa vyombo vya habari (magazeti, radio na televisheni) ambavyo baadhi yake vimetumia uhuru huo kupotosha wananchi na kusababisha mgawanyiko unaohatarisha ustawi wa Muungano.

*Uimarishwaji wa Taasisi za Muungano:* Tanzania imeshuhudia changamoto juu ya uimarishwaji wa Taasisi zilizowekwa kikatiba na kisheria za kushughulikia Mambo ya Muungano ikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya mawasiliano na urejeshaji wa taarifa. Katika kipindi hicho, baadhi ya taasisi kama vile Tume ya Pamoja ya Fedha, Msajili wa Vyama vya Siasa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi zimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria. Hata hivyo, kumekuwepo changamoto ya kuzipa mamlaka kamili na taswira ya pande mbili za Muungano ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

*Elimu kwa Umma kuhusu Muungano:* Kumekuwepo na changamoto ya uelewa mdogo wa wananchi, hususan vijana, kuhusu historia na chimbuko la Muungano. Aidha, Serikali zote mbili zimeendeleza jitihada za kujenga uelewa wa pamoja na unaolingana kuhusu historia na chimbuko la Muungano ili kuondoa mashaka juu ya uhalali wa Muungano. Pamoja na jitihada hizo uelewa wa wananchi juu ya masuala mbalimbali ya Muungano siyo wa kuridhisha. Kutokana na hali hiyo, Serikali zote zitafanya jitihada zaidi za kuelimisha wananchi ili wawe na uelewa wa pamoja kuhusu Muungano.

*Uimarishaji wa Mshikamano wa Watu:* Serikali zote mbili zimeimarisha mshikamano wa wananchi ili wajione kuwa ni Watanzania wa Taifa moja. Hata hivyo, hali hiyo imeendelea kuwa changamoto kutokana na baadhi ya wanasiasa na makundi mbalimbali katika jamii kuanza kuhamasisha Utanganyika na Uzanzibari jambo linalofifisha jitihada za umoja na mshikamano wa kitaifa.

### 3.2.2 Kiuchumi

*Utangamano wa Uchumi:* Kuingiliana na kutangamana kwa uchumi baina ya Tanzania na nchi nyingine duniani, kumefungua milango na fursa za kuimarisha uchumi, maendeleo na ustawi wa Watanzania. Hata hivyo, utangamano huo mara nyingine huleta changamoto zinazotokana na misukosuko ya kiuchumi, kisiasa au kijamii kwa nchi tunazoshirikiana nazo. Hali hiyo husababishwa na uhusiano wa karibu uliopo ambao hufanya matatizo ya nchi tunazoshirikiana nazo kuwa ni ya Taifa na hivyo huathiri kasi ya maendeleo. Taifa linapoelekea katika awamu ya pili ya miaka 50, linapaswa kuweka mikakati madhubuti ya kushirikiana na nchi nyingine hususan zile zinazoibuka na kuwa na nguvu za

kiuchumi ili iweze kwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi duniani kwa lengo la kuinua Pato la Taifa kwa manufaa ya wananchi wake.

*Mikakati ya Pamoja ya Kuimarisha Uchumi:* Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotegemea bidhaa kutoka katika soko la nje zaidi kuliko soko la ndani. Hivyo, changamoto kubwa inayolikabili Taifa ni kuwekwa na kutekelezwa mikakati ya pamoja ya kuimarisha uchumi katika pande mbili za Muungano na kuongeza kasi ya kusimamia mikakati hiyo ya uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi kwa ajili ya soko la ndani na kuuza nje ili kuinusuru nchi kugeuzwa kuwa soko la bidhaa duni kutoka nje. Aidha, ipo haja ya kuendelea kuwepo ushirikiano wa karibu baina ya Serikali mbili na sekta binafsi kwani uchumi endelevu unategemea nguvu na mchango wa kila upande.

*Fursa za Ajira:* Tatizo la ukosefu wa ajira ni changamoto inayozikabili nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania. Changamoto inayolikabili Taifa kwa sasa ni kuongeza fursa za ajira na kuwanufaisha wananchi walio wengi hasa vijana ambao ndio kundi kubwa katika soko la ajira. Katika kuhakikisha kuwa Sera ya Uwekezaji inatekelezwa kwa ukamilifu, wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wamewekeza katika mashamba makubwa, viwanda, madini, mafuta na gesi, na katika sekta ya utalii. Uwekezaji huo umetoa fursa za ajira kwa vijana. Hata hivyo, changamoto kubwa ni namna ya kuongeza fursa za ajira kwa kuwawezesha vijana wengi zaidi kujiajiri na kuajiriwa.

*Kuimarisha Miundombinu:* Serikali zote mbili zimejenga na kuimarisha miundombinu ikiwemo barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na umeme. Lengo ni kukidhi mahitaji ya watumiaji yatokanayo na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii na kuwezesha usafirishaji wa bidhaa na watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Changamoto iliyopo ni kuimarisha na kutunza miundombinu hiyo pamoja na kuendeleza ujenzi mpya na uwekaji wa miundombinu na mitambo ya kisasa ya mawasiliano.

*Udhibiti wa Kasi ya Mfumuko wa Bei:* Uchumi tulivu pamoja na mambo mengine huhitaji uwepo wa bei zinazokua kwa umakini. Kupanda kwa bei kusikoendana na uwezo wa uzalishaji mali na uwezo wa wananchi kununua bidhaa na huduma ni changamoto kubwa kwa uchumi. Serikali imejitahidi kukabiliana na suala hilo. Kuongezeka kwa kasi ya ongezeko la bei kunaathiri wananchi ambao kipato chao ni kidogo na uwezo wao wa kununua ni mdogo.

Kwa upande wa wawekezaji mfumuko wa bei umekuwa unaathiri ununuzi wa bidhaa za kati na za msingi, hivyo kupunguza uwezo wao wa kununua na kuwekeza mitaji. Pamoja na kuwa Serikali zimekuwa zikijitahidi kukabiliana na changamoto hiyo, bado mfumuko wa bei umeendelea kuathiri wananchi walio wengi kutokana na uzalishaji mdogo wa bidhaa usiotoshelevu. Hivyo, jitihada zilizopo zinapaswa kuendelezwa na kuimarishwa ili kuleta matokeo endelevu katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

*Fursa za Uchumi katika Jumuiya za Kikanda na Mtangamano wa Utatu (SADC, COMESA, EAC):* Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kumetoa fursa za kiuchumi kwa Tanzania. Fursa hizo ni pamoja na uwepo wa soko la pamoja, eneo huru la biashara na umoja wa forodha. Uwepo wa fursa hizo umetoa uhuru wa raia wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kufanya shughuli za kiuchumi ambazo zimesaidia kuongeza bidhaa zinazohitajika ndani ya nchi, kupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje kwa kuwa zinapatikana ndani ya Jumuiya na kuondoa vikwazo vya soko. Changamoto iliyopo ni kuhakikisha kwamba Tanzania inazalisha na kusambaza bidhaa zinazohitajika ndani ya Jumuiya ili kuiwezesha kuwa mshiriki imara katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### 3.2.3 Ulinzi na Usalama

*Kujenga Jeshi la Kisasa:* Ulinzi na usalama wa Taifa limekuwa ni jambo la kipaumbele tangu kuasisiwa kwa Muungano. Vyombo vya ulinzi na usalama vilivyopo toka mwaka 1964 vimeimarika kwa kuwa na mbinu, vifaa, mahusiano na umahiri katika utendaji. Hata hivyo, rasilimali fedha na rasilimali watu zilizoelekezwa katika vyombo hivyo haziendani na kasi ya ukuaji wa mahitaji na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Mwelekeo duniani hivi sasa ni kuwa na jeshi dogo lenye weledi na vifaa vya kisasa vitakavyomudu mahitaji ya sasa. Katika kuendeleza ulinzi na usalama, Tanzania inapaswa kuwianisha mipango na rasilimali zake katika kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama. Changamoto ni upungufu wa fedha za kuimarisha ulinzi na usalama ili kuendana na mabadiliko haya.

*Utii wa Sheria:* Utii wa Sheria ni wajibu wa kila raia ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na ni suala linalopewa kipaumbele na Serikali zote mbili. Aidha, katika Programu ya Kuimarisha Utendaji wa Jeshi la Polisi, msisitizo umewekwa kwa wananchi wenyewe kuwa watii kwa Sheria,

wasimamizi wa utekelezaji wa Sheria bila shuruti, na vyombo vya utekelezaji wa Sheria kwa mihimilii kuwajibika kutenda haki. Changamoto iliyopo ni kuendeleza jitihada za kutoa elimu kwa wananchi kuhusu wajibu wao wa kutii na kutekeleza Sheria bila shuruti.

*Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi:* Tanzania inapakana na nchi nane, jambo linalotoa fursa za ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa Tanzania. Hata hivyo, urefu wa mpaka na tofauti ya hali ya amani na utulivu wa nchi jirani ni changamoto kwa Taifa katika kulinda mipaka yake. Kimsingi, ulinzi wa mipaka ya Taifa unahitaji ushiriki wa wananchi na kuimarishwa kwa vyombo vyenye wajibu wa kulinda mipaka ya nchi. Jukumu la kuimarisha jeshi, ulinzi na usalama wa mipaka yetu ni jambo muhimu. Hivyo, Serikali haina budi kuendelea kukabiliana na changamoto hiyo kwa kuhakikisha kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vina uwezo wa kutosha na mbinu za kisasa zaidi, kwa kushirikisha wananchi wake na kutumia sayansi na teknolojia.

*Kuimarisha Amani na Utulivu:* Kuendelea kuwa na uchumi imara na uwepo wa jamii yenye maendeleo endelevu kunahitaji mazingira ya amani na utulivu. Taifa limeshuhudia baadhi ya wananchi wakitumia vibaya uhuru wao wa kisiasa, kisheria na uwezo wao wa rasilimali kufanya vitendo vinavyohatarisha amani na utulivu nchini. Aidha, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na wimbi la wananchi kujichukulia Sheria mkononi katika matukio ya uvunjifu wa amani. Katika kipindi hiki pia, yamejitokeza matukio ya kuingia na kusambaa kwa silaha ndogo ndogo kutoka nchi jirani kutokana na hali ya kukosekana kwa amani katika nchi hizo.

Sanjari na hilo, kumeibuka uhalifu wa kutumia mitandao ya kompyuta, utakatishaji wa fedha haramu, wizi wa kwenye mabenki kwa kupitia mashine za kutolea pesa (*Automated Tellering Machine - ATM),* usafirishaji wa dawa za kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na makosa ya kughushi. Matukio hayo yanaibua na kuleta changamoto mpya zinazohitaji ufumbuzi makini na wa haraka. Hivyo, katika juhudi za kuimarisha uchumi na kuwaletea wananchi maendeleo endelevu, Serikali zote mbili hazina budi kuhakikisha kuwa vitendo hivyo vya uhalifu vinaendelea kudhibitiwa. Vilevile, katika miaka ya hivi karibuni pameibuka matukio kadhaa yanayohisiwa kuwa ya kigaidi na uharamia katika eneo la Afrika Mashariki na ukanda wa Bahari

ya Hindi.  Matukio hayo yameongeza hofu kwa jamii na kuathiri shughuli mbalimbali za maendeleo nchini. Suala la kupambana na wimbi la ugaidi ni changamoto kubwa ambapo Serikali haina budi kuongeza nguvu kwa kushirikiana na mataifa na wadau mbalimbali kuhakikisha kuwa watu, nchi na taasisi zake hazitumiki wala kujihusisha na vitendo hivyo.

*Vita Dhidi ya Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya:* Ujenzi wa jamii imara na nguvukazi kwa vizazi vijavyo unahitaji kuhakikisha kuwa vijana wanaendelezwa na kutumika ipasavyo nchini. Dawa za kulevya ni changamoto kubwa inayoikabili Taifa hususan katika matumizi, uuzaji na usafirishaji ndani na nje. Katika kuhakikisha suala hilo linapata ufumbuzi, Serikali zitaendelea kuimarisha programu na mikakati iliyopo ili kuhakikisha kuwa afya ya akili ya jamii ya Watanzania inalindwa dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo mihadharati, bangi na mirungi. Jitihada za kuendelea kupiga vita biashara hiyo ni endelevu hasa katika kuhakikisha kuwa nchi haitumiki kama njia ya kupitishia dawa hizo.  Aidha, Serikali zitaendelea kuzuia uzalishaji wa bangi na mirungi mashambani na kuendelea kuelimisha jamii juu ya athari ya matumizi ya madawa ya kulevya.

*Wahamiaji Haramu:* Kijiografia, Tanzania imepakana na Bahari ya Hindi na nchi jirani nane zinazoifanya nchi kuwa na mipaka mipana yenye mianya na nafasi za kutua ufukweni. Hali hiyo,  imetoa fursa kwa watu wanaotaka kuingia na kutoka nchini kinyume cha Sheria kufanya hivyo. Pia mianya hiyo, imekuwa ni changamoto kubwa katika udhibiti wa wahamiaji haramu. Aidha, kuingia nchini kwa wahamiaji wengi miaka mingi iliyopita kutoka Mataifa mbalimbali na kuishi kwa muda mrefu nchini ni changamoto kubwa katika suala la utambuzi wa uraia wa wahamiaji hao. Serikali itaimarisha juhudi za kudhibiti wahamiaji haramu kwa kuwabaini na kuwachukulia hatua zinazostahiki.

### 3.2.4 Kijamii

*Kuongezeka kwa Mahitaji ya Huduma za Jamii:* Taifa limeshuhudia ongezeko kubwa la idadi ya watu nchini kunakotokana na sababu mbalimbali zikiwemo uzazi bila ya mpango na ndoa za mapema.  Kutokana na ongezeko hilo, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora.  Miongoni mwa huduma hizo ni afya, elimu, maji safi na salama, nishati ya umeme na miundombinu ya barabara. Changamoto kwa Serikali ni

kubuni njia mbadala zitakazowawezesha wananchi kutumia rasilimali zilizopo kwa njia endelevu.

*Ukuzaji Sekta ya Michezo:* Katika miaka ya hivi karibuni, michezo imekuwa njia ya kukuza ajira, kuimarisha afya, kuleta burudani na uhusiano nchini, hususan kwa vijana. Serikali zote mbili zimekuwa zikitoa msukumo wa pekee katika kusimamia sekta hiyo na kuhakikisha kuwa Tanzania inapata sifa kubwa kimataifa. Hata hivyo, pamoja na jitihada mbalimbali za kuinua michezo ikiwemo ujenzi wa viwanja, ajira ya makocha wa kigeni na kutoa misaada ya fedha na vifaa, bado Tanzania haina mafanikio makubwa katika sekta hiyo ikilinganishwa na Mataifa mengine duniani. Changamoto kubwa ni kukuza ajira na kuongeza mchango wa sekta ya michezo katika uchumi; kujenga miundombinu na kuongeza idadi ya wataalamu wa michezo mbalimbali ili kuongeza fursa za kuibua na kukuza vipaji na kuwezesha wanamichezo Watanzania kufanya vizuri zaidi katika mashindano ya kitaifa na kimataifa.

*Kutunza na Kuendeleza Mila na Utamaduni wa Mtanzania:* Utamaduni ni moja ya Kigezo na kielelezo kikuu cha utambulisho wa Taifa la Tanzania. Hilo linajidhihirisha kupitia mfumo mzima wa maisha ya kila siku yenye kuhusiana na mambo mbalimbali yakiwemo mavazi, ngoma, vyakula, upole na ukarimu, mila na desturi, pamoja na lugha ya Kiswahili ambayo imekuwa kiungo kikubwa kinachowaunganisha Watanzania. Serikali zote mbili, kwa pamoja zimeshirikiana kuhakikisha utamaduni wa Mtanzania unaendelezwa na kudumishwa. Hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa ili kufikia lengo hilo. Pamoja na jitihada hizo, mmong'onyoko wa maadili kwa baadhi ya wananchi hususan vijana kunakosababishwa na mwingiliano mkubwa wa utamaduni na mataifa ya nje bado ni changamoto kubwa.

### 3.2.5 Sayansi, Teknolojia na Utafiti

Sayansi na Teknolojia ni eneo ambalo maendeleo yake duniani yanakua kwa kasi kubwa. Katika kuwezesha maendeleo ya kweli ya sayansi na teknolojia nchini, suala la utafiti ni jambo linalopaswa kupewa msukumo wa pekee. Kwa kutambua hilo, Serikali inatenga rasilimali fedha ili kugharamia shughuli za utafiti. Serikali zote mbili zimewezesha kufanyika kwa tafiti katika Sekta za kipaumbele. Changamoto kuu ni upatikanaji wa rasilimali fedha za kukidhi mahitaji ili kuhakikisha kuwa kiwango cha kukua kwa sayansi na teknolojia nchini kinakwenda sambamba na ukuaji huo duniani. Mahususi ni namna

ya kukidhi Azimio la Maputo *(Maputo Declaration)* ambapo Serikali za nchi wanachama wa SADC zilikubaliana kutenga asilimia moja ya Pato la Taifa katika bajeti zake kwa ajili ya shughuli za utafiti. Hivyo, Serikali zitaendeleza jitihada za kugharamia mahitaji ya utafiti, kuwajengea uwezo watafiti, kuweka mfumo imara wa uratibu na matumizi ya matokeo ya tafiti hizo. Aidha, juhudi zitaongezwa kushirikisha sekta binafsi katika masuala ya utafiti kwa kuwa kwa sasa mchango wake bado ni mdogo sana.

## 3.3 Changamoto Mahususi za Muungano

Kama ilivyo kwa Mataifa mengine yaliyoungana, Muungano wa Tanzania umekabiliwa na changamoto mbalimbali katika kipindi cha miaka 50 cha uhai wake. Aidha, zipo changamoto zilizopatiwa ufumbuzi, na ambazo ziko katika hatua mbalimbali za kupatiwa ufumbuzi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaendelea kuchukua hatua madhubuti za kukabiliana na kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto hizo kwa njia ya mazungumzo yanayojumuisha wajumbe wa pande zote mbili katika ngazi za wataalam, watendaji wakuu na viongozi wa kitaifa. Changamoto hizo na namna zilivyofanyiwa kazi zimeainishwa katika vipengele vifuatavyo:-

### 3.3.1 Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, imeainisha kuwa haki za binadamu na utawala bora ni suala la kikatiba. Kwa kuwa Katiba na mikataba ya kimataifa husimamiwa na kutekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hoja ya msingi iliyojitokeza ni kuwa Sheria Na. 7 ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2001 inayosimamiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilikuwa haitekelezwi Zanzibar. Hivyo, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho Oktoba 2006 ili kukidhi matakwa ya Tume kufanya kazi pande mbili za Muungano.

### 3.3.2 Uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu

Ukanda wa Uchumi katika Bahari Kuu unasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, Sheria Na. 1 ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu ya mwaka 1998 haikuhusisha taasisi za SMZ katika utekelezaji wake. Kutokana na hali hiyo, Sheria ilifanyiwa marekebisho

mwezi Februari, 2007 na kutambua taasisi zinazohusika na matumizi ya Bahari Kuu kwa upande wa Zanzibar na kuzijumuisha katika Kamati ya Utendaji ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Hivi sasa, Mamlaka ya kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ni moja, yenye Makao Makuu yake Zanzibar.

### 3.3.3 Utekelezaji wa Sheria ya Usafiri wa Majini

Masuala yote yanayohusu uchukuzi na usalama wa njia ya majini katika mikataba yote ya kimataifa inayoihusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanatekelezwa kupitia Sheria ya *Merchant Shipping* ya mwaka 2003. Baada ya mashauriano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Usafiri Baharini (International Maritime Organization - IMO), imekubalika kuwa Zanzibar iwe na Mamlaka yake ya Usafiri Majini (Zanzibar Maritime Authority) chini ya Sheria yake ya Maritime Transport iliyoanza kutumika mwaka 2006. Kupitia Sheria hiyo, Zanzibar inatekeleza baadhi ya majukumu kulingana na mikataba ya kimataifa chini ya usimamizi wa Serikali ya Muungano wa Tanzania.

### 3.3.4 Mgawanyo wa Mapato ya Misaada na Uwezo wa Zanzibar Kukopa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipata misaada mbalimbali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na nchi wahisani kwa ajili ya kutekeleza programu za maendeleo. Hata hivyo, mgawanyo wa mapato hayo umeleta changamoto baina ya pande mbili za Muungano kwa upande mmoja kuonekana kutopata mgao stahiki. Pande mbili za Muungano zimeridhia Zanzibar iendelee kupata mgao wa asilimia 4.5.

Aidha, hoja ya uwezo wa Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi imepata ufumbuzi. Zanzibar ina uwezo wa kukopa ndani ya nchi bila ya kikwazo chochote. Kwa mikopo ya nje, SMZ inakopa kupitia udhamini wa Serikali ya Muungano ambapo SMT huhamisha mkopo unaoombwa kutoka nje kwenda SMZ. Serikali zote mbili zinashirikiana katika maandalizi ya bajeti, ikiwemo mapendekezo ya upatikanaji wa Misaada na Mikopo ya kibajeti kutoka nje.

### 3.3.5 Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa SMT

Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa kwa lengo la kuchochea maendeleo katika majimbo ya uchaguzi ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, kwa upande wa Zanzibar ilijitokeza changamoto kwa

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutohusishwa katika Kamati ya Usimamizi wa Mfuko. Katika kukabiliana na hali hiyo, SMZ imeamua kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa malengo sawa na Wabunge wa SMT.

### 3.3.6 Kodi Nyinginezo

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hainufaiki ipasavyo na kodi inayotokana na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mishahara ya wafanyakazi wa taasisi za Muungano waliopo Zanzibar pamoja na kampuni na mashirika yanayofanya kazi Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, pande mbili za Muungano zilikubaliana SMZ ipate sehemu ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye Kodi ya Mishahara ya Wafanyakazi (PAYE) na kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina wa SMZ wakati utaratibu wa kurekebisha Sheria unaendelea.

### 3.3.7 Ongezeko la Gharama za Umeme

Kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa umeme, mwaka 2008, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) iliongeza bei za umeme kwa watumiaji umeme wa Tanzania Bara na Zanzibar. Vilevile, mwaka 2011, bei za umeme pamoja na *"Demand Charge"* ziliongezeka. Kupanda kwa gharama hizo kulileta malalamiko kwa watumiaji wa umeme kwa upande wa Zanzibar kutokana na kutotolewa kikamilifu kwa sababu halisi ya ongezeko hilo. Baada ya mjadala wa kitaalamu na wa kina, hatimaye makubaliano yalifikiwa ambapo TANESCO na ZECO walitakiwa kuongeza uwazi katika gharama za uzalishaji na usambazaji umeme nchini.

### 3.3.8 Wafanyabiashara wa Zanzibar Kutozwa Kodi mara Mbili

Kuwepo kwa tofauti ya ukadiriaji wa viwango vya thamani za bidhaa, na kodi ya forodha baina ya Ofisi za TRA zilizoko Tanzania Bara na zile zilizoko Zanzibar, kumeleta changamoto kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Katika kuhakikisha kuwa changamoto hiyo haijitokezi tena, pande mbili za Muungano zimekubaliana kuwa mfumo unaotumika sasa wa tathmini uendelee katika kipindi cha mpito, wakati TRA inafanya tathmini ya mfumo wa kodi ya forodha ili kubaini faida na upungufu uliopo.

## 3.4 Changamoto Mahususi zinazotafutiwa ufumbuzi

### 3.4.1 Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

Katika kuhakikisha kuwa Zanzibar inashiriki kikamilifu na kutumia fursa zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Zanzibar iliwasilisha miradi ya maendeleo ya kiuchumi kwa ajili ya kujumuishwa katika Miradi ya Kikanda inayotekelezwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi iliyowasilishwa kwa Sekretarieti ya Jumuiya kwa ajili ya kutafutiwa fedha kwa Wabia wa Maendeleo na Wawekezaji ni ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba; Bandari ya Maruhubi na mradi wa Ujenzi wa Chelezo (Dry Dock Construction) na Kivuko (Roll on Roll off – RORO) kati ya bandari ya Zanzibar, Dar es Salaam, Pemba, Tanga na Mombasa.

### 3.4.2 Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia

Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia ni mambo yaliyomo kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano. Pamekuwepo na hoja ya namna ya kugawana mapato yatokanayo na rasilimali ya mafuta na gesi asilia yatakapopatikana. Baada ya majadiliano baina ya viongozi wa SMT na SMZ, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wameridhia kuliondoa suala la uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano katika utaratibu unaoendelea wa kupata Katiba Mpya.

### 3.4.3 Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Kimataifa

Imeonekana kwamba Zanzibar haishirikishwi ipasavyo katika masuala ya ushirikiano wa kiuchumi unaohitajika na Taasisi za Kimataifa. Katika kushughulikia suala hilo, Serikali zote mbili zilitayarisha mwongozo kuhusu ushirikishwaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala yote ya Kimataifa. Mwongozo huo umezingatia maeneo kuhusu ziara za viongozi wa kitaifa; mikutano ya kimataifa; nafasi za masomo ya elimu ya juu nje ya nchi na utafutaji wa fedha za misaada au mikopo za kutekeleza miradi mbalimbali kutoka nje ya nchi. Aidha, suala hilo ni miongoni mwa changamoto zitakazopatiwa ufumbuzi ndani ya utaratibu unaoendelea wa kupata Katiba Mpya.

### 3.4.4 Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano

Nafasi za ajira kwa Wazanzibari katika taasisi za Muungano ni mojawapo ya masuala ambayo yamejadiliwa katika vikao vya mashauriano. Aidha, Serikali zimekubaliana yafanyike marekebisho ya Sheria na kanuni; uwepo mkakati wa kiserikali wa kuhamasisha watumishi wa SMZ na Wazanzibari kuomba ajira zinazotangazwa na SMT au Taasisi za Muungano; kuhamasisha Taasisi za Muungano kuwa na ofisi Zanzibar; na Sekretarieti ya ajira katika utumishi wa umma kuhakikisha kuwa utaratibu wa kuendesha mahojiano unafanyika pia Zanzibar. Kwa nafasi zinazohitaji uteuzi, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hushauriana nafasi hizo zinapojitokeza. Kuhusu nafasi za watumishi wa kawaida kwenye taasisi za Muungano, utaratibu maalum umewekwa na uko katika hatua za utekelezaji.

### 3.4.5 Usajili wa Vyombo vya Moto

Kumekuwa na changamoto juu ya matumizi ya vyombo vya moto vinavyosajiliwa upande mmoja wa Muungano kutumika upande mwingine. Baada ya majadiliano ya Serikali zote mbili, imeonekana upo umuhimu wa kuwianisha Sheria za Usajili wa Magari ili gari ikitoka upande mmoja wa Muungano kwenda upande mwingine, ijulikane kuwa imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kanzidata inayojumuisha taarifa kuhusu usajili wa magari ziimarishwe na kuwekwa bayana.

### 3.4.6 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha

Tume ya Pamoja ya Fedha imefanya tafiti mbalimbali na kutoa mapendekezo kwa Serikali zote mbili (SMT na SMZ). Mapendekezo yaliyowasilishwa mwaka 2006 yanajumuisha vigezo vya kuchangia gharama na kugawana mapato ya Muungano. SMT na SMZ zimefanyia kazi mapendekezo hayo. Changamoto kubwa ni kwa pande mbili za Muungano kukawia kufikia uamuzi kuhusu mapendekezo hayo. Hata hivyo, changamoto itatatuliwa katika Katiba Mpya itakayotungwa.

# Fursa na Matarajio ya Muungano kwa Miaka Ijayo

## 4.1 Utangulizi

Katika kipindi cha Miaka 50 tangu kuasisiwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili, 1964 na kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waasisi wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume walikuwa na dhamira nzuri ya kuhakikisha kuwa Muungano huo unadumishwa kwa manufaa ya kizazi kilichopo na vijavyo.

Dhamira na juhudi za Waasisi hao zimekuwa zikiendelezwa na viongozi wa awamu nyingine wa pande zote mbili za Muungano kwa kuendeleza misingi, kuweka na kutekeleza mikakati madhubuti ya Taifa. Kutokana na misingi hiyo, wananchi wamekuwa na imani na matarajio makubwa juu ya Muungano huo ambao umekuwa ni wa mfano barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha Miaka 50 ya Muungano, na changamoto zilizolikabili Taifa, yapo mambo kadhaa ambayo yanatoa fursa adhimu na adimu kwa Watanzania kujiletea maendeleo na ustawi wao. Kutokana na kuwepo kwa fursa hizo, Taifa lina matarajio makubwa katika kuendeleza mafanikio yaliyopatikana ambayo yataendelea kuimarisha zaidi Muungano.

Tanzania imeendelea kuwa nchi ya amani na utulivu. Hali hiyo siyo tu imewawezesha wananchi kufanya shughuli za kimaendeleo kwa uhuru na amani, bali pia imetoa fursa kwa wawekezaji kutoka nje kuwekeza nchini. Taifa likiwa linaelekea katika miaka ijayo ya Muungano, amani na utulivu inayotokana na maridhiano na kuvumiliana kwa makundi mbalimbali ya kisiasa na kijamii ni nyenzo muhimu ambayo italiwezesha Taifa kuendelea kustawi na kuwa kituo kikubwa cha uwekezaji duniani. Aidha, utungaji wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulioanza Machi, 2014 ni fursa muhimu katika kuimarisha Muungano huo na kudumisha Utawala Bora kwa kuzingatia maslahi ya pande zote mbili za Muungano.

## 4.2 Fursa

*Nafasi ya Tanzania Kijiografia:* Tanzania ipo katika eneo zuri kijiografia kwa vile imezungukwa na nchi sita zisizokuwa na mwambao wa bahari. Nchi hizo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia. Vilevile, ina ukanda wa pwani wenye urefu wa kilomita 1,424, wenye bandari za asili (Bagamoyo, Dar es Salaam, Lindi, Malindi, Mkoani, Mkokotoni, Mtwara, Tanga na Wete) ambazo huifanya Tanzania kuwa lango kuu la biashara kati ya nchi hizo jirani na nchi nyingine duniani. Hiyo ni fursa nzuri kwa Taifa kukuza biashara na kuchangia upatikanaji wa fedha za kigeni na ajira kwa wananchi. Hali kadhalika, uwepo wa Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote barani Afrika na milima mingine kama vile Meru, Udzungwa na Usambara pamoja na fukwe nzuri na za kipekee zilizopo Zanzibar ni fursa muhimu katika kuitangaza Tanzania, na hivyo kuvutia uwekezaji na kukuza biashara katika Sekta ya Utalii. Vilevile, bonde la mto Wami, Kilombero, Ruaha na Rufiji ni fursa nzuri ya kukuza na kuendeleza sekta ya kilimo.

*Kuwepo kwa Rasilimali za asili:* Tanzania ina rasilimali za asili nyingi kama vile gesi asili, hifadhi ya makaa ya mawe; hifadhi ya urani; joto ardhi (geothermal), mito na maziwa, upepo, nishati ya jua na rasilimali nyingine mbadala ambazo ni nyenzo muhimu katika uzalishaji wa nishati na kuchochea ukuaji wa viwanda. Tanzania pia imejaaliwa kuwa na madini ya *phosphate* ambayo huchanganywa na gesi asilia kuzalisha mbolea. Aidha, Taifa limebarikiwa kuwa na chokaa yenye ubora kwa uzalishaji wa saruji. Madini mengine ni pamoja na dhahabu, almasi, tanzanite, rubi, nikeli, bati, magadi, makaa ya mawe na chuma ambayo ni fursa inayoweza kutumika kujenga uchumi imara, kukuza ajira na kuongeza fedha za kigeni kwa Tanzania.

*Vivutio vya Utalii:* Tanzania ina mbuga za wanyama 15 maarufu duniani, zikiwemo Hifadhi za Ngorongoro, Serengeti, Manyara na Mikumi; mbuga za akiba 33, maeneo tengefu 43 ya mbuga za uwindaji yaliyodhibitiwa, na urithi mkubwa wa utamaduni wa Kitanzania ambao ni kivutio kwa watalii. Pia kuna hekta milioni 35.3 za misitu nyika na hifadhi za misitu za Taifa ikijumuisha misitu ya hifadhi ya asili ya Jozani, Ngezi na hifadhi ya Kisiwa cha Misali iliyoko Zanzibar.

*Mtangamano wa Kikanda:* Fursa nyingine ni soko la kikanda linalotokana na mtangamano wa kikanda ambapo Tanzania ni mwanachama katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Kupitia fursa hiyo, Tanzania inaweza kuuza bidhaa katika masoko ya Jumuiya hizo na hivyo kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa, jambo ambalo hukuza na kuongeza ajira na kipato cha Watanzania.

*Ardhi na Maji:* Tanzania ina hekta milioni 44.13 za ardhi yenye rutuba na inayofaa kwa kilimo, kati ya hizo hekta milioni 44 ziko Tanzania Bara na hekta milioni 0.13 ziko Zanzibar. Maeneo mengi ya nchi yanapata mvua za kutosha na kuna vyanzo vingi vya maji vikiwa ni pamoja na mito, maziwa na maji chini ya ardhi. Rasilimali hiyo ya maji pamoja na ardhi yenye rutuba ni fursa kubwa na nzuri ambayo inaweza kutumika katika kupanua kilimo cha umwagiliaji, na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo.

*Miundombinu:* Tanzania imepiga hatua kubwa katika kujenga na kuimarisha miundombinu ya barabara, mawasiliano na viwanja vya ndege. Kuimarika kwa miundombinu hiyo kunatoa fursa ya kuimarisha miundombinu mingine ya barabara, reli, na bandari. Hali hiyo inafungua maeneo mapya ya uwekezaji katika Sekta mbalimbali za kilimo, biashara, viwanda, madini na nyinginezo, na hivyo kuifanya Tanzania kupiga hatua kubwa katika uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma.

*Ukubwa wa eneo na nguvukazi ya kutosha:* Tanzania ina eneo la kilomita za mraba takriban 948,740. Ni nchi yenye eneo kubwa zaidi kuliko nchi nyingine za Afrika Mashariki na pia ni nchi ya 31 kwa ukubwa duniani. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 Tanzania ilikuwa na watu milioni 44.9, ambapo milioni 1.3 wako Zanzibar. Fursa iliyopo ni kuweka mikakati ya kutumia ardhi nzuri na rasilimali zilizopo katika ardhi kuzalisha mazao na bidhaa kwa ajili ya mahitaji ya ndani na kuuza nje. Aidha, nguvukazi iliyopo, ambayo kwa sehemu kubwa ni vijana, ni nguzo madhubuti katika kuzalisha mali na pia kununua bidhaa zinazozalishwa nchini kwa wingi ili kuimarisha uzalishaji wa viwanda vya ndani ya nchi.

*Fursa za Kijamii na Kiutamaduni:* Kiswahili ni lugha ya Taifa la Tanzania ambayo ilitumiwa na waasisi wa Taifa kuwaunganisha wananchi katika harakati za kupigania uhuru na hata baada ya uhuru wa Tanganyika na Zanzibar. Matumizi ya lugha ya Kiswahili ni fursa ambayo itaendeleza

umoja na mshikamano wa wananchi katika kipindi kijacho cha Muungano. Aidha, kupanuka kwa matumizi ya lugha hiyo katika nchi jirani za Burundi, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda, Somalia na Uganda, na kukubalika kutumika katika Umoja wa Afrika na SADC kumetoa fursa ya kuimarika kwa ushirikiano baina ya Tanzania na nchi hizo katika nyanja za uchumi, siasa na jamii. Pia, Kiswahili kimeongeza fursa za ajira na kuleta maendeleo kwa Watanzania ambao hutumika kama walimu, wakalimani, wafasiri, waongozaji wa watalii na watunzi wa vitabu.

Aidha, kuendelea kwa ushirikiano katika uwanja wa utamaduni baina ya Watanzania Bara na Zanzibar kunatoa fursa nzuri ya kukuza tamaduni za asili na hivyo kutambulika kimataifa. Tamasha la kimataifa la Sauti za Busara linalofanyika Zanzibar kila mwaka limekuwa jukwaa muhimu ambapo wasanii waliobobea kutoka pande zote za dunia hukutana na kuonesha kazi zao za sanaa. Jukwaa hilo linatoa fursa nzuri kwa wasanii wa Tanzania kutoka pande zote za Muungano kuendelea kutangaza utamaduni na Taifa kwa ujumla na pia kuongeza kipato chao.

## 4.3 Matarajio

Kwa kutambua na kuzingatia fursa na changamoto zilizopo, katika miaka ijayo, Serikali inatarajia kwamba Muungano utaimarika na mafanikio yaliyopatikana yataendelezwa kwa lengo la kuinua hali za maisha ya wananchi. Kuimarika na kudumu kwa Muungano huo kutakuwa ni nguzo muhimu ya kuendeleza udugu wa damu na matarajio ya Waasisi wa Muungano ya kuwa na Tanzania yenye uchumi imara, amani na utulivu, na haki na usawa kwa kila Mtanzania.

### Kisiasa

*Katiba Mpya:* Matarajio ya Watanzania ni kuwa na Katiba imara inayozingatia matakwa ya wananchi na mabadiliko muhimu ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na ulinzi na usalama. Katiba hiyo izingatie misingi ya utawala bora pamoja na kutoa fursa sawa kwa makundi yote kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo na zitakazoibuka, na hivyo kuimarisha zaidi Muungano. Vilevile, mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa utaendelea kudumishwa ili kutoa fursa kwa wananchi kushiriki katika siasa, ikiwemo kuchagua viongozi wao kwa uhuru na haki.

*Diplomasia:* Tanzania imefanikiwa kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa kwa kujenga taswira nzuri na ushawishi mkubwa katika nyanja za kimataifa. Kwa kutumia vyombo vyake vya ulinzi na usalama, Tanzania imeweka historia kubwa duniani ya kudumisha amani na kutatua migogoro katika nchi zinazokabiliwa na migogoro. Aidha, viongozi wa Tanzania wamekuwa wakiongoza juhudi za kupatanisha migogoro inayotokea katika mataifa mengine. Tanzania ikiwa inaelekea katika miaka ijayo ya Muungano, inatarajia kuendeleza jitihada za kuimarisha amani na uelewano miongoni mwa mataifa mbalimbali kwa kutatua migogoro pale inapotokea na kutumia vyombo vyake vya usalama kurejesha amani pale inapohatarishwa. Aidha, katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje, msisitizo utawekwa zaidi kwenye diplomasia ya uchumi ili kuvutia mitaji na kuimarisha masoko kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.

**Kiuchumi**

*Kujenga Uchumi wa Kisasa:* Kutokana na fursa za kiuchumi zilizopo, matarajio ni kujenga uchumi wa kisasa na jumuishi kwa kutumia ipasavyo rasilimali zilizopo nchini, ili Watanzania wanufaike na ukuaji wa uchumi. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zenye uchumi wa kati duniani utakaokwenda sanjari na ukuaji wa kipato kwa kila mwananchi. Aidha, uchumi unatarajiwa ukue kwa kiwango cha tarakimu mbili na zaidi, na hivyo kuwaongezea wananchi kipato, ajira na kuwapunguzia umaskini. Pia, ni matarajio ya Watanzania kuwa mfumuko wa bei utadhibitiwa kwa kiwango kisichoathiri thamani halisi ya kipato cha mwananchi na ukuaji wa Pato la Taifa. Vilevile, ni matarajio ya Serikali kwa miaka ijayo kuwa kiwango cha uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa ajili ya mauzo nje ya nchi yataongezeka kiasi cha kuwezesha fedha za kigeni kupatikana kwa wingi na hivyo kuongeza akiba ya fedha hizo.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatarajiwa kutumia fursa ya kuwa lango kuu la biashara kwa Kanda ya Afrika ya Mashariki na Kati kwa kuimarisha biashara na nchi jirani, sanjari na kuongeza fursa za kibiashara baina ya Tanzania bara na Zanzibar. Vilevile, Taifa linatarajiwa kuendelea kukuza ubia na kuimarisha ushirikiano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa kuweka mbele maslahi ya nchi ili kunufaika zaidi na fursa za ushirikiano na nchi na kanda za uchumi ambazo Tanzania ni mwanachama.

**Kijamii na Kiutamaduni**

*Huduma za Jamii:* Tanzania inatarajia kuwa na huduma bora zaidi za kijamii kama vile afya, elimu, maji safi na salama na kuhakikisha zinapatikana kwa wakati wote kwa kila mwananchi. Serikali itahakikisha kuwa mazingira mazuri na wezeshi yaliyopo yanatumika ipasavyo kuvutia ushiriki wa Sekta Binafsi katika kujenga miundombinu ya kutoa huduma bora, endelevu na za uhakika kwa wananchi ikiwemo kujenga vyuo, shule, hospitali, na miundombinu ya maji. Serikali pia itaongeza au kuelekeza nguvu zake katika kujenga na kuimarisha huduma za kijamii kwa kutenga rasilimali fedha zaidi zinazoendana na ukuaji wa mapato yake. Vijana watakuwa nguzo muhimu katika kujenga Tanzania imara.

*Huduma za Utamaduni na Michezo:* Matarajio ya Serikali ni kuchukua hatua za kuendeleza lugha ya Kiswahili ili kutoa fursa za ajira kwa Watanzania. Vilevile, Tanzania inatarajia kutumia ngoma za asili, bidhaa za sanaa na mavazi ya asili, kama alama ya utambulisho wa jamii na Taifa na hivyo kujitangaza kimataifa. Aidha, fursa hizo pamoja na michezo na sanaa za maonesho, ufundi na uchoraji zitaongeza ajira na kipato kwa wananchi na kuwa chachu muhimu ya kuimarisha na kujenga miundombinu ya kukuza na kuendeleza sanaa nchini.

## Hitimisho

Taarifa hii imeeleza kwa muhtasari historia ya Tanganyika na Zanzibar kabla na baada ya kutawaliwa na wakoloni. Pia, inatoa sura halisi ya mwenendo wa harakati za ukombozi zilizofanikisha upatikanaji wa uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar; mambo ambayo yaliyotoa fursa kwa nchi hizo mbili kuungana na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muungano ambao umedumu kwa muda wa nusu karne.

Taarifa imeeleza utekelezaji wa mambo yaliyowekwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano, mambo yanayotekelezwa na pande mbili za Muungano kwa mujibu wa Sheria na ushirikiano katika mambo yasiyo ya Muungano.

Aidha, taarifa imebainisha mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 50 iliyopita licha ya changamoto zilizojitokeza. Katika kipindi hicho, mafanikio yaliyopatikana yamekuwa na manufaa makubwa kwa pande mbili za Muungano katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Mafanikio hayo ni matokeo ya kutumia vema fursa zilizojitokeza na kulifanya Taifa kupiga hatua zaidi za maendeleo katika kujenga na kuimarisha misingi ya kuheshimu utu, haki za binadamu, umoja, usawa, amani na mshikamano.

Changamoto kadhaa zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mambo ya Muungano zimeelezwa pamoja na hatua zilizochukuliwa kuzikabili na kuzipatia ufumbuzi ili kuhakikisha kuwa wananchi wa kila upande wa Muungano wananufaika na maendeleo yanayotokana nao.

Taarifa hii pia imebainisha matarajio ya miaka ijayo kuwa ni kuudumisha Muungano huo kwa kuulinda, kuuimarisha na kuendeleza amani na utulivu uliopo. Vilevile, kuhakikisha kwamba kiwango cha ustawi wa wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinaongezeka kutokana na kunufaika na rasilimali za Taifa. Inatarajiwa kwamba, hatua kubwa ya maendeleo itafikiwa na Taifa kwa kuongeza uzalishaji na tija katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, biashara na utalii. Halikadhalika, Taifa linatarajia kujitosheleza kwa wataalamu wenye ujuzi wa Sayansi na Teknolojia wa kiwango cha juu na kuingiza matumizi ya teknolojia ya kisasa katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

Matarajio hayo yatafikiwa kwa Serikali kuendelea kukuza ushirikiano na wananchi, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia katika kutekeleza mipango yake ya maendeleo. Hatua hiyo itakwenda sambamba na kuendelea kuimarisha na kujenga misingi imara ya uzalendo, umoja, amani na utulivu, matumizi bora ya rasilimali za nchi, siasa safi na uongozi bora wenye kuzingatia demokrasia, Sheria na haki za binadamu.

***Utanzania Wetu ni Muungano Wetu;***

***Tuulinde, Tuuimarishe na Kuudumisha.***

# ARTICLES OF UNION

BETWEEN

THE REPUBLIC OF TANGANYIKA

AND

THE PEOPLES' REPUBLIC

OF ZANZIBAR

ARTICLES OF UNION

b e t w e e n

THE REPUBLIC OF TANGANYIKA AND THE PEOPLES' REPUBLIC OF ZANZIBAR

# ARTICLES OF UNION

## between

## THE REPUBLIC OF TANGANYIKA AND THE PEOPLES' REPUBLIC OF ZANZIBAR

WHEREAS the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar, being mindful of the long association of the peoples of these lands and of their ties of kinship and amity, and being desirous of furthering that association and strengthening these ties and of furthering the unity of African peoples, have met and considered the union of the Republic of Tanganyika with the Peoples' Republic of Zanzibar:

AND WHEREAS the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar are desirous that the two Republics shall be united in one Sovereign Republic in accordance with the Articles hereinafter contained:-

It is therefore AGREED between the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar as follows:-

(i) The Republic of Tanganyika and the Peoples' Republic of Zanzibar shall be united in one Sovereign Republic.

(ii) During the period from the commencement of the union until the Constituent Assembly provided for in Article (vii) shall have met and adopted a Constitution for the united Republic [hereinafter referred to as the interim period] the united Republic shall be governed in accordance with the provisions of Articles (iii) to (vi).

(iii) During the interim period the Constitution of the united Republic shall be the Constitution of Tanganyika so modified as to provide for -

(a) a separate legislature and executive in and for Zanzibar as from time to time constituted in accordance with the existing law of Zanzibar and having exclusive authority within Zanzibar for matters other than those reserved to the Parliament and Executive of the united Republic;

(b) the offices of two Vice-Presidents one of whom (being a person normally resident in Zanzibar) shall be the head of the aforesaid executive in and for Zanzibar and shall be the principal assistant of the President of the United Republic in the discharge of his executive functions in relation to Zanzibar;

(c) the representation of Zanzibar in the Parliament of the united Republic;

(d) such other matters as may be expedient or desirable to give effect to the united Republic and to these Articles.

/ (iv)

(iv) There shall be reserved to the Parliament and Executive of the united Republic the following matters -

(a) The Constitution and Government of the united Republic
(b) External Affairs
(c) Defence
(d) Police
(e) Emergency Powers
(f) Citizenship
(g) Immigration
(h) External Trade and Borrowing
(i) The Public Service of the united Republic
(j) Income Tax, Corporation Tax, Customs and Excise
(k) Harbours, Civil Aviation, Posts and Telegraphs.

And the said Parliament and Executive shall have exclusive authority in such matters throughout and for the purposes of the united Republic and in addition exclusive authority in respect of all other matters in and for Tanganyika.

(v) The existing laws of Tanganyika and of Zanzibar shall remain in force in their respective territories subject -

(a) to any provision made hereafter by a competent legislature;

(b) to such provision as may be made by order of the President of the united Republic for the extension to Zanzibar of any law relating to any of the matters set out in Article (iv), and the revocation of any corresponding law of Zanzibar;

(c) to such amendments as may be expedient or desirable to give effect to the union and to these Articles.

(vi) (a) The first President of the united Republic shall be MWALIMU JULIUS K. NYERERE and he shall carry on the Government of the united Republic in accordance with the provisions of these Articles and with the assistance of the Vice-Presidents aforesaid and of such other ministers and officers as he may appoint from Tanganyika and Zanzibar and their respective public services.

(b) The first Vice-President from Zanzibar to be appointed in accordance with the modifications provided for in Article (iii) shall be SHEIKH ABEID KARUME.

(vii) The President of the united Republic in agreement with the Vice-President who is head of the Executive in Zanzibar shall -

(a) Appoint a Commission to make proposals for a Constitution for the united Republic.

/ (b)

(b) Summon a Constituent Assembly composed of Representatives from Tanganyika and from Zanzibar in such numbers as they may determine to meet within one year of the commencement of the union for the purpose of considering the proposals of the Commission aforesaid and to adopt a Constitution for the united Republic.

(viii) These Articles shall be subject to the enactment of laws by the Parliament of Tanganyika and by the Revolutionary Council of the Peoples' Republic of Zanzibar in conjunction with the Cabinet of Ministers thereof, ratifying the same and providing for the Government of the united Republic and of Zanzibar in accordance therewith.

IN WITNESS WHEREOF Julius K. Nyerere, the President of the Republic of Tanganyika, and Abeid Karume, the President of the Peoples' Republic of Zanzibar, have signed these Articles, in duplicate, at Zanzibar, on this 22nd. day of APRIL, , 1964.

Julius K. Nyerere

for the Republic of Tanganyika

Abeid Aman Karume

for the Peoples' Republic of Zanzibar

# Tanzania Tanzania

*Tanzania, Tanzania, nakupenda kwa moyo wote,*
*Nchi yangu Tanzania, jina lako ni tamu sana,*
*Nilalapo nakuota wewe, niamkapo ni heri mama wee,*
*Tanzania Tanzania, Nakupenda kwa moyo wote.*

*Tanzania, Tanzania, ninapokwenda safarini,*
*Kutazama maajabu, biashara nayo makazi,*
*Sitaweza kusahau mimi, mambo mema ya kwetu kabisa,*
*Tanzania Tanzania, Nakupenda kwa moyo wote.*

*Tanzania Tanzania, watu wako ni wema sana*
*Nchi nyingi zakuota, nuru yako hakuna tena*
*Na wageni wakukimbilia, ngome yako imara kweli wee,*
*Tanzania, Tanzania, heri yako kwa mataifa.*

*Nchi nzuri Tanzania, Karibu wasio kwao,*
*Wenye shida na taabu, hukimbizwa na walowezi,*
*Tanzania yawakaribisha, mpigane kiume chema wee,*
*Tanzania Tanzania, Mola awe nawe daima.*

# Wimbo wa Taifa

*Mungu ibariki Afrika,*
*Wabar iki Viongozi wake,*
*Hekima Umoja na Amani,*
*Hizi ni Ngao zetu,*
*Afrika na Watu wake,*
*Ibariki Afrika,*
*Ibariki Afrika,*
*Tubariki Watoto wa Afrika.*

*Mungu ibariki Tanzania,*
*Mungu ibariki Tanzania,*
*Dumisha Uhuru na Umoja,*
*Wake kwa Waume na Watoto,*
*Mungu ibariki,*
*Tanzania na Watu wake,*
*Ibariki Tanzania,*
*Ibariki Tanzania,*
*Tubariki Watoto wa Tanzania.*